# Kuwatambua wanafunzi walioko nje ya skuli na kuwasaidia katika kipindi cha elimu ya mpito

Moduli

# 3



# Mwongozo wa Mkufunzi

SMZ SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR

MADRASA EARLY CHILDHOOD PROGRAMME

NAD – The Norwegian Association of Disabled

nfu Norsk Forbund for Utviklingshemmede

EENET Enabling Education Network

# Kuwatambua wanafunzi walioko nje ya skuli na kuwasaidia katika kipindi cha elimu ya mpito

## Moduli ya Tatu

### Moduli ya Mkufunzi

Taasisi ya Elimu ya Zanzibar
S.L.P 840, Mazizini, Zanzibar info@zie.go.tz www.zie.go.tz
Simu: +255-24-2230193

Toleo la Kwanza 2022

Imetayarishwa na Enabling Education Network Machi, 2018

TEZ, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali 2022

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kwa ajili ya kuuza bila ya ruhusa ya Taasisi ya Elimu ya Zanzibar (TEZ). Matumizi yoyote ya toleo hili kwa kunakili, kutafsiri na kukitoa kwa njia ya kielektroniki bila ya idhini ya Taasisi ya Elimu ni kosa la kisheria na utashitakiwa.

Kazi hii imepewa leseni chini ya Creative Common Attribution – Shirika lisilo la kibiashara- 4.0 Leseni ya Kimataifa. Ili kuona kivuli cha leseni, tembelea http://creativecommons.org/licenses/by-nc-sa/4.0/

# Dibaji

Moduli za Elimu Mjumuisho zinelenga kuweka mazingira yaliyo sawa katika kuhakikisha kila mtu anashiriki vyema katika nyanja mbali mbali za kijamii, kiuchumi na kisiasa. Katika jamii ni vyema kila mmoja kuwa na mchango wake katika kutengeneza jamii husika. Utayarishwaji wa moduli za elimu mjumuisho utasaidia kufikia malengo yaliyowekwa katika mkutano wa Jomtien nchini Thailand (1990) ambako UNICEF ilipewa jukumu la kuhakikisha kuwa nchi zichukue hatua za kuondokana na utafauti wa elimu uliopo kati ya makundi ya vijana wenye mazingira magumu. Vile vile utayarishwaji wa Moduli za elimu mjumuisho zimeibuka kutokana na:

- Warsha ya mafunzo ya wakufunzi iliyotayarishwa na Diakonia, Palestina, Julai 2011.
- Elimu Mjumuisho: Mwongozo wa wakufunzi wa walimu, uliotayarishwa na Shirikisho la Kimataifa la Walemavu (HIF), Cambodia, 2011.
- Programu ya mafunzo ya wakufunzi iliyoandaliwa na Mfuko wa Watoto wa Umoja wa Mataifa (UNICEF), Macedonia, 2012–13.
- Programu ya mafunzo ya wakufunzi iliyoandaliwa na UNICEF, Libya, 2012– 2013.
- Utangulizi wa Elimu Mjumuisho: „Mwongozo wa Wakufunzi‟ ulioandaliwa na HIF, Liberia, 2012–13.

Napenda kutambua mchango wa Jumuiya za watu wenye ulemavu za Norway (Norwegian Association of Disabled, NAD na Norwegian Association for Persons with Developmental Disabilities, NFU) katika kusaidia kuandika moduli za elimu mjumuisho na kuhakikisha kuwa zinamuongoza vyema mwalimu katika kukidhi mahitaji ya Elimu Mjumuisho. Aidha napenda kutambua mchango wa Madrasa Early Childhood Program (MECP-Z) kwa kusimamia upitiaji wa moduli hizi. Mwisho natoa shukurani zangu za dhati kwa Kitengo cha elimu mjumuisho Zanzibar kwa kuzifanyia majaribio kwa hatua ya kwanza.

Ni matarajio yetu kuwa moduli za elimu mjumuisho zitatumika katika kuwaongoza walimu kukabiliana na mazingira jumuishi Zanzibar. Vile vile, wakufunzi wa vyuo vya ualimu na wahadhiri wa nyuo vikuu watatumia miongozo hii kwa ajili ya kuhakikisha walimu wanapata uzoefu katika kukabiliana na mazingira ya elimu mjumuisho Zanzibar.

__________________________

Khamis Abdulla Said
Katibu Mkuu
Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar.

# Shukurani

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali (WEMA) inatoa shukurani za dhati kwa Taasisi mbalimbali zilizohusika katika kutayarisha na kupitia Moduli hizi za elimu mjumuisho. Taasisi hizo ni: Taasisi ya Elimu ya Zanzibar, Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu, Kitengo cha Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha Zanzibar, Idara ya Mafunzo ya Ualimu, Vyuo vya Ualimu na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar. Aidha, Taasisi ya Elimu ya Zanzibar na Jumuiya ya makuzi ya Awali ya Mtoto zimehakikisha kuwa moduli zilizotayarishwa zinamuongoza vyema mwalimu katika kukidhi mahitaji ya mazingira ya elimu mjumuisho.

Aidha, Wizara inawashukuru waliotayarisha na kuzijaribu Moduli zote kwa zana zilizotayarishwa, na kujaribiwa na wafanyakazi wa Mtandao wa Kuwezesha Elimu na washauri kutoka maeneo mbalimbali barani Afrika, Asia na Ulaya kwa kipindi cha miaka 10 au zaidi.

Mwisho natoa shukurani zangu za dhati kwa wafadhili wa Elimu Zanzibar kupitia Jumuiya za watu wenye ulemavu za Norway kwa kuendelea kushirikiana na Wizara ya Elimu na

Mafunzo ya Amali (WEMA) katika kufanikisha uandaaji wa moduli hii.

___________________

Abdalla M. Mussa,
Mkurugenzi Mtendaji,
Taasisi ya Elimu ya Zanzibar.

# Yaliyomo

Yaliyomo ........................................................................................................ 6

Utangulizi........................................................................................................ 8

Kipindi cha 3.1: Utangulizi juu ya Wanafunzi Walioko Nje ya Skuli .................. 10

Kipindi cha 3.2: Mtazamo unaohusu haki juu ya tatizo la kuwa nje ya skuli: Mifumo ya sera na sheria za kitaifa na kimataifa ............................................ 17

Kipindi cha 3.3: Wanafunzi wa Zanzibar Walioko Nje ya Skuli: Ukubwa wa Tatizo ........................................................................................................ 20

Kipindi cha 3.4: Wanafunzi walioko nje ya skuli Zanzibar: Mikakati na Utatuzi wa changamoto za Kuwatambua Wanafunzi Walioko Nje ya Skuli ........................ 25

Kipindi cha 3.5: Kufahamu Elimu ya kipindi cha Mpito na Athari zake............. 36

Kipindi cha 3.6: Kuzifikia changamoto ........................................................... 41

Kipindi cha 3.7: Kuanzisha mpito wa elimu mjumuisho ndani ya skuli yetu..... 64

Vitendo vya Kuchangamsha ........................................................................ 70

Kielelezo nambari 3.1: Kufafanua mambo mbalimbali: Ni nani watoto walio nje ya skuli na kwanini wapo nje ya skuli? .................................................... 75

Kielelezo nambari 3.2: Orodha ya Vikwazo vya Kujifunza kwa Watoto ............ 87

Kielelezo nambari 3.3: Mfumo wa sera na sheria........................................... 88

Kielelezo nambari 3.4: Vikwazo vinavyolingana na haki .................................. 92

Kielelezo nambari 3.5: Kadi tisa za almasi – vikwazo vya watoto kuwepo skuli 98

Kielelezo nambari 3.6: Visa Mafunzo vya Watoto walio nje ya skuli................. 99

Kielelezo nambari 3.7: Mifano ya Karatasi za Uchunguzi............................... 101

Kielelezo nambari 3.8: Miongozo ya usaili ................................................... 102

Kielelezo nambari 3.9: Matokeo ya Utafiti – Sampuli A ................................. 104

Kielelezo nambari 3.10: Matokeo ya Utafiti – Sampuli B ............................... 105

Kielelezo nambari 3.11: Matokeo ya Utafiti – Sampuli c ............................... 106

Kielelezo nambari 3.12: Matokeo ya Utafiti – Sampuli D ............................... 107

Kielelezo nambari 3.13: Filamu ya ‘Kufika Skuli’ ya EENET, Mpango wa 3 na Maelezo yake.......108
Kielelezo nambari 3.14: Khadija mwenye Miaka 7 .......110
Kielelezo nambari 3.16: Rashid mwenye miaka 10.......112
Kielelezo nambari 3.17: Suleiman mwenye umri wa miaka 11.......113
Kielelezo nambari 3.18: Juma mwenye umri wa miaka 14 .......114
Kielelezo nambari 3.19: Shamila mwenye umri wa miaka 15.......115
Kielelezo nambari 3.20: Kanuni muhimu za mabadiliko .......116
Kielelezo nambari 3.21: Kadi za Changamoto.......117
Kielelezo nambari 3.22: Kadi za mikakati .......119
Kielelezo nambari 3.23: Ushauri wa Mipango ya Mpito wa Elimu – kutoka Nyumbani au Maandalizi kwenda Skuli ya Msingi.......124
Kielelezo nambari 3.24: Mafunzo ya Marafiki .......125
Kielelezo nambari 3.25: Muongozo wa Rafiki.......128
Kielelezo nambari 3.26: Kubali au Kataa .......130
Kielelezo nambari 3.27: Msaada wa Lugha kwa Wanafunzi wapya– Baadhi ya nukta kwa walimu.......131
Kielelezo nambari 3.28: Kadi za mapitio/tathmini.......133
Kielelezo nambari 3.29: Bango la Maendeleo Endelevu.......135
Kielelezo nambari 3.30: Mapitio ya maswali na vidokezo kwa kuisaidia skuli kujitathmini .......136
Kielelezo nambari 3.31: Kusaidia Mpito Jumuishi – Orodha ya dondoo kwa ajili ya Walimu.......138

Rejea.......139

# Utangulizi

Moduli hii ina malengo ya jumla mawili

Kwanza ni kuwapatia walimu na wadau wengine wanaohusika kama vile wafanyakazi wasaidizi wa skuli, maafisa elimu wa wilaya, wanajamii pamoja na wadau wengine wenye mtazamo mpana wa suala la wanafunzi walioko nje ya skuli katika vipengele vya kitaifa na kimataifa. Moduli hii pia, inabainisha vikwazo na mambo yanayopelekea wanafunzi kuweko nje ya skuli pamoja na mtiririko wa sababu na madhara yanayowapata kwa kuwepo nje ya skuli. Moduli hii inawasaidia washiriki kubaini, kuzingatia na kujadili vikwazo vinavyowakabili wanafunzi kitaaluma na kuelewa matatizo ya wanafunzi walioko nje ya skuli katika mtazamo mpana wa haki za binaadamu.

Lengo la pili ni kuimarisha njia muafaka kwa skuli ili kuhakikisha wanafunzi wote; walioko nje ya skuli na wanaokwenda skuli wanahudhuria skuli na wanapata msaada wanaouhitaji kwa njia rahisi na ya ufanisi wanapokuwa skuli. Kikawaida elimu ya kipindi cha mpito inajumuisha wanafunzi ambao wamehitimu, wanaoendelea na wapya katika taaluma. Wanafunzi walio wengi huanza skuli katika utaratibu maalumu uliopangwa. Kwa mfano, wanatoka mazingira ya nyumbani na kwenda kuanza elimu ya maandalizi, wanatoka maandalizi na kwenda elimu ya msingi, wanatoka elimu ya msingi wanakwenda sekondari na wanatoka sekondari wanakwenda elimu ya juu au katika ajira. Hata hivyo, kuna wanafunzi wengine wengi ambao wapo nje ya utaratibu huu uliopangwa. Wanafunzi hao ni kama hawa wafuatao:

- Wanafunzi walioko nje ya skuli ambao wana umri wa kwenda skuli lakini hawajapelekwa kabisa skuli au wana matatizo yanayowazuia kufika skuli. Kwa mfano, matatizo ya kifedha, au umbali wa masafa wa kuifikia skuli, au wana mahitaji ya ziada mfano mahitaji maalumu ya kujifunza na/au ulemavu ambao skuli haiwezi kumudu kuwa na mwanafunzi huyo.
- Wanafunzi ambao wanatoka katika familia zinazohamahama (mfano familia zinazotoka nchi moja kwenda nyengine au zinazotoka vijijini kwenda mijini kwa ajili ya kutafuta kazi au kuungana na wanafamilia)
- Wanafunzi ambao wamelazimika kuhama (kwa mfano, familia ambazo zimehamishwa kutokana na miradi ya maendeleo ya serikali au familia zinazohama kutokana na machafuko ya kisiasa).
- Wanafunzi ambao hawajajumuishwa na skuli zao.

Vilevile, elimu ya mpito inaweza kujitokeza ndani ya mazingira ya kujifunza. Kwa mfano, kutoka darasa moja kwenda jengine, au kutoka ngazi moja kwenda nyengine, au hata ndani ya siku moja, mfano kutoka somo moja kwenda jengine au kutoka mada moja kwenda nyengine, au kutoka muda wa masomo kwenda muda wa mapumziko na kinyume chake.

Hivyo, ni muhimu kusisitiza kwamba hakuna njia moja tu inayowafanya wanafunzi kuwa nje ya skuli. Hii ni kwa sababu, uzoefu wa kila mwanafunzi wa kuwa nje ya skuli, kutoanza skuli au kutoka skuli moja kwenda nyengine ni tafauti. Hivyo, kila skuli na jamii iliyoizunguka inapaswa kuendana na hali halisi na kuchukua hatua zinazotafautiana pamoja na kutoa suluhisho kulingana na mazingira yanayohusika.

Utaratibu wa upangaji wa vipindi katika moduli hii ufanyike kwa kurejea moduli nyengine za mafunzo katika mfululizo huu, kwa kuzingatia rejea maalumu ya; “Kuchunguza na kutambua mahitaji ya kujifunza” (Moduli ya 4), “Kubuni mpango binafsi wa kielimu na zana za kufundishia na kujifunzia” (Moduli ya 5), “Kukuza ushiriki wa wanafunzi” (Moduli ya 7). Maelezo mengine pia yanapatikana katika moduli ya ziada ya “Kuwazingatia wanafunzi wenye mahitaji maalumu”. Moduli hizo zinatoa Ushauri na muongozo juu ya kuyatambua mahitaji maalumu, na namna mahitaji hayo yanavyoweza kumtoa mwanafunzi nje ya mfumo wa elimu pamoja na vidokezo na mawazo ya kiutendaji kwa mwalimu ya kuwasaidia wanafunzi mwenye mahitaji maalumu katika skuli na mazingira ya darasani.

## Muda wa Mafunzo

Wakufunzi wanapaswa kuyabadilisha mafunzo haya ili yaendane na mazingira yao na muda waliopangiwa kwa mafunzo. Wakufunzi wanaweza kuamua kutotumia vitendo vyote au kufupisha baadhi ya vitendo ikiwa muda ni mchache au kurefusha vitendo ikiwa walimu wanahitaji msaada zaidi katika kuifahamu mada fulani.

Ikiwa vitendo vyote vitatumiwa bila kubadilishwa, kufupishwa au kurefushwa, moduli hii itahitaji saa 13 mpaka 15 za mafunzo ambazo ni wastani wa siku 3 kutegemeana na ukubwa wa muda wa mafunzo, idadi na ukubwa wa muda wa mapumziko na mambo mengine.

# Kipindi cha 3.1: Utangulizi juu ya Wanafunzi Walioko Nje ya Skuli

Wanafunzi wengi ulimwenguni hawahudhurii skuli. Wanafunzi hao hujulikana kama wanafunzi walioko nje ya skuli. Kuna mambo mengi ambayo yanawazuia kuhudhuria skuli kama vile umbali wa kwenda na kutoka skuli, umaskini, migogoro na maafa.

Kipindi hiki kimedhamiria kutoa mtazamo mpana wa suala la wanafunzi walioko nje ya skuli kitaifa na kimataifa. Kipindi hiki kitazungumzia vikwazo vinavyowakabili wanafunzi katika kujifunza kwa ujumla na pia kwa kupitia mifano mahsusi ya visa mafunzo.

## Kitendo cha 3.1a: Vikwazo Vinavyowakabili Wanafunzi katika Kujifunza

Kikuu

Muda: Dakika 30

Kitendo hiki kitawasaidia washiriki kuzingatia na kujadili vikwazo vya wanafunzi katika kujifunza. Vilevile, kitendo hiki kitaonesha ufahamu wa washiriki juu ya vikwazo vinavyowakabili wanafunzi walioko nje ya skuli.

Mkufunzi awatake washiriki kukaa katika vikundi. Kila kikundi kichague katibu wa kuweka kumbukumbu za majadiliano. Washiriki katika vikundi vyao wajadiliane na waandike vikwazo vinavyowasababisha wanafunzi kuwa nje ya skuli. Kwa kila kikwazo au sababu inayomfanya mwanafunzi kuwa nje ya skuli, wafikirie mifano halisi. Kwa mfano, ikiwa umaskini au mahitaji ya ziada ya kujifunza ndio vikwazo, washiriki wanapaswa kutoa mifano halisi ya vikwazo hivi.

Baada ya dakika 15, mkufunzi awatake washiriki kwa kila kikundi kutoa mrejesho na kuweka kumbukumbu za jawabu katika chati mgeuzo. Ikiwa kikwazo fulani kimetajwa, kikundi kinachofuata kinatakiwa kutoa kikwazo chengine (wasirejee kikwazo ambacho kimeshajadiliwa). Vilevile, kila kikundi kitoe mifano halisi itakayothibitisha jawabu zao. Kisha, mkufunzi aoneshe mrejesho ulioandikwa katika chati kwa ajili ya kuwawezesha washiriki kupata marejeo ya kipindi kilichopo na vipindi vyengine vinavyofuata.

Mkufunzi anaweza kurejea vipengele vifuatavyo wakati au baada ya majadiliano. Matokeo ya utafiti wa Elimu Mjumuisho Zanzibar wa mwaka 2020 uligundua sababu kadhaa zilizopelekea wanafunzi kutohudhuria skuli, kama hizi zifuatazo;

- Mitazamo ya watu juu ya mahitaji ya ziada ya kujifunza, jinsia, ukabila, dini na utamduni,
- Upungufu wa vifaa visaidizi na huduma kwa wanafunzi wenye mahitaji ya ziada,
- Uhamaji wa watu unaosababishwa na migogoro na maafa ikiwemo vita na mabadiliko ya hali ya hewa
- Kuishi mbali na skuli,
- Mazingira yasiyosalama ya kujifunza au kutoweza kufika skuli salama,
- Changamoto za kiafya,
- Changamoto ya Matumizi ya lugha (matumizi ya lugha nyengine kinyume na lugha mama ya wanafuzi inaweza kuwa ni kikwazo),
- Kutoka katika makundi hatarishi na yaliyotengwa ambayo yanapelekea kutopata huduma za kiafya na kielimu,
- Umasikini na kinyume chake
- Ajira za watoto na Uyatima.

## Kitendo cha 3.1b: Mchezo wa "Lakini kwa nini" – kufikiri kwa makini

Kikuu

Muda: Dakika 10

Kitendo hiki kitawashirikisha washiriki katika kufikiria kwa makini kuhusu **mtiririko wa sababu na matukio** yanayopelekea wanafunzi kuwa nje ya skuli.

Mkufunzi awasimulie kisa mafunzo kifuatacho washiriki:

"Hii ni hadithi inayomhusu msichana mwenye miaka 8 anayeitwa Maryam. Maryam anaishi katika Kijiji kilichojitenga. Kijiji anachoishi Maryam hakina skuli na hivyo hajawahi kwenda skuli. Jee kwa nini Maryam yupo nje ya skuli?"

Kisha, mkufunzi aongoze mjadala ambao utawashajihisha washiriki kufikiria sababu ambazo zimemsababisha Maryam kuwa nje ya skuli. Kwa mfano:

Jawabu ya mshiriki: "Kwa sababu hakuna skuli Kijijini kwao."

Swali la mkufunzi: "**Lakini kwa nini** hakuna skuli kijijini kwao."

Jawabu ya mshiriki: "Labda kwa sababu Kijiji chao ni maskini"

Swali la mkufunzi: "**Lakini kwa nini** Kijiji chao ni maskini?"

Jawabu ya mshiriki: "Kwa sababu Kijiji chao kipo mbali sana."

Swali la mkufunzi: "**Lakini kwa nini** sehemu za mbali za milimani ni maskini?"

Mkufunzi ataendelea na mtiririko wa kuuliza maswali ili kuwawezesha washiriki kuchambua kwa umakini sababu za kijamii, kimazingira na kisiasa zinazomsababisha Maryam kuwa nje ya skuli. Mawazo ya washiriki yaandikwe katika chati au ubao.

Lengo la mchezo huu ni kuwawezesha washiriki kutoa sababu nyingi zinazowezekana zinazomfanya Maryam kuwa nje ya skuli. Hii inakusudiwa kuwasaidia washiriki kufikiri kwa kina kuhusu sababu za ziada zinazowapelekea wanafunzi kuwa nje ya skuli.




*Wakufunzi wakuu wakicheza mchezo wa "lakini kwa nini"*

**[Maelezo ya picha: Mtu mmoja amesimama upande wa kushoto wa picha akielekea kikundi cha watu waliokaa. Mtu huyo ameweka mikono yake mbele yake kwa pamoja. Watu wengine wanamtazama na wengine wanatabasamu.]**

Kisha mkufunzi anaweza kuwaelezea washiriki:

"Mchezo wa 'Lakini kwa nini?' ni kitendo kinachotusaidia kuchambua vyanzo vya matatizo mbalimbali. Kutambua chanzo cha tatizo na kufahamu namna chanzo cha tatizo na tatizo vinavyowiyana huweza kutusaidia kupata ufumbuzi wa tatizo hilo. Huu ni mfano wa kufikiri kwa makini. Huu ni mchezo wenye faida sana kwetu kwani hutuwezesha kufikiria kwa kina zaidi vikwazo mbalimbali vinavyowapelekea wanafunzi kuwa nje ya skuli. Hivyo, mkufunzi anaweza akautumia mchezo huu kufundishia wanafunzi wake. Mkufunzi anaweza kuwataka washiriki kufikiria tatizo la wanafunzi walioko nje ya skuli, lakini matatizo na mambo mengine pia yataweza kujitokeza.

Mkufunzi amalizie kitendo hiki kwa kutaka mrejesho kutoka kwa walimu kuhusiana na mchezo wa 'Lakini kwa nini' na kuandika michango ya walimu katika chati au ubao.

## Kitendo cha Ziada

Zaida

Muda: Dakika 20

**Kitendo cha 3.1b** kinaweza kufanywa ikiwa kuna muda wa kutosha. Washiriki watapewa dakika tano (5) ili kila mmoja aandae hadithi ya **'Lakini kwa nini'** kwa kutumia mfano wa hadithi ya Maryam.

Washiriki watagawiwa katika **jozi** na kutakiwa kucheza mchezo wa 'Lakini kwa nini' kwa zamu. Washiriki wanatakiwa kuchunguza hatua za mchezo huu na kuzingatia namna maswali yanavyoulizwa na kujibiwa, na namna watakavyoendeleza mtiririko wa kuuliza maswali na jawabu. Kitendo hiki kitafanywa kwa dakika kumi (10).

Mwisho, mkufunzi aongoze mrejesho wa kipindi kwa dakika tano (5).

## Kitendo cha 3.1c: Kuwatambua wanafunzi walioko nje ya skuli – vikwazo na sababu zao

Kikuu

Muda: Dakika 20

**Kielelezo nambari 3.1**

**Utambuzi wa mambo: Ni wepi wanafunzi walioko nje ya skuli na kwa nini wapo nje ya skuli?**

Mkufunzi ahakikishe anafahamu maudhui yaliyomo katika **Kielelezo nambari 3.1** kabla hajaongoza kipindi hiki. Washiriki wanaweza kupewa **Kielelezo nambarinambari 3.1** kwa ajili ya kusoma kwa muda wao wenyewe baada ya mafunzo.

**Kielelezo nambari 3.2**

**Vikwazo vinavyowakabili wanafunzi katika kujifunza**

Washiriki wapewe nakala ya **Kielelezo nambari 3.2** kinachoonesha baadhi ya aina za vikwazo vinavyowasababisha wanafunzi kuwa nje ya skuli.

Vilevile, mkufunzi anaweza kuwataka washiriki kuandika mfumo wa aina tatu kuu za vikwazo katika chati na kuhakikisha kuwa washiriki wanaacha nafasi ya kutosha ya kuandika mifano katika kila aina ya kikwazo.

Mkufunzi awatake washiriki katika vikundi kurejea vikwazo ambavyo viliorodheshwa katika **Kitendo cha 3.1a** na kujadili kwa dakika 5 vikwazo ambavyo vinaendana na aina hizi. Kisha mkufunzi aongoze mjadala kwa kuhakikisha kwamba kila aina ya kikwazo kimejadiliwa pamoja na kutoa mifano halisi. Mifano hii inaweza kutokana na uzowefu wa washiriki, uzowefu wa mkufunzi pamoja na dondoo kutoka katika **Kielelezo nambari 3.2**.




*Wakufunzi wakuu wakipitia aina za vikwazo*

**[Maelezo ya picha: Karatasi zimebandikwa ubaoni. Baadhi zimepewa majina ya aina za vikwazo (kwa mfano, wingi wa wanafunzi, ukosefu wa vifaa). Wanaume wawili wanaendelea na kazi ya kubandika orodha ya vikwazo katika ukuta.]**

Vilevile mkufunzi anaweza kufanya uwasilishaji kwa mujibu wa maelezo yanayopatikana katika Kielelezo nambari 3.2 kutegemea kiwango cha maudhui ambacho kimejadiliwa.

Inaweza kuwa ni muhimu kwa mkufunzi kutoa maelezo ya awali juu ya kitendo hiki kwamba kitaangazia mambo yanayowahusu wanafunzi walioko nje ya skuli kimataifa ili kuwasaidia washiriki kujifunza mambo mengi yanayowazuia wanafunzi kuhudhuria skuli duniani. Baadae, kutakuwa na uchunguzi wa kina wa vikwazo vinavyoendana na mazingira ya Zanzibar katika mafunzo haya. Hii ni kwa sababu kupata ufahamu wa mambo katika mazingira mengine duniani kunasaidia sana kuvifahamu vizuri vikwazo katika mazingira yetu.

## Kitendo cha Ziada

Zaida

Muda: Dakika 20-30

Kitendo hiki kitawasaidia washiriki kutafakari kiasi kikubwa cha taarifa kilichowasilishwa na kujadiliwa katika vitendo vilivyopita kwa kutoa ufahamu wao juu ya wanafunzi walioko nje ya skuli.

Washiriki watafanya kazi katika vikundi vidogovidogo. Kila kikundi kiwe na karatasi safi, upande wa juu wa karatasi hiyo waandike:

**“Wanafunzi walioko nje ya skuli ni: …”**

Kila mshiriki katika kikundi anatakiwa akamilishe sentensi hii bila ya kumuangalia mwenzake. Mshiriki wa kwanza ataandika maana yake kisha ataikunja karatasi ili mshiriki mwengine asione kilichoandikwa. Kisha mshiriki wa pili naye ataandika maana yake nakuikunja karatasi na kumpa mwengine mpaka washiriki wote katika kikundi wamalize. Baada ya kila mshiriki kuandika maelezo yake, kikundi kimoja wataikunjua karatasi na kusoma sentensi zote. Kisha, kwa kupitia sentensi zote, washiriki watoe sentensi moja ya ujumla inayoelezea wanafunzi walioko nje ya skuli.

Mkufunzi awaongoze washiriki kujadiliana kwa pamoja ili kupata maana moja ya wanafunzi walioko nje ya skuli na iandikwe katika chati kwa matumizi ya baadae.

Mkufunzi ahakikishe washiriki wote wanafahamu vizuri maana ya wanafunzi walioko nje ya skuli kuwa ni wanafunzi ambao:

- hawajawahi kuhudhuria skuli, au
- wameacha skuli, au
- wakati mwengine wanakwenda skuli, na baadhi ya wakati hawendi.

## Kipindi cha 3.2: Mtazamo unaohusu haki juu ya tatizo la kuwa nje ya skuli: Mifumo ya sera na sheria za kitaifa na kimataifa

Vitendo vilivyopita viliwasaidia washiriki kufahamu na kutafakari juu ya vikwazo vinavyowafanya wanafunzi kuwa nje ya skuli. Vikwazo hivi vinahitaji kutafutiwa ufumbuzi. Katika ufumbuzi huu, ni muhimu kufahamu matatizo ya kuwa nje ya skuli kwa mfumo mpana wa haki za binaadamu.

Vikwazo vingi huwafanya wanafunzi kuwa nje ya skuli ijapokua elimu ni haki ya msingi kwa wanafunzi wote. Elimu ni nyenzo muhimu kwa maendeleo ya binaadamu. Nchi nyingi duniani huchukua dhamana ya kisheria juu ya haki ya kupata elimu ya msingi na kuna ahadi mbalimbali za mifumo ya sera na sheria za kimataifa, kikanda na kitaifa zenye mamlaka ya jambo hili. Hivyo, ni muhimu kutambua mifumo ya sera na sheria ambazo zinazohusika na haki za kielimu za wanafunzi.

Haki za mtoto kupata elimu zimeanzishwa ikiwa ni mfululizo wa maazimio ya kimataifa kama vile Mkataba wa Umoja wa Mataifa unaotokana na Azimio la Kimataifa la Haki za Kibinaadamu wa mwaka 1948. Mkataba huu umebainisha haki za watoto mwaka 1989. Juhudi nyengine zilizoanzishwa kusaidia haki hii ni zile harakati za Elimu kwa Wote, Malengo ya Maendeleo ya Milenia na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa.

Kwa upande wa Zanzibar, sera ya serikali juu ya 'fursa sawa ya elimu ya kujitosheleza' imehakikishwa chini ya kifungu cha 10(6) cha katiba ya Zanzibar[1]. Vilevile chini ya mabadiliko ya sheria ya elimu ya mwaka 1993 ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Dira ya Zanzibar ya mwaka 2020 ni mpango wa ujumla unaoelekeza sera ya mipango ya maendeleo ili kuondoa umaskini katika jamii. Lengo kuu la dira ya elimu ya Zanzibar ya mwaka 2020 ni 'kujumuisha upatikanaji wa usawa wa elimu bora na mafunzo ya ujuzi.'[2]

---

[1] Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar 2006 Katiba ya Zanzibar yamwaka 1985, Zanzibar: Machapisho ya Chuo cha elimu, Katiba ya Zanzibar

[2] Ministry of Education and Vocational Training Zanzibar 2017 *Zanzibar Education Development Plan II 2017/18 – 2021/2* Accessed February 2022 https://planipolis.iiep.unesco.org/en/2017/zanzibar-educationdevelopment-plan-ii-20172018%E2%80%9320212022-6391

Kufahamu kuwa elimu ni haki na sio anasa maana yake ni kufanya kazi ili kutatua matatizo ya wanafunzi walioko nje ya skuli ni lazima na ni wajibu, sio hiyari.

## Kitendo cha 3.2a: Ukumbusho kuhusu Mifumo ya Sera na Sheria

Kikuu

Muda: Dakika 15

Mkufunzi awaulize washiriki iwapo wanafahamu mifumo ya sera za kimataifa, kikanda na kitaifa au mifumo ya sera na sharia za ndani zinazozungumzia haki za kielimu za wanafunzi. Majibu yao yaandikwe katika chati. Mazoezi haya yatumie kiasi cha dakika tano (5).

Kisha washiriki wapewe **Kielelezo nambari 3.3** watakisoma kimyakimya wao wenyewe. Mazoezi haya yachukuwe kiasi cha dakika 5-10.

**Kielelezo nambari 3.3** **Mifumo wa Sera na Sheria**

Baada ya washiriki kumaliza kusoma, mkufunzi awaulize kwa kina iwapo wana maswali au mambo ambayo wanataka kujadili (dakika 5).

## Kitendo cha 3.2b: Kuoanisha Vikwazo na Haki

Kikuu

Muda: Dakika 25

Kitendo hiki kitawashirikisha washiriki katika kujenga uhusiano wa haki za mwanafunzi za kielimu na vikwazo vinavyomzuia kushiriki katika elimu. Vile vile kitendo hiki kitawasidia walimu kuunganisha ufahamu wa vikwazo wanavyokumbana navyo wanafunzi wakiwa skuli pamoja na kufahamu vikwazo na haki zinazozungumziwa na makubaliano ya kimataifa.

Kitendo hiki kinatumia mkataba unaohusiana na mtoto wa Umoja wa Mataifa juu ya haki za mtoto. Pia, mkufunzi awatake washiriki waangalie makala katika mikataba ambayo inazungumzia elimu na kuoanisha vikwazo anavyopitia mwanafunzi akiwa skuli na makala inayozungumzia utatuzi wake. Kwa kutumia

mkataba wa Umoja wa Mataifa, itapelekea mazoezi haya kufanikiwa zaidi. Vilevile, itaonesha mfano wa mbinu za kutumiwa katika kujadili haki za mtoto na elimu ambazo washiriki wanaweza kutumia katika kufundishia.

Mkufunzi awape washiriki **Kielelezo namab 3.4**. Washiriki wafanye kazi katika vikundi vidogovidogo na kusoma toleo linalohusiana na mtoto la Umoja wa Mataifa la haki za mtoto.

**Kielelezo nambari 3.4** **Kuoanisha Vikwazo na Haki**

Kisha washiriki waainishe makala zinazohusiana na elimu. Baadhi ya makala katika mkataba zimezungumzia moja kwa moja masuala ya elimu, nyengine hazijazungumzia moja kwa moja na baadhi hazijazungumzia kabisa.

Mwisho, vikundi vijaribu kuoanisha vikwazo vilivyoainishwa katika **Kipindi cha 3.1**, ambavyo vinawasababisha wanafunzi kuwa nje ya skuli kwa msaada wa Makala ya mkataba ambao umeyazungumzia mambo hayo. Vikwazo hivi vilikusanywa na mkufunzi katika chati na kuoneshwa kwa washiriki mwisho wa **Kitendo cha 3.1a**. Washiriki watumie nafasi chini ya kila Makala katika **Kielelezo nambari 3.4** ili kuandika jawabu zao. Vilevile, washiriki wanaweza kutumia **Kielelezo nambari 3.1** na **Kielelezo nambari 3.2** iwapo watataka kujikumbusha kwamba baadhi ya uwiano kati ya vikwazo na haki unaonekana waziwazi wakati uwiano mwengine haupo wazi na hivyo huhitaji ufafanuzi wa ziada.

Mkufunzi awe anapita katika vikundi akitizama na kunukuu dondoo muhimu za majadiliano. Dondoo hizi zinaweza kutumika baadae mwisho wa somo. Baada ya dakika 10-15, mkufunzi aongoze mrejesho wa kipindi akiwataka washiriki kila kikundi kutoa mifano tafauti ya vikwazo pamoja na haki katika vikundi vyao. Mkufunzi ataandika jawabu katika chati. Pia, atawataka washiriki kuzingatia hatua za kufanya mazoezi haya. Ili kufanikisha hili, mkufunzi anaweza kutaja dondoo muhimu zilizojadiliwa au mambo ambayo washiriki hawakukubaliana wakati wa kazi zao za vikundi.

# Kipindi cha 3.3: Wanafunzi wa Zanzibar Walioko Nje ya Skuli: Ukubwa wa Tatizo

Kuna sababu nyingi zinazopelekea wanafunzi wa Zanzibar kuwa nje ya skuli, kutohudhuria kikawaida au kutoroka baada ya kuhudhuria kwa muda. Tukiangalia dhana ya kimataifa ya wanafunzi walioko nje ya skuli, kipindi hiki kitawasaidia washiriki kufikiri kwa makini kuhusu wanafunzi wa Zanzibar walioko nje ya skuli. Kipindi hiki pia kitafanya mapitio ya kuziainisha changamoto na mambo yanayopelekea matatizo ya wanafunzi kuwa nje ya skuli na kufikiria utatuzi wake.

## Kitendo cha 3.3a: Kwa Nini Wanafunzi Wako Nje ya Skuli Zanzibar?

Kikuu

Muda: Dakika 45

Kipindi hiki kinakusudia kuwasaidia washiriki kufikiria sababu ya changamoto na vikwazo vya ujifunzaji wanavyokutana navyo wanafunzi wa Zanzibar.

Mkufunzi awashauri washiriki kufanyakazi katika vikundi vidogovidogo. Kila kikundi kitapewa bahasha ya vipande vilivyokatwa vya kadi 9 za almasi kutoka katika **Kielelezo nambari 3.5**. Kadi zikatwe vizuri na inapendelewa ziingizwe ndani ya bahasha.


**Kielelezo nambari 3.5** — **Kadi 9 za Almasi– Changamoto za Wanafunzi waliopo Skuli**

Kila kikundi kinapaswa kuchagua kadi 9 za almasi na kuzipanga juu ya meza kwa muundo wa almasi unaoonesha mpangilio wa vikwazo vikubwa zaidi kwenda vikwazo vidogo zaidi vinavyowasababisha wanafunzi kuwa nje ya skuli Zanzibar. Ile changamoto au kikwazo kikubwa zaidi kitawekwa juu na kile kikwazo kidogo kitawekwa chini. Washiriki wakubaliane na mpangilio wa kadi hizo katika kundi lao. Mazoezi haya yachukue dakika 15.

Mkufunzi anatakiwa kuchora mfano wa mchoro wa almasi 9 kwenye chati au ubaoni ili kuwaonesha walimu mfano wa namna ya kupangilia kadi hizo.

**Mpangilio wa mchoro wa almasi 9**

Changamoto kubwa zaidi



Changamoto ndogo zaidi



*Washiriki wa Zanzibar wakifanya kazi ya kupanga mchoro wa almasi 9*

**[Maelezo ya picha: Vipande kadhaa vya karatasi vipo juu ya meza. Vinaelezea vitu kama vile lugha na mtazamo wa watu juu ya ulemavu. Ipo mikono minne juu ya meza. Mkono mmoja ndio unaotembea na kuvipanga vipande vya karatasi.]**

Kielelezo nambari 3.5 kimekusanya kadi zaidi ya tisa, kwa hivyo washiriki wanatakiwa kuchagua kadi zipi wanapaswa kuzijumuisha. Vikwazo vilivyochapishwa katika mchoro wa almasi 9 vinalingana na vya Vielelezo vya nambari 3.1 na 3.2. Pia kuna kadi ambazo hazina maandishi katika kila kipeperushi. Mkufunzi ahakikishe kila kikundi kimepata kadi ambazo hazina maandishi. Ikiwa watapenda, vikundi vinaweza kuandika changamoto tafauti katika kadi tupu na kuzitumia pamoja na walizonazo katika muundo wao wa almasi 9. Pia wanaweza kutengeneza kadi nyengine kama itahitajika. Mazoezi haya yatatumia dakika 15 – 20.

Vikundi vitakapomaliza kupanga kadi zao, washiriki wote watatembea kwenye vikundi vyengine meza hadi meza; kujadiliana kwa nini wamezipanga kadi hizo katika mpangilio unaoonekana. Mazoezi haya yatachukua dakika 20 – 25.



*Wakufunzi wakuu wakijadili mpangilio wa kila kikundi wa almasi 9*

**[Maelezo ya picha:  Watu 14 wanawake na wanume wako katika meza moja, wengine wamesimama na wengine wamekaa. Juu ya meza kuna kadi zilizoandikwa na kupangwa katika muundo wa almasi, mwanamke anaonesha kadi na wengine wanatazama kadi hizo.]**

Mkufunzi ashirikiane na washiriki wote wanapotembelea kwenye makundi ili kuwashajihisha kuuliza maswali na kusaidia mijadala iende vizuri.

Ni vyema kutafuta njia za kuweka kumbukumbu ya mpangilio wa kila kikundi wa almasi 9 na kuzijadili kwa pamoja. Mfano kupiga picha ya mpangilio wa almasi 9, na matarajio ya kikundi katika chati au ubaoni.

## Kitendo cha 3.3b: Kuchunguza Kisa Mafunzo cha kwanza

Kikuu

Muda: Dakika 35

Washiriki wakae katika vikundi vidogovidogo na wasome Kisa Mafunzo cha kwanza walichowekewa katika **Kielelezo nambari 3.6** kinachomhusu mwanafunzi ambae yupo nje ya skuli katika mazingira ya Zanzibar.

**Tanbihi:**
Mkufunzi aoneshe visa mafunzo tafauti kwa kila kikundi ili kuhakikisha washiriki wameweza kuviangalia visa mafunzo vingi. Mkufunzi anaweza kushauriana katika kubadilishana majina ya wahusika wa kisa mafunzo ili kuendana na mazingira yao.

**Kielelezo nambari 3.6** **Kisa Mafunzo cha Wanafunzi Walioko Nje ya Skuli**

Katika makundi yao washiriki wabainishe:

- Kwa nini wanafunzi wako nje ya skuli? Mfano ikiwa wanafunzi wametoroka skuli, wanahudhuria kwa vipindi fulani au hawajawahi kupelekwa skuli kabisa).
- Ni vikwazo gani vinavyowakabili wanafunzi hao katika mazingira yao ya kujifunza. Ikiwemo mambo yanayohusiana na familia za wanafunzi, maeneo, ukabila, taarifa zao za awali katika elimu na mengineo.
- Vipi changamoto hizo zinaweza kutatuliwa; ni yepi matarajio tatuzi?

Majadiliano yasizidi dakika 15. Ikiwa kikundi kimemaliza kujadiliana kuhusu kisa mafunzo walichopewa, wanaweza kuchagua kisa mafunzo chengine.

Katika kikao cha washiriki wote, kikundi kimoja kitoe mrejesho ambao umeainishwa katika chati. Vikundi vyengine vitaongeza maoni yao. Mazoezi

haya yatarejewa na vikundi vyengine hadi vikundi vyote viweze kutoa maelezo ya visa mafunzo walivyovijadili katika vikundi vyao.

## Kitendo cha 3.3c: Kuchunguza Kisa Mafunzo cha pili

Kikuu

Muda: Dakika 35

Washiriki wanatakiwa kupeana mifano ya wanafunzi walioko nje ya skuli za Zanzibar waliowahi kuwa nao au kujua taarifa zao. Jawabu ziandikwe kwenye chati au ubaoni na zitumike kuchangamsha majadiliano yanayohusu wanafunzi walioko nje ya skuli za Zanzibar. Mjadala huo utumie dakika 10.

Katika hatua inayofuata, washiriki wafanye kazi kwa vikundi na waandike kisa mafunzo kifupi kinachoelezea mwanafunzi ambae yupo nje ya skuli. Mazoezi haya yatumie dakika 10 – 15.

Kisa mafunzo ni muhimu kihusishwe na mazingira halisi ya wanafunzi walioko nje ya skuli ambao washiriki wanawaelewa.

Kila kisa mafunzo kiandikwe kwenye chati ili kiweze kuwekwa ubaoni au ukutani ili washiriki waweze kukijadili:

- Kwa nini mwanafunzi yupo nje ya skuli. Na ikiwa mwanafunzi ametoroka skuli au hajawahi kupelekwa skuli kabisa, na
- Kuna vikwazo gani vinavyokabili ujifunzaji wa mwanafunzi, ikiwemo maelezo yoyote yanayohusiana na familia ya mwanafunzi, eneo analoishi, ukabila, taarifa zake za awali za kielimu na mengineyo.

Ikiwa mwanafunzi ametoroka skuli taarifa zake na taarifa za skuli yake ya awali zioneshwe katika kisa mafunzo hicho.

Wakati washiriki wakiendelea kuvifanyia kazi visa mafunzo vyao, mkufunzi anatakiwa atembee ndani ya darasa ili kuchunguza na kuweka kumbukumbu juu ya kisa mafunzo ambacho kitawavutia washiriki na hivyo kukijadili kwa pamoja.

Visa mafunzo vipya inabidi vioneshwe na vijadiliwe na washiriki wote.

# Kipindi cha 3.4: Wanafunzi walioko nje ya skuli Zanzibar: Mikakati na Utatuzi wa changamoto za Kuwatambua Wanafunzi Walioko Nje ya Skuli

Kuwatafuta na kuwatambua wanafunzi walioko nje ya skuli kunaweza kuwa na changamoto mbalimbali. Hata hivyo, skuli na watendaji wengine wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali (mfano, Afisa Elimu Wilaya) wanaweza kuzitumia skuli kupata taarifa za awali zitakazosaidia kuwatambua wanafunzi hao. Taarifa hizo zinaweza kuwasaidia watendaji wa elimu wa ngazi zote kuzifahamu sababu za wanafunzi kutokuhudhuria skuli. Sambamba na kubuni mikakati na njia za utatuzi wa changamoto zilizopo katika kuhakikisha watoto wote wanapata haki yao ya elimu ipasavyo.

Vipindi vilivyopita, tuliangalia wanafunzi walioko nje ya skuli katika mtazamo wa kimataifa, kipindi hiki kinawasaidia washiriki kuwafikiria wanafunzi hao. Kwa hivyo katika kipindi hiki washiriki wataweza kugundua matatizo yanayowakabili wanafunzi hao na kutafuta njia muafaka za utatuzi wa changamoto hizo ili wanafunzi hao waweze kurejea skuli na kupata elimu bora na endelevu.

## Kitendo cha 3.4a: Kuwatafuta na Kuwatambua Wanafunzi Walioko Nje ya Skuli

**Kikuu**

Muda: Dakika 30

Ili kuyajua matatizo yanayowakabili wanafunzi walioko nje ya skuli, kwanza ni muhimu kuwatafuta na kuwatambua. Kitendo hiki kimedhamiria kuwataka washiriki wazingatie changamoto zinazojitokeza katika kuwatafuta na kuwatambua wanafunzi hao na kuweka mikakati inayohusu namna ya kufikia utatuzi wa changamoto hizo.

Mkufunzi awatake washiriki wafikirie kwa makini, kisha watoe mawazo yao kuhusu namna ya kuwatafuta na kuwatambua wanafunzi walioko nje ya skuli. Wakati wa kufanya mazoezi haya mkufunzi awatake washiriki wazingatie:

- Ni pahali gani wanafunzi hawa wanapatikana au wanaishi? Mkufunzi awachoree washiriki ramani ya jamii inayohusika katika chati ili iwasaidie.

- Kwa nini wanafunzi hao wako nje ya skuli?
- Nani anayewafahamu na anayejua kwamba wanafunzi hao wapo nje ya skuli?
- Ni nani aliyeweka njia bora za kuwatafuta na kuwatambua wanafunzi hao?
- Ni mamlaka gani zenye jukumu la kusaidia kuwatafuta na kuwatambua wanafunzi walioko nje ya skuli? Je, ni polisi? Wafanyakazi wa kijamii? Wizara ya Afya? Ustawi wa Jamii, wazee au watoto wenyewe?

Mkufunzi aweke kumbukumbu katika chati au ubao. (Dakika 10 hadi 15).

Kisha mkufunzi awatake washiriki wafanye kazi kwa vikundi katika kukizingatia kisa mafunzo kilichotengenezwa kwenye **Kipindi cha 3.3c**. Kutokana na kisa mkasa hiki, washiriki waorodheshe mikakati ya kuwatafuta na kuwatambua wanafunzi walioko nje ya skuli. (dakika 10 – 15).

Katika mjadala wa pamoja, mkufunzi awatake washiriki wabainishe mikakati wanayoweza kuitumia kwa ajili ya kuwatafuta na kuwatambua wanafunzi walioko nje ya skuli. Jawabu za washiriki ziwekewe kumbukumbu kwa kuziandika. Mkufunzi anapaswa kuwahamasisha washiriki kutaja mikakati mingi ya kuwatambua wanafunzi hao kadri inavyowezekana (dakika 10 – 15).

## Kitendo cha 3.4b: Kutumia utafiti tatuzi katika kuwatambua na kuwatafuta wanafunzi walioko nje ya skuli

Kikuu

Muda: Dakika 60

Kitendo hiki kina lengo la kuwasaidia washiriki kuendeleza utafiti tatuzi ndani ya skuli na jamii zao Kuwatafuta na kuwatambua wanafunzi walioko nje ya skuli. Utafiti huu umeelezewa katika Moduli ya 1 lakini inaweza kutia mashaka kwa washiriki kufuata hatua za utafiti huu ipasavyo kama walishindwa kuifahamu dhana hii vizuri hapo kabla. Kwa hivyo kitendo cha utafiti huu unaohitaji usimamizi kinaweza kutumika kabla ya kujaribu kwa mara nyengine kufanya utafiti halisi ndani ya skuli na jamii.

Kipindi hiki kinatoa muhtasari juu ya namna ya utekelezaji wa vitendo vya utafiti huu vinavyoweza kufanywa pahali popote iwe katika jamii, skuli, na

kwengineko. Lengo kuu la kipindi hiki ni kuwasaidia washiriki kuzifahamu mbinu za kufanya utafiti huu katika mazingira na hali mbalimbali. Mkufunzi awaeleze washiriki kwa uwazi kwamba, utafiti huu unalingana na hali halisi na hivyo, haipaswi kuiga vitendo vya utafiti huu katika mazingira mengine. Kwa hivyo, mkufunzi awabainishie washiriki kwamba, **kazi ya utafiti tatuzi lengwa ni kutuwezesha kuwafahamu kwa undani wanafunzi walioko nje ya skuli, mahali wanapopatikana na sababu zinazowafanya wasihudhurie skuli.**

Mkufunzi awaongoze washiriki wakae katika vikundi vidogovidogo. Kila kikundi kizingatie na kijitayarishe kufanyia kazi mbinu nne (4) tafauti za kufanya utafiti tatuzi; mbinu hizo ni uchunguzi, usaili, vikundi lengwa na uchoraji wa ramani. Katika kuhakikisha kila mbinu inaangaliwa angalau na kikundi kimoja, mkufunzi awaelekeze washiriki katika mbinu ambayo kila kikundi kinapaswa kianze kuifanyia kazi. Kwa kufanya hivyo, mbinu zote nne zitafanyiwa kazi. Kama muda utakuwa wa kutosha, mkufunzi akielekeze kila kikundi kichague mbinu nyengine na kiifanyie kazi.

Kabla ya kuanza kufanya kazi hii ya vikundi, washiriki wote wanapaswa kusikiliza kwa makini maelezo ya ufafanuzi wa namna ya kuitumia mbinu inayohusika ya utafiti huu. Mkufunzi atumie nukuu zifuatazo kuelezea ufafanuzi wa utekelezaji wa kila mbinu kwa washiriki, hata hivyo kabla ya ufafanuzi, mkufunzi awatake washiriki waeleze wanachokijua kwenye mbinu hizo. Mkufunzi awashajiishe washiriki kurejea kisa mafunzo katika **kielelezo nambari 3.6** kinachoeleza muktadha huu ili waweze kufahamu mazoezi haya vizuri.

## Uchunguzi

**Kielelezo nambari 3.7** **Mfano wa Fomu ya Uchunguzi**

Mkufunzi awapatie washiriki wote fomu ya uchunguzi, **kielelezo nambari 3.7** na awatake waiangalie kwa makini. Washiriki wafikirie mambo gani wanaweza kuyagundua katika skuli na jamii zao ikiwa wanataka kujua pahali wanapopatikana wanafunzi walioko nje ya skuli na sababu za kutohudhuria skuli. Kisha mkufunzi awaeleze washiriki kwamba utumiaji wa mbinu hii ya uchunguzi unapaswa kuzingatia mambo yafuatayo:

- washiriki wa kikundi wafanye maamuzi ya pamoja juu ya mahali watakapofanya uchunguzi wa wanafunzi walioko nje ya skuli na sababu za kutokuhudhuria skuli mfano: katika maeneo ya masoko muda wa skuli kuwachunguza wanafunzi walioko nje ya skuli wakiuza mbogamboga, au katika mazingira ya nyumbani ambako wazazi au walezi hawafikirii umuhimu wa mtoto wa kike kupatiwa elimu; au madarasani ambapo wanafunzi hao hawawezi kukufikia au baadhi ya walimu na wanafunzi wanaonyesha ubaguzi dhidi ya vikundi fulani vya watu na kadhalika.
- washiriki wa kikundi wachague hali moja ya kuichunguza. Mfano wanafunzi wapo sokoni wanauza mbogamboga wakati wa skuli kwa kuzingatia fomu ya uchunguzi, washiriki wajadiliane na wakubaliane mambo ya kuandika katika uandishi watumie safu wima mbili. Safu wima moja waandike kumbukumbu ya wanayoyaona na kuyasikia, na safu wima nyengine ni kwa kumbukumbu za hisia binafsi au ufahamu juu ya kile kinachochunguzwa. Utaratibu huu wa uandishi utatafautisha baina ya kile wanachokiona washiriki au kukisikia na kile wanachokifikiria kwa sababu watu wawili wanaweza kuona tokeo moja lakini kila mmoja akalitafsiri tafauti na mwenzake.
- washiriki waweke kumbukumbu ya kile walichokiona bila ya upendeleo kadiri inavyowezekana. Wazingatie kila linalotokea kama vile uhusiano baina ya watu, lugha ya ishara, kinachozungumzwa na pia ukimya uliotawala.
- mwisho, washiriki wapendekeze vitendo ambavyo vinaweza kutekelezwa ili kuondoa vikwazo vinavyozuia kuwajumuisha wanafunzi katika kupata elimu bora.
- kila mshiriki wa kikundi analazimika aijaze fomu ya uchunguzi kwa sababu kila mmoja ataihitaji katika vitendo vinavyofuata.

## Usaili– Kuuliza Maswali

**Kielelezo nambari 3.8** **Muongozo wa Usaili**

Muongozo wa usaili Kielelezo nambari 3.8 unapaswa utolewe kwa washiriki wote. Washiriki wanapaswa kufikiria aina ya watu wa kwenda kuwafanyia usaili katika skuli au jamii inayohusika ili waweze kufahamu maeneo wanayopatikana wanafunzi walioko nje ya skuli na sababu zinazowalazimisha wasihudhurie skuli mfano wanafunzi walioko nje ya skuli wenyewe, wanafunzi waliopo skuli, wazazi au walezi wa wanafunzi, wawakilishi wa jamii, watendaji wa afya, na

wengineo. Mkufunzi awaeleze washiriki kwamba katika kufanya usaili mambo yafuatayo yanahitaji kuzingatiwa:

- Washiriki wakubaliane aina ya watu wa kuwasaili.
- Kumbuka, usaili ni kitendo cha kuuliza maswali na kusikiliza. Kwa hivyo, aina ya maswali tunayoyauliza, namna tunavyouliza na namna tunavyosikiliza na tunavyoonesha mrejesho wa majibu yao ni mambo muhimu ya kuyazingatia katika mchakato huo. Kuna aina mbili za maswali.  Maswali yaliyojifunga ambayo yanahitaji majibu mafupi (mfano, ndio na hapana) na maswali ya wazi yanayohitaji majibu marefu (mfano, suali la kwa nini?).
- Mfano mwegine wa maswali yaliyojifunga ni 'somo gani ulikuwa unalipenda zaidi skuli?' Hili ni swali lililojifunga kwa sababu linahitaji jawabu fupi la neno moja au mawili na halihitaji maelezo ya ziada. Hata hivyo, swali hili lililojifunga linaweza likawa swali la wazi utakapolibadilisha na likawa; 'Somo gani ulikuwa unalipenda zaidi skuli na kwa nini ulilipenda zaidi?'
- Weka mpangilio wa usaili. Mbali na hatua ya matayarisho, zipo hatua tatu muhimu katika mchakato mzima wa usaili; utangulizi, kufanya usaili, kuufunga au kuuhitimisha usaili. Pangilia aina ya maswali watakayoulizwa, na jinsi ya washiriki watakavyozitekeleza hatua zote tatu za usaili.
- Kila mshiriki wa kikundi anapaswa kuchukua nukuu za usaili kwa sababu kila mmoja atazihitaji katika vitendo vinavyofuata.

Ili kuhakikisha kila mmoja amefahamu, mkufunzi awatake washiriki wote watoe mifano ya maswali yaliyojifunga na maswali ya wazi ambayo wanaweza kuyauliza kwenye usaili unaohusu Elimu Mjumuisho. Kwa hivyo mkufunzi atapata kufahamu kwa kiasi gani washiriki wameelewa kuuliza maswali ya wazi na yaliyojifunga.

Hatua za mchakato wa usaili unaweza kuandikwa kwenye chati (baina ya kila hatua iachwe nafasi ya:

- Matayarisho
- Utangulizi
- Kufanya usaili
- Kufunga usaili/mwisho wa usaili

Washiriki wote wanaweza kutoa mapendekezo ya namna ya kujaza taarifa katika 'hatua za mchakato wa usaili'. Mfano, mkufunzi ajifanye anamsaili mshiriki, lakini anaonekana mchovu na hana hamu. Kisha mkufunzi awatake

washiriki waelezee kitu gani msaili amekifanya sivyo na kitu gani sahihi alipaswa akifanye.

## Kikundi cha Mijadala

Mkufunzi awaeleze washiriki kuwa vikundi vya mijadala ni vikundi vinavyojadiliana. Washiriki kwanza wakubaliane kuwepo kwa msimamizi (mwenyekiti) wa kikundi lengwa atakayeongoza mjadala. Pia washiriki wajadiliane aina ya watu wa kuunda kikundi legwa ambao wataweza kutoa taarifa za wanafunzi walioko nje ya skuli na sababu za kutohudhuria skuli. Mkufunzi awatake washiriki kuzingatia mambo muhimu yafuatayo wakati wa majadiliano na kikundi lengwa:

- Kukubaliana kuhusu wanaokwenda kufanya mjadala.
- Kumbuka, mjadala wa kikundi lengwa unaweza kushirikisha kikundi kimoja mahsusi katika vikundi vya wadau wa elimu. Mfano; wazazi au walezi wa wanafunzi, au ukashirikisha wadau mbalimbali wa elimu.
- Mjadala unaweza ukafanywa kwa kila kikundi peke yake. Mfano; mjadala na wanafunzi ambapo wazazi, walimu au walezi wao hawapo. Pia mjadala unaweza ukashirikisha vikundi mbalimbali vya wadau wa elimu kuunda kikundi kimoja kitakachojadili jambo mahasusi. mfano wazazi, walimu na wanafunzi wanaweza kujadili kwa pamoja sababu za wanafunzi kutohudhuria skuli.
- Kupanga mijadala ya kikundi lengwa na mambo wanayohitaji kujadiliwa.
- Kutaarisha njia zilezile zilizofanywa katika mbinu ya usaili lakini ukiwa na maswali ya muongozo yatakayoanzisha na kuendeleza mjadala. Kufikiria mbinu wanazoweza kuzitumia kuanzisha mjadala wa kikundi lengwa; hata kama washiriki wa kikundi lengwa wana haya au wanashindwa kuelezea maoni yao.
- Kila mshiriki wa kikundi anapaswa aandike nukuu za mjadala kwa sababu kila mmoja atazihitaji katika kitendo kinachofuata.



*Kikundi lengwa pamoja na watoto*

**[Maelezo ya picha: Wazee 4, wanawake 3 na mwanamme 1, wanaendesha mjadala wa kikundi lengwa wakiwa na wanafunzi; wote wamekaa kitako darasani juu ya madawati yaliyopangwa duara. Wazee wawili wamemuelekezea mgongo mpiga picha na mzee mwengine sehemu ya mwili wake imejificha. Wazee wawili wanaonekana wanaandika nukuu za mjadala. Ijapokuwa haipo wazi, kutoka katika picha ni nani anayezungumza, kila mshiriki anaonekana kusikiliza kwa makini.]**

## Mbinu ya Ramani

Mkufunzi awaeleze washiriki kwamba ramani ni ile njia ya kuzingatia (na kuyajadili kwa pamoja) mazingira ya skuli au jamii ya washiriki. Wanaweza kutumia ramani kuonyesha vikwazo (na utatuzi) katika skuli au jamii mahasusi. Washiriki wa vikundi vinavyotayarisha ramani ya mazingira ya wanafunzi wanapaswa kuzingatia yafuatayo:

- Kuamua pahali gani na kwa ajili ya kitu gani wanakwenda kutumia mbinu hii ya ramani. Kwa hivyo mbinu hii ya ramani itumike kuonesha mazingira halisi ya wanafunzi walioko nje ya skuli pamoja na viashiria vya sababu za kutokuhudhuria skuli. Ubora wa mbinu hii ni kutoa msaada mkubwa katika kujenga ufahamu wa watu juu ya matatizo yanayowakabili wanafunzi walioko nje ya skuli.
- Kupanga maeneo muhimu ya kuyaingiza katika ramani. Ni vikwazo gani wanataka kuvionesha, na vipi wanaweza kuonesha utatuzi wa vikwazo hivyo katika hali inayotekelezeka.

- Kuchora ramani ya eneo linalohusika/ la kielelezo. Kuonesha ramani hiyo itakuwaje. Kutumia chati, kalamu na penseli za rangi kwa kuchora ramani hiyo.
- Ramani zilizochorwa zioneshwe ili washiriki wa vikundi waweze kufanya rejea kwa mahitaji ya kitendo kinachofuata.

Kwa ujumla, mkufunzi awatake washiriki wanapofanya utafiti tatuzi wazingatie mambo yafuatayo:

- Washiriki wanaweza kuchagua kutumia mbinu fulani ya utafiti tatuzi pamoja na watu na/au maeneo yanayohitaji mazingatio maalumu katika kuonesha uhalisia wa maisha, kama vile kuchunguza mahusiano katika familiya. Hali ikiwa hivyo washiriki wahakikishe wanafuata hatua zote za kitaalamu na za kiusalama wakati wa upangaji na utekelezaji.
- Kumbuka mchunguzi mara zote anatakiwa asijidhihirishe. Kwa mfano, kama anachunguza darasani asiwaulize wanafunzi au walimu maswali au kuingilia kati muendelezo wa somo.
- Kitendo cha kutumia mbinu ya ramani kiwashirikishe wadau wote wa elimu katika jamii inayohusika. Kwa namna hii, washiriki wataweza kugundua vikwazo vilivyopo na mapendekezo yaliyotolewa na wadau wote ya kutatua vikwazo hivyo. Hii ni kwa sababu kila mdau anao uzoefu na kumbukumbu ya maisha halisi ya jamii inayohusika.



*Washiriki wakitayarisha ramani*

**[Maelezo ya picha: Wanawake wawili wamekaa kwenye viti. Juu ya meza ipo karatasi kubwa yenye ramani ambayo haijamalizika kuchorwa; ramani inaonesha barabara/njia na maumbo mengine ambayo huwezi kuyapambanua kwa urahisi.]**




*Mfano wa ramani*

**[Maelezo ya picha: Ramani ina maumbo mengi ya mraba na mstatili yenye ukumbwa na rangi tafauti yenye kuonesha mpangilio wa eneo la soko.]**




*Mfano wa ramani iliyochorwa Macedonia*

**[Maelezo ya picha: ramani inaonesha mitaa katika mpangilio huo wa mitaa yapo maumbo mbalimbali ya mraba yenye kuonesha nyumba, maduka na skuli. Kuna alama zenye kuonesha vikwazo vya ujumuishi.]**

## Kitendo cha 3.4c: Mrejesho juu ya Mazoezi ya Utafiti Tatuzi

Kikuu

Muda: Dakika 30

Moja kati ya faida za utafiti tatuzi ni kwamba watu tafauti hushirikishwa katika utafiti, kutumia mbinu bora na zinazoendana na wadau wanaotaka kupata taarifa kutoka kwao. Wakati wa kipindi cha utekelezaji, washiriki wanaweza kukosa muda wa kujaribu zaidi ya mbinu moja kwa kila mmoja. Kwa hivyo, kipindi cha mrejesho wa kina kinaweza kuwasaidia kufahamishana kile walichokisoma wakati wa kutumia mbinu tafauti.

Nyuma ndani ya chumba cha mafunzo, mkufunzi atengeneze vikundi vipya. Kila kikundi awepo angalau mshiriki mmoja aliyefanya uchunguzi, mmoja aliyefanya mbinu ya ramani na kadhalika. Kila kikundi kipya kinalazimika kufanya uwasilishaji (uwasilishaji wa kuona na mazungumzo) utakaoweka pamoja taarifa zote zilizokusanywa kwa kuzingatia mbinu mbalimbali.

Baada ya muda ulioainishwa, mkufunzi ashajihishe kutumiwa kwa mbinu bora za kuwasilisha mrejesho ambazo zimependekezwa katika vipindi vilivyopita (sherehe, mkutano na waandishi wa Habari na wengineo.)



*Washiriki wakitayarisha uwasilishaji wa mrejesho wa utafiti tatuzi.*

**[Maelezo ya picha: Watu 4 wameizunguka meza, wawili wamekaa, wawili wamesimama; wawili waliosimama wanaonekana baadhi ya sehemu. Juu ya meza zipo karatasi mbili kubwa. Mwanamke anaandika kwenye karatasi hizo.]**

Mkufunzi vilevile anaweza kuwataka washiriki, wafikirie mbinu walizozitumia wakati wa kipindi cha utendaji wa utafiti tatuzi faida na hasara, mambo gani yalifanyika vyema, mambo gani hayakufanikiwa na mambo gani yafanyike kuimarisha matumizi ya mbinu kwa vipindi vitakavyokuja baadae.



*Mshiriki akiwasilisha ramani*

**[Maelezo ya picha: mtu amesimama mbele ya karatasi kadhaa za chati zinazoning'inia kwenye ukuta. Karatasi hizo zinaonesha ramani, kielelezo na maneno. Kuna mtu anaonesha katika karatasi kubwa lao kwa kutumia fimbo.]**

Mwisho mkufunzi awaeleze washiriki kwamba mwishoni mwa mafunzo watapangiwa kazi nyengine za utafiti tatuzi. Watatakiwa wachague na wazikamilishe kabla ya moduli inayofuata.

## Kipindi cha 3.5: Kufahamu Elimu ya kipindi cha Mpito na Athari zake

Kipindi hiki kinakusudia kuwawezesha washiriki kuzingatia mambo ambayo uongozi wa skuli unatakiwa kufanya ili kuwarejesha skuli wanafunzi walioko nje ya skuli pamoja na kuwasaidia wanafunzi wengine waliopo katika mpito wa elimu. Vilevile, kipindi hiki kitawasaidia washiriki kufahamu maana ya elimu ya mpito na namna inavyoweza kuathiri kushiriki na kufaulu kwa wanafunzi katika kujifunza.

Mkufunzi anapaswa kuwa na maana zifuatazo za mpito wa elimu ambazo anatakiwa kuzionesha mwanzo wa kipindi:

**Mpito wa elimu** ni kile kipindi ambacho wanafunzi wanaanza au wanamaliza skuli, ni wakati ambao wanafunzi wanakwenda skuli kwa mara ya kwanza, au wanapohama kutoka ngazi, darasa au skuli moja kwenda nyengine.

> "Mpito ni mchakato unaotokea kwa muda fulani (kwa mfano) kutoka wakati watoto wanaanza kujitayarisha kuanza skuli hadi wakati ambao wameshayazoea mazingira ya skuli ikiliganishwa na siku au wiki ya mwanzo walipoanza skuli."[3]

Kipindi cha mpito wa elimu kinaweza kuwa ni kipindi kigumu kwa wanafunzi, familia zao na walimu wao. Wanafunzi wengi wanatoroka skuli wakati wanapokuwa au wanapomaliza kipindi cha mpito wa elimu, hususan ikiwa wana mahitaji maalumu ambayo hayajazingatiwa wakati wa kipindi cha mpito wa elimu.

---

[3] Hirst, M., Jervis, N., Visagie, K., Sojo, V. and Cavanagh, S. (2011) Transition to primary school: a review of the literature, Commonwealth of Australia, Canberra. https://minerva-access.unimelb.edu.au/bitstream/handle/11343/123771/Transition-to-Primary-School-A-literaturereview.pdf?sequence=1&isAllowed=y

## Kitendo cha 3.5a: Uzoefu wetu Wenyewe wa Mpito wa Elimu

Kikuu

Muda: Dakika 30

+

Mkufunzi awatake washiriki kutafakari uzoefu wao wenyewe wa mpito wa elimu. Kila mshiriki azungumze na mwenzake au jirani yake na ajaribu kukumbuka **nini kilitokea** na **vipi walijisikia** wakati walipoanza skuli mpya au walipohama darasa au skuli katikati ya mwaka.

Baada ya dakika 10-15, mkufunzi awatake washiriki kujitolea kutoa mrejesho kwa darasa zima juu ya uzoefu mzuri au mbaya ambao umetolewa na majirani zao. Mkufunzi anaweza akaruhusu mjadala juu ya mambo yoyote yatakayojitokeza yanayohusiana na kumbukumbu za uzoefu wa mpito wa elimu.

Kisha mkufunzi awatake washiriki kuendelea kufanyakazi katika jozi zao na kujadili yafuatayo:

- Ni aina gani ya mpito wa elimu ambao wanafunzi wao wanapitia, kwa mfano, kutoka nyumbani kwenda katika maeneo au skuli za maandalizi au skuli za msingi, kutoka skuli za msingi kwenda skuli za sekondari, kutoka skuli za sekondari kwenda elimu ya juu, kutoka skuli maalumu za wanafunzi wenye mahitaji ya ziada kwenda katika skuli za kawaida au kinyume chake, kutoka katika kikundi kimoja cha kujifunza ndani ya darasa au mwaka mmoja kwenda mwengine, pamoja na kuwasili skuli katikati ya mwaka.
- Ikiwa kuna baadhi ya wanafunzi wanaingia au wanahama skuli nje ya wakati uliopangwa, kwa nini wanafanya hivyo?
- Jee! wanafunzi wao waliopo katika mpito wa elimu wanapewa msaada stahiki? Kivipi?

Mwisho, mkufunzi awatake washiriki kutoa mrejesho wa mawazo yao kwa darasa zima huku akiwa anaandika dondoo muhimu katika chati au ubaoni.

# Kitendo cha 3.5b: Kufahamu Athari za Mpito wa Elimu

Kikuu

Muda: Dakika 30

Lengo la kipindi hiki ni kuwawezesha washiriki kuzingatia namna ya mpito wa elimu unavyoathiri ujifunzaji au kujifunza.

Kwanza, mkufunzi anatakiwa kueleza kwamba, wanafunzi wanapitia uzoefu na athari tafauti za mpito wa elimu. Utafiti[4] umebaini athari mbalimbali zikiwemo zifuatazo:

- Uzoefu wa mwanzo anaoupata mwanafunzi skuli unaweza ukawa na mchango mzuri katika maendeleo ya mwanafunzi katika kujifunza.
- Kwa wanafunzi wengi mabadiliko ya mazingira na hisia ya kwamba wanaendelea mbele huwa ni kichocheo cha maendeleo, lakini ikiwa watahisi mabadiliko haya ni ya ghafla, kuna hatari ya wanafunzi kurudi nyuma kimasomo, kuwa na wasiwasi na kutotulia skuli.

**Kielelezo nambari 3.9** — **Matokeo ya utafiti – sampuli A**

**Kielelezo nambari 3.10** — **Matokeo ya utafiti – sampuli B**

**Kielelezo nambari 3.11** — **Matokeo ya utafiti – sampuli C**

**Kielelezo nambari 3.12** — **Matokeo ya utafiti – sampuli D**

Mkufunzi atoe moja kati ya **Kielelezo nambari 3.9 - 3.12** kwa kila kikundi pamoja na nakala za ziada ili kuhakikisha kwamba kila mshiriki anapata nakala ya kusoma. Mkufunzi ahakikishe kwamba kila kikundi kinapata kielelezo tafauti isipokuwa kama kuna zaidi ya vikundi vinne ambapo wakati mwengine vikundi

[4] Tazama rejea zilizopo mwisho wa moduli hii.

zaidi ya kimoja vinafanyia kazi kielelezo kimoja. Mkufunzi aeleze kwamba vielelezo hivi ni baadhi ya madondoo kutoka katika baadhi ya tafiti zilizofanywa katika miaka mbalimbali na kuchaguliwa kutoka vyanzo au rejea mbalimbali.

Sampuli hizi hazikusudii kuwakilisha tafiti zote muhimu zilizofanywa katika eneo hili, lakini zimewekwa kwa ajili ya kuchochea mjadala na mabadilishano mazuri ya uzoefu kwa washiriki.

Mkufunzi aeleze kwamba ijapokuwa sampuli hizi zinahusiana zaidi na matokeo ya tafiti juu ya athari za mpito wa elimu kutoka skuli za msingi kwenda za sekondari, bado matokeo haya yanaendana na ngazi nyengine za skuli. Kuna tafiti chache sana juu ya mipito ya elimu ya ndani kwa ndani kama vile kutoka mwaka mmoja kwenda mwaka mwengine, kutoka darasa moja kwenda jengine au wakati wanafunzi wanapojiunga katika kikundi chengine cha kufanya kazi au cha masomo.

Mkufunzi awatake washiriki katika kila kikundi:

- Kusoma kwa pamoja na kuifahamu sampuli ya habari waliyopewa.
- Kubadilishana mawazo kwa pamoja juu ya namna gani matokeo ya tafiti yanavyohusiana na wanafunzi katika skuli zao.
- Kuzungushia duara au kuonesha kwa peni au penseli ya rangi kitu chochote kipya kwao au kilichowashangaza.

Ikiwa muda utaruhusu, mkufunzi anaweza kuwapa kielelezo tafauti kikundi kilichomaliza kazi mapema.

Mkufunzi atake kila kikundi kubadilishana walichojifunza na kujadiliana kwa pamoja darasa zima pamoja na kuandika dondoo za msingi zitakazojitokeza. Vilevile, mkufunzi anatakiwa ahakikishe kwamba washiriki wanelewa kuwa:

> ‘Uzoefu wa wanafunzi wetu wa mpito wa elimu unatafautiana. Wanafuzi wengi wana uzoefu mzuri ijapokuwa baadhi ya wanafunzi wanaathiriwa na wasiwasi na matatizo ya muda mrefu’.

Mwisho, mkufunzi avitake vikundi vyote kila kimoja kuunda sentensi inayohusiana na mpito wakianzia na: ‘**Mpito ni …..’**

Kila kikundi kiunde maelezo ambayo yatasisitiza athari wanazopitia wanafunzi, lakini ikumbukwe kwamba athari hizi ni sehemu ya maisha na zinaweza kusaidia kujenga na kuimarisha uthabiti, kujiamini, kubadilika au kuendana na mazingira pamoja na kujithamini kwa mwanafunzi. Maelezo yaliyotolewa na vikundi yanaweza kusomwa na kuandikwa katika chati na kubandikwa ukutani.

# Kipindi cha 3.6: Kuzifikia changamoto

Kipindi hiki kinawashajihisha washiriki kuzingatia mikakati sahihi ya kuwasaidia wanafunzi wanaopambana na aina tafauti za changamoto katika mapitio yao ya elimu.

## Kitendo cha 3.6a: Kufika skuli

Kikuu

Muda: Dakika 90

Madhumuni ya kipindi hiki ni kuwashajiisha washiriki kuwaonea huruma wanafunzi, hasa wanafunzi wapya wanofika skuli, wanaokabiliana na vikwazo katika siku za mwanzo za kuanza skuli[5].

Mkufunzi anapaswa aanze kwa kuelezea kwamba mwendo wa kutoka nyumbani kwenda skuli ya maandalizi au skuli ya msingi, kutoka skuli ya maandalizi kwenda skuli ya msingi, au kutoka skuli ya msingi kwenda skuli ya sekondari unaweza ukajumuisha mabadiliko yafuatayo ambayo mwanafunzi anapaswa akabiliane nayo:

- Ikiwa anaanza skuli ya maandalizi anayaacha mazingira ya nyumbani kwa mara ya kwanza.
- Kwenda kwenye mazingira tafauti ambayo kimsingi ni makubwa.
- Idadi kubwa ya wanafunzi ambao ni wakubwa tafauti na skuli aliyotoka (skuli yake ya awali).
- Kuunda marafiki wapya na kuanzisha mahusiano mapya.
- kujifunza kwa lugha tafauti au lugha za ziada.
- Kukabiliana na mitazamo tafauti ya kufundisha na ya mtaala.
- Matarajio tafauti ya wazazi/wasimamizi, walimu na uongozi wa skuli.
- Mazingira mapya yasiyowafikisha katika matarajio na mielekeo yao.
- Mabadiliko ya vyoo, wakati wakula, nyenzo, mpangilio wa madarasa, njia, na mazingira ya nje ya skuli.

[5] Mazoezi haya yanapatikana katika vifaa saidizi vya EENET vilivyo ndani ya programu ya video: https:www.eenet.org.uk/the-10-videos-and-manuals/

Mkufunzi anapaswa awaeleze washiriki kwamba wataangalia filamu kwa dakika 5 ambayo inaonesha uzoefu wanafunzi wanaoupata skuli kila siku. Filamu haikusudiwi kuonesha hali halisi au hali ya mambo ya mazingira ya skuli washiriki wanayoifanyia kazi, lakini itaonesha maeneo muhimu tu yanayohusu mapito ya kujifunza ambayo yanafanana kwa skuli zote.

Kufika skuli ni jambo muhimu. Linaweza kuonesha kwamba wanafunzi wapya wameanza vizuri katika skuli yao mpya, aidha wanafunzi ambao tayari wameshahudhuria skuli, wanaianza vizuri siku yao. Itaonekana kama wamejihisi kupokewa vizuri au hawakupokewa vizuri, ambapo inaweza kuathiri ushiriki wao wa siku nzima. Inaweza pia kuwafanya waendelee kwenda skuli.

- Baadhi ya wanafunzi wanaweza kuona kufika skuli ni shida kubwa, inachanganya au ni jambo baya sana.
- Kuna vitu vingi vyepesi au rahisi, visivyo na gharama au vyenye gharama nafuu tunaweza kuvifanya ili kuifanya skuli ni mahali pazuri na kuwasiadia wanafunzi kwenda skuli kwa urahisi.
- Tunaweza kubadilisha mitazamo, mazingira, utendaji wetu na tabia, na vifaa tunavovitumia. Tunaweza hata kufanya mabadiliko ya sera, kuhakikisha kwamba skuli zetu zipo salama na zinawajumuisha wanafunzi wote.
- Mkufunzi awatake washiriki, kuangalia filamu, **Kielelezo nambari 3.13**, mpango wa 3 wa video ya 'Kufika skuli' wa EENET kufikiria inakuaje kwa wanafunzi wapya walioandikishwa skuli, wanapofika skuli, siku yao ya kwanza?

**Kielelezo nambari 3.13** **Filamu ya 'Kufika skuli' ya EENET, mpango wa na maelezo yake**

Ikiwa mkufunzi ameshindwa kuipata filamu kupitia mtandao na kuionesha kwa washiriki anapaswa kukipatia kila kikundi mkarara (maandishi ya filamu inayohusika). Baada ya kuangalia filamu, mkufunzi awashajiishe washiriki kutoa mrejesho mfupi wa mambo muhimu yaliyojitokeza katika filamu hiyo.

Mkufunzi awagawe washiriki katika vikundi wakiwa na idadi sawa akiwa na dhamira ya kupata idadi ya watu 5 katika kila kikundi. Kisha awape washiriki maelekezo yafuatayo:

- tengeneza igizo dhima ambalo litachukua kiasi cha dakika 4. Nusu ya kikundi kitatengeneza igizo dhima linaloonesha mapokezi mabaya ya ufikaji

skuli. Vikundi vyengine vitatengeneza igizo dhima la mapokezi mazuri ya ufikaji skuli.

- kabla hujaanza kupangilia utengenezaji wa igizo dhima, tumia njia ya chemshabongo kujua mawazo ya wanakikundi. Igizo dhima liwe linahusu uzoefu wa mwanafunzi wa kufika na kupokelewa skuli kwa mara ya kwanza katikati ya mwaka.
- wale watakaotengeneza igizo dhima linalooonesha mapokezi mabaya ya kufika skuli wafikirie yale mambo yasiyo sahihi yanayoweza kutokea. Haya yanaweza kuwa ni mambo uliyoyapitia ulipokuwa mwanafunzi au mambo ambayo yametokea ulipokuwa unafundisha au dhima zilizojitokeza katika filamu na kukupa hisia.
- wale ambao watatengeneza igizo dhima linalooonesha hali sahihi ya ufikaji skuli, wafikirie mambo yote yaliyofanywa na kuwafanya wanafunzi wajihisi wamepokelewa vizuri, wajiamini na wako salama walipofika skuli. Fikiria utatuzi (suluhisho) unaoweza kufanywa kwa kuzingatia rasilimali au vifaa vilivyopo katika skuli yako.
- Hakikisha kila mshiriki anapata nafasi ya kushiriki katika igizo dhima. Unaweza kuwa mwalimu, mwanafunzi, mzazi au mlezi au mtu mwengine. Wahusika wako wanapaswa kuwa wanaume na wanawake. Unaweza kuamua wasifu mahasusi kwa mwanafunzi mpya, kwa mfano anaweza kuwa hawezi kuzungumza lugha inayotumika skuli, au anaweza kuwa na mahitaji ya ziada. Fikiria wahusika wako watazungumza nini na watafanya nini.

Mkufunzi awapatie washiriki angalau dakika 20 za kutafakari na baadae wataarishe maigizo yao. Baada ya hapo avialike vikundi vioneshe maigizo yao; vikundi vyenye igizo dhima hasi vialikwe mwanzo kuonesha maigizo yao na vikundi vyenye igizo dhima chanya vifuatie kuonesha maigizo yao.




*Igizo dhima katika warsha ya Zanzibar*

**[Maelezo ya picha: Washiriki watatu wa kike wamesimama katika chumba cha mafunzo wanajadiłliana. Washiriki waliobakia wamekaa na kusikiliza mjadala.]**

Baada ya kila kikundi kuonesha igizo lake, mkufunzi anapaswa kuwaalika washiriki wote kufanya mjadala wa pamoja wakiongozwa na maswali haya:

- Mambo yepi hasi yanatokea katika skuli yako? Nani unadhani wanaathiriwa na mambo haya? Na vipi wanaathiriwa?
- Ni mambo yepi chanya yanatokea katika skuli yako? Ni nani wanasaidia matokeo hayo?

Mwisho, mkufunzi awatake washiriki waorodheshe vitu viwili wanavyoweza kuvibadilisha au kuvianzisha ili kuhakikisha skuli zao zinafikika (ni rafiki) na zinajumuisha wote. Hakikisha haya ni mawazo wanayoweza kuyatekeleza kwa kuwepo kwa nyenzo (vifaa) zilizotajwa.

## Maelezo kwa wakufunzi

Kwa kumbukumbu za wakufunzi, hizi ni jawabu zinazotarajiwa kutoka kwa washiriki

Maigizo dhima kwa mafikio hasi katika skuli yanaweza kuhusisha majawabu yafuatayo:

- Kumuona mwalimu mkali na aliyechukiwa mara tu unapofika mlangoni au getini.

- Unajihisi kuzidiwa na kukwama katikati ya kundi kubwa la wanafunzi.
- Kujiona ni mwenye kukandamizwa na kudhulumiwa.
- Kujiona mpweke au hajui namna ya kutengeneza marafiki au kuzungumza na wanafunzi wengine
- Kujaribu kutafuta pahali penye ukimya kusubiri.
- Kutokuelewa wanafunzi wengine na walimu wanachokizungumza Kushindwa kusoma alama zilizopo skuli.
- Kujihisi wamechanganyikiwa.
- Kushindwa kwenda darasani.

Maigizo dhima kwa mafikio chanya katika skuli yataibua yale washiriki waliyoyaona katika filamu na yanaweza yakahusisha:

- Kuamkiwa na mwalimu mwenye furaha na tabasamu.
- Kukutana na marafiki.
- Kushirikiana na rafiki yako anayekusaidia kuzunguuka au kutafuta pahali pa kwenda.
- Kuziona ishara au alama zinazokukaribisha na kukuelekeza ufanye nini au wapi pa kwenda.
- Kwenda sehemu yenye ukimya iliyotengwa kusubiri masomo yaanze.
- Kuwepo kwa utaratibu uliopangwa wa kuingia darasani. Mfano, kila mmoja anapanga mstari na anasubiri mwalimu aseme ingieni, au wanafunzi wanajua wanaingia wawiliwawilli, na mengineyo.

## Kitendo cha 3.6b: Visa mafunzo–utafanya nini?

Kikuu

Muda: Dakika 45

Mkufunzi awakumbushe washiriki kuitambua skuli ya mjumuisho yenye mazingira rafiki ambayo watawapatia wanafunzi wapya haya yafuatayo:

- Mazingira rafiki, salama na yasiyo na msongo wa mawazo.
- Fursa ya kuwa na marafiki na kufanya kazi kwa pamoja.
- Pahali ambapo watathamini na watajivunia.
- Kutambulika ujuzi na vipaji vyao.
- Kupata nafasi ya haraka kushiriki katika jamii.
- Mazingira ya kawaida ya kujifunza.
- Kupatikana kwa fursa za kujifunza.
- Msaada kwa mahitaji ya ziada.

Skuli yenye mazingira rafiki kama hayo ni muhimu sana kwa maendeleo ya kila mwanafunzi na hususan hao wenye mazingira magumu. Wanafunzi wapya wanaoingia skuli katikati ya mwaka wanaweza kuwa wanatoroka katika hali ngumu. Mfano, familia zao zitakuwa zimo katika hali ya kuhama, watakuwa katika athari ya skuli ambayo italingana na skuli aliyotoka. Labda ana mahitaji ya ziada yaliyopelekea kuchelewa kutoa maamuzi, amefukuzwa kutoka skuli nyengine, familia yake ilikosa uwezo wa kiuchumi na kushindwa kumuandikisha skuli kwa wakati muafaka. Rudia moduli ya ziada inayosema **Kuwashirikisha Wanafunzi wenye Mahitaji ya Ziada** Ikiwa inahitajika iwe ni ukumbusho wa baadhi ya changamoto zinazowakabili wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

Mkufunzi anapaswa kuelezea kwamba kisa mafunzo kinachofuatia ni kuhusu mwanafunzi mwenye mazingira magumu. Baadhi yao ni wale ambao wamefika skuli au wamefika skuli katikati ya mwaka. Awatake washiriki waangalie vizuri na kukaa pamoja huku wakitafakari njia sahihi ya kumsaidia kila mmoja.

| | |
|---|---|
| **Kielelezo nambari 3.14** | **Kisa mafunzo – Khadija, ana umri wa miaka7** |
| **Kielelezo nambari 3.15** | **Kisa mafunzo – Afifa, ana umri wa miaka7** |
| **Kielelezo nambari 3.16** | **Kisa mafunzo – Rashid, ana umri wa miaka 10** |
| **Kielelezo nambari 3.17** | **Kisa mafunzo – Suleiman, ana umri wa miaka 11** |
| **Kielelezo nambari 3.18** | **Kisa mafunzo – Juma, ana umri wa miaka 14** |
| **Kielelezo nambari 3.19** | **Kisa mafunzo – Shamila, ana umri wa miaka 15** |

Ikiwa kutakuwa na idadi ya kutosha, mkufunzi awatake washiriki wakae kwenye vikundi vya watu 4-5 wakiwa na wenzao wanaofundisha ngazi sawa katika skuli zao (mfano; wa skuli za maandalizi, skuli za msingi, skuli za sekondari). Mkufunzi awapatie washiriki **Kielelezo nambari 3.14 – 3.19 katika kila kundi (kila mshiriki apatiwe nakala moja)**. Kielelezo nambari3.14 na 3.15 ni msingi awali (chini). **Kielelezo nambari 3.16.3** na **3.17** ni msingi juu na **Kielelezo nambari 3.18 – 3.19** ni sekondari.

Hata hivyo, hakuna tatizo iwapo washiriki katika baadhi ya makundi wataangalia kisa mafunzo kutoka skuli/ngazi tafauti na zile wanazofanya kazi wao. Kwa hakika, kutakua na manufaa kwa kundi zima kwa kupata mitazamo tafauti kutokana na kujiingiza kivitendo katika majadiliano ya kisa mafunzo hicho.

Kila kikundi kinapaswa kusoma kisa mafunzo pamoja na kujadili maswali waliyopewa katika kila kisa mafunzo. Ikiwa muda unatosha na kikundi kikahisi kimejadiliana kiasi cha kutosha kisa mafunzo hicho, mkufunzi awape kisa mafunzo chengine (inawezekana kimetoka katika skuli/ngazi hiyo hiyo, skuli/ngazi tafauti).

## Maswali ya mjadala

- Una maoni gani?
- Wanafunzi wana mahitaji gani na mikakati gani unaweza kutumia kusaidia mahitaji hayo?
- Vipi wewe pamoja na watoa huduma wengine au wataalamu mnawasaidia wanafunzi kufanikiwa katika mpito wa elimu?

Katika majadiliano yao, mkufunzi anapaswa kuwashajihisha washiriki kuzingatia mazingira rafiki, kuwapa taarifa au maelekezo ya awali na matendo ya upimaji katika darasa. Ikiwemo kutumia usaidizi rika na ikiwa ipo ndani ya majukumu yao, uwepo wa uongozi na usimamiaji wa uingiaji skuli. Ni muhimu kusisitiza kwamba skuli ya mjumuisho haitarajii wanafunzi wawe tayari kusoma wanapofika. Ijapokuwa ikiwezekana kutoa taarifa na msaada kumsaidia kila mmoja kujitayarisha ni jambo jema; kwa hivyo ni jambo muhimu sana kuziweka skuli tayari kwa ajili ya kuwapokea wanafunzi na kuimarisha uwezo wa kusaidia vizuri mpito wa elimu kwa wanafunzi.

Baada ya dakika 15–20 mkufunzi awatake washiriki watoe mrejesho na ashajihishe mijadala, na waandike nukta muhimu kwenye ubao/chati mgeuzo kwa kila kisa mafunzo.

**Maelezo kwa mkufunzi kwa ajili ya kusaidia mjadala wakati wa mrejesho wa kisa mafunzo**

Kumbuka kusisitiza walichojifunza kupitia filamu waliyoiangalia katika kitendo kilichopita na sifa muhimu za msaada wa mpito wa mjumuisho (angalia dondoo zilizowekewa alama hapo juu, zinakielezea kitendo).

Kama ulivyo utaratibu, tunapofanya mrejesho wa mjadala wa kisa mafunzo, kumbuka marekebisho mengi yanahitajika. Usihukumu maoni ya washiriki kuwa ni sahihi au si sahihi.

Majadiliano ni muhimu kwa kuwasaidia washiriki kuainisha vikwazo na kwa pamoja kufikia suluhisho, mara zote inahitaji kazi shirikishi kwa familia za wanafunzi katika mazungumzo.

Vilevile ni muhimu kuipongeza skuli kwa kila walichompa mwanafunzi bila kujali ugumu wa mahitaji yake. Usalama mzuri wa matokeo ya maisha yao ambayo wanayapata katika skuli. Ambapo mwanafunzi atapewa mrejesho wa mpangilio wa siku na jamii pengine baada ya kuzitambua baadhi ya changamoto. Pia kushiriki kusoma itapelekea fikra ya usalama, dhamira na matumaini kwa mwanafunzi.

Kuzizingatia fikra chanya za kila kikundi. Kusisitiza umuhimu wa pamoja katika kusaidia maingiliano ya jamii, katika jukumu lenye mawanda mapana kwa mada zinazohusika zinazojumuisha kipato cha nyumbani, michezo, sanaa, msaada wa kielimu wa kusoma na kuandika na mengineyo katika kuangalia ubora wa mwanafunzi badala ya upungufu wake.
Nukta nyengine za ziada ambazo unaweza kizitumia katika kisa mafunzo ni:

**Khadija**

*Mambo ya kuzingatia ni Pamoja na:*
kuonekana dhaifu na mdogo kwa mujibu wa umri wake; je ni kutokana na kutengana na kupotea kwa familia? Kutokua na marafiki; je ni kutokana na kutowajali na kuchoka?

*Mahitaji au mikakati au msaada ni pamoja na:*
Zungumza na mama yake ili kupata uzoefu alionao; iwapo je, Khadija anapata mlo kamili na huduma za kiafya? Je, Khadija anakosa usingizi anapokuwa nyumbani? Anajiwekaje anapokuwa nyumbani? Mawasiliano pia kwake ni tatizo? Lugha ipi Khadija anaifahamu?

Pale itakapowezekana, hakikisha Khadija anapatiwa michezo kwa ajili ya kumtathmini na kuonesha ushiriki wake katika jamii, hasa michezo yamaji au mchanga, kutumiwe mikakati ya ziada itakayomuwezesha kujifunza lugha darasani ikiwa zitahitajika; afanyiwe uchunguzi wa kiafya; Utambulisho wa msaada wa jamii katika msikiti ambao utakuwa ni muhimu sana kuisaidia familia kupata utulivu na kutafuta ushirikiano na msaada wa kihisia na kwa ruhusa yake, amuunganishe mama yake na wanafamilia wengine katika jamii. Ikiwemo jumuiya ya msaada wa jamii ikiwa ni yenye kutoa msaada wa kumsaidia.

**Afifa**

*Mambo ya kuzingatia ni pamoja na:*
Afifa yuko nje ya skuli. Mtazamo wa mwalimu/skuli unaonekana kuwa hasi (sio mzuri). Afifa ana matatizo katika kuzungumza, kuwasiliana na ya kijamii.

*Mahitaji, mikakati au msaada ni pamoja na:*
Mpeleke Afifa skuli; yatambue mahitaji yake mengine ya ziada; mjengee uwezo katika maswala mengine ya kijamii; mpatie fursa nyingi zaidi za kumuwezesha kusikiliza na kuzungumza na mengineyo.

**Rashid**

*Mambo ya kuzingatia ni pamoja na:*
Athari ya kupoteza wazazi akiwa katika umri mdogo; pengine amezowea kutosimamiwa katika tabia (maadili). Ni zipi athari za kihisia zinazotokana na kutengana na bibi yake hivi karibuni? Amelazimika kurejea kwa mama yake na kuanzisha uhusiano mpya na baba yake wa kambo; hajali na hana utulivu. Pengine tabia yake inatokana na matatizo ya kutojua kusoma na kuandika au tatizo la kujifunza.

*Mahitaji, mikakati au msaada ni pamoja na:*
Zungumza na familia na kutambua uzoefu walionao. Zingatia matakwa ya baba wa kambo juu ya kazi anazozifanya Rashid na kujenga ushirikiano; Jadili au pendekeza njia za kumkutanisha Rashidi na bibi yake. Hakikisha Rashidi anaweza kushiriki michezo. Mpatie mikakati ya kumsaidia kusoma darasani; wakati wa mapumziko au mlo wa mcahna mpatie miongozo juu ya namna ya kujishughulisha na michezo au kuwasilisha mahitaji yake kwa walimu. Hali hiyo inaweza kumpunguzia matatizo aliyonayo.

**Suleiman**

*Mambo ya kuzingatia ni Pamoja na:*
Suleiman ana wasiwasi na hana uhakika na maisha yake ya baadae pamoja na familia yake; hali hii inaathiri utendaji wake.

*Mahitaji au mikakati au msaada unaohitajika:*
Zungumza na familia, ili kupata taarifa zaidi iwapo wanahisi kwamba skuli inaweza kuwapatia msaada; ikiwa pamoja na kumuunganisha na huduma zozote saidizi au watetezi wa kijamii. Mpatie Suleiman huduma za ushauri

kupitia mtu anaemuamini au aliyemzidi umri; mjuulishe mwalimu wa Suleiman ili afahamu hali aliyonayo Suleimani. Kusanya taarifa za maendeleo ya kazi za Suleimani anazopaswa kuzifanya, je hataweza kurudia tena skuli kwa muda mfupi ujao. Apatiwe muongozo na kazi za nyumbani ambazo zitamsaidia kujifunza mwenyewe ikiwa itahitajika. Pia atengenezewe mfumo wa elimu masafa ikiwa unapatikana. Kuwe na mawasiliano ikiwa ataondoka na mengineyo.

**Juma**

*Mambo ya kuzingatia ni pamoja na:*
Wasiwasi wa Juma ni kuhusu afya ya mama yake; pamoja na mahitaji, hofu ya skuli na athari za tishio la unyanyasaji kutoka kwa wavulana wengine; mtazamo wa mama yake juu ya mahudhurio.

*Mahitaji au mikakati au msaada unaohitajika:*
Inahitajika kuondoshwa kwa matishio kutoka kwa wavulana wakubwa; inahitajika kuanzishwa kwa michakato ya makubaliano wakati Juma anapokua na wasiwasi; zungumza na mama yake Juma ili aweze kujikubalisha kumfanya Juma arudie tena skuli; pia zungumza na Juma; anzisha tena michakato, andaa mipango ambayo itamuwezesha Juma kuungana na wenzake anapokwenda na kurudi skuli; andaa mipango myengine itakayomfanya Juma ajihisi yupo salama; andaa fursa kwa ajili ya Juma za kumjengea uwezo wa kujiamini katika jamii na kujenga urafiki na mengineyo.

**Shamila**

*Mambo ya kuzingatia ni Pamoja na:*
Masuala ya ulemavu na kutozingatiwa uwezo mkubwa alionao; mtazamo hasi wa mwalimu wa usajili na upya wa skuli.

*Mahitaji au mikakati au msaada unaohitajika:*
Pinga/kataza mtazamo wa mwalimu wa usajili. Toa taarifa juu ya maendeleo ya awali ya Shamila na wapatie taaluma hiyo wafanyakazi. Wahakikishie hilo walimu wapya wa Shamila kwamba Shamila anahitaji kusoma na anafurahia kufundishwa na kushiriki katika mikakati rahisi inayomsaidia yeye kushiriki na kufanikiwa. Kuwashirikisha wataalamu na watoa huduma za msaada, inapowezekana. Anzisha mafunzo na mifumo ambayo itakuwa ni njia ya kuimarisha ubora wa tathmini za awali za skuli na michakato ya kuwaingiza

katika mifumo hiyo. Andaa ratiba ya awali kulingana na vifaa vinavyopatikana. Jiunge na watetezi wao ili kufanya rahisi upatikanaji wa kiti cha magurudumu kwa ajili ya kukitumia awapo skuli.

**Kielelezo nambari 3.20**

**Kanuni za msingi kwa ajili ya mpito salama**

Mkufunzi anapaswa kuwapa washiriki **Kielelezo nambari 3.20**. Hizi ni kanuni za msingi ambazo zilizoelezwa na mradi pamoja na taarifa ya Daraja la Matumaini iliyopewa kichwa cha habari "Mikakati ya kuimarisha mazingira jumuishi kwa Watoto". Muongozo kuhusu mpito kwa ajili ya kusaidia mpito salama. Kutoka maandalizi hadi skuli za msingi (2017). Muongozo wa Daraja la Matumaini unaweza kuhakikisha kuwa kwa kile anachokijua kila mwanafunzi kinamsaidia kumuendeleza katika mazingira mapya. Inaweza pia kusaidia katika kuhakikisha kwamba, mabadiliko hayo aliyoyapata yanathibitisha kuwa yupo salama na anapata msaada wa kumjengea uzowefu kuliko kumharibia.

## Kitendo cha 3.6c: Mikakati ya Mpito jumuishi

**Kikuu**

Muda: Dakika 30

**Kielelezo nambari 3.21**

**Kadi za changamoto**

**Kielelezo nambari 3.22**

Kadi za mkakati

Mkufunzi atoe kadi kutoka katika **Kielelezo nambari 3.21** na **Kielelezo nambari 3.22** kwa kila kikundi. Kadi kutoka **Kielelezo nambari 3.21** na **Kielelezo nambari 3.22** ziwe za rangi tafauti.

Mkufunzi awatake washiriki waoanishe mikakati na changamoto zinazolingana. Vilevile mkufunzi abainishe kwamba; hatuwezi kutumia kadi moja ya mkakati kwa kulinganisha na kadi moja ya changamoto; kadi mbalimbali za mikakati zinaweza kutatua/kulingana na kadi nyengine tafauti za changamoto. Hivyo, vikundi vinatakiwa kuziweka katika makundi yanayolingana kadi za mikakati na zile za changamoto. Ikiwa mkufunzi anataka kujikita katika changamoto

maalumu, changamoto hizo zinapaswa kuchaguliwa pamoja na mikakati inayowiyana; changamoto nyengine zinaweza kuachwa na kutojadiliwa. Mbinu hii sio sahihi kwa kufundishia mikakati ya kuwasaidia wanafunzi walioko katika mpito wa elimu kwa ujumla, lakini ikiwa inakusudiwa kutoa mafunzo juu ya mpito maalumu wa elimu, uchaguzi wa changamoto maalumu ni sahihi kabisa.

Katika kadi ambazo hazina maandishi, washiriki wanaweza kuandika changamoto na mikakati ya ziada ikiwa zipo zilizobainishwa wakati wa mjadala.

Baada ya dakika 15-20, mkufunzi awatake washiriki katika vikundi kutoa mrejesho kwa darasa zima juu ya maamuzi waliyofikia juu ya mikakati inayofaa na kujadili yafuatayo:  Je mikakati hiyo ni sahihi?

Katika ngazi ya mwanafunzi/skuli au familia au jamii, ni jukumu au kazi ya nani kutoa mikakati hiyo?




*Uoanishaji wa mikakati na changamoto katika warsha iliyafanyika Zanzibar*

**[Maelezo ya picha: Washiriki wanawake na wanaume wakiwa katika vikundi. Katika kila kikundi kuna kadi za mikakati na changamoto ambazo washiriki wanazitazama na kuzijadili. Vilevile mkufunzi amesimama pembezoni mwa moja kati ya meza za washiriki akisikiliza mjadala.]**

Kwa ajili ya rejea kwa mkufunzi, jadweli lifuatalo linapendekeza uwiano wa changamoto na mikakati:

| Changamoto | Mikakati |
|---|---|
| Nashindwa kutembea ndani ya mazingira ya skuli au sizijui njia za kuyaendea maeneo ya skuli yangu mpya. | Wafanyie wanafunzi wapya matembezi ya maeneo au mazingira ya skuli, wapatie ramani na andaa msaada rika. Mfano, Rafiki wa darasa moja ili kumsaidia mwanafunzi kuyajua maeneo ya skuli. |

| Changamoto | Mikakati |
|---|---|
| Nimechanganyikiwa na ratiba mpya ya skuli. Sijui muda gani ninapaswa niende wapi? Nimekuwa nagombwa kwa kuchelewa kila wakati. | Hakikisha wanafunzi wapya wanapatiwa msaada-rika kwa wiki kadhaa na kwamba wanafunzi wanatakiwa kusaidiana na kuzawadiwa kutokana na kufanya hivyo. |
| Tangu niingie madarasa ya juu, ushiriki wa wazazi wangu skuli umekuwa ni mdogo sana japokuwa nahitaji wazungumze na walimu wangu ninapokuwa na matatizo. | Wakaribishe skuli wazazi na walezi wote kwa upole na andaa kikao cha kukaribisha wanafunzi wapya na wazee wao ili kujadili na kubadilishana mawazo mbalimbali kabla ya wanafunzi wapya hawajaanza kusoma. Baada ya wiki chache, waalike tena wazazi au walezi wa wanafunzi wapya ili kubadilishana mawazo juu ya maendoleo ya awali ya wanafunzi na kuelezea matarajio ya skuli. |
| Nikiwa mtoto wa kike, sasa hivi mimi ndiye mtoto mkubwa, hivyo ninapaswa kufanya kazi nyingi za nyumbani. Jambo hili linanisababishia kuchelewa sana skuli na kuingia matatizoni. | Wawezeshe walimu kutembelea nyumbani kwa baadhi ya wanafunzi ili kujua changamoto na mahitaji yao na namna wanavyopata msaada kutoka katika jamii na familia zao. |
| Wazazi wangu hawafahamu kwamba napaswa kufanya mazoezi ya nyumbani ninaporudi skuli. Wao wanatarajia kila siku nikisharudi skuli nimhudumikie ndugu yangu na kufanya kazi nyengine za nyumbani. | Kutana na wazazi au walezi mapema wakati wa kuandaa mipango binafsi ya maendeleo ya elimu na mpito wa elimu. Wagaie wazazi au walezi vipeperushi vinavyoelezea nini cha kutarajia na ni shughuli gani wao na skuli wanapaswa |

| | |
|---|---|
| | kuzifanya ili kuwasaidia wanafunzi walioko katika mpito wa elimu. |
| Skuli yangu mpya ipo katika upande tafauti wa mji na inanibidi kwenda skuli mwenyewe ijapokuwa sio salama. | Wasaidie wanafunzi wapya waweze kushughulikia masomo yao na kwa pamoja wabadilishane mawazo juu ya uzoefu wao wa mpito wa elimu. Baadhi ya skuli zimekuwa zikifanya mijadala mizuri juu ya namna wanafunzi wanavyohisi na changamoto wanazokabiliana nazo wanapohamia skuli mpya. |

| Changamoto | Mikakati |
|---|---|
| Sijazoea kuwa mbali na wazazi wangu kwa muda wa siku nzima. | Wakaribishe wazazi au walezi kuingia madarasani (hasa katika skuli za maandalizi) ili kuwasaidia watoto wao kuzoea mazingira ya skuli. Washirikishe wazazi au walezi katika kuandaa mipango na shughuli zitakazowasaidia wanafunzi wanapokuwa katika mpito wa elimu. |
| Walimu katika skuli hii wanatumia njia/namna tafauti za kufundishia. Siwezi kuendana na matarajio yao. | Kuwa na wafanyakazi wanaosimamia mpito wa elimu kutoka ngazi moja ya elimu kwenda nyengine au skuli moja kwenda nyengine. |
| | Ungana na wadau wengine ili kuwasaidia wanafunzi kabla, baada na wakati wanapokuwa katika mpito wa elimu. |
| Masomo katika skuli hii hayavutii. Ninasoma vitu vile vile ambavyo nimeshavisoma katika skuli niliyotoka. | Rekebisha mtaala na mbinu za kufundishia ili kuendana na uzoefu wa awali wa wanafunzi katika skuli walizotoka. |
| | Hakikisha mipango binafsi ya elimu ya wanafunzi inaandikwa na kupewa walimu au skuli zao mpya. |
| | Andaa utaratibu wa kufanya tathmini ya awali kwa wanafunzi na panga matarajio ya kielimu na kijamii pamoja na kupitia |

| | |
|---|---|
| | maendeleo ya wanafunzi wapya baada ya wiki chache. |
| Walimu katika skuli yangu ya zamani walipanga mpango maalumu wa kunisidia kimasomo lakini walimu wangu wapya hawalijui hili. Mipango yote ya kunisaidia inapaswa kufanywa tena. Natamani walimu wangu wa zamani wangeweza kushirikishwa katika jambo hili. | Andaa utaratibu wa kubadilishana walimu baina ya skuli. Kwa mfano, mwalimu wa skuli mpya ambaye anahusika na mwaka wa mpito wa elimu pamoja na Mratibu wa Elimu Mjumuisho wanaweza kutembelea madarasa ya wanafunzi ambao wanatarajia kuhama skuli waliopo kwenda skuli nyengine ili kuweza kuwajua na kujibu maswali yao. |
| Nataka kujiunga na Chuo cha Mafunzo ya Amali. Sijui vyuo ambavyo ni mjumuisho kwa wanafunzi wenye mahitaji ya ziada. Katika skuli yangu vile vile hakuna | Hakikisha wanafunzi wa skuli za sekondari wana taarifa za kutosha juu ya kuwepo kwa vyuo vya amali ambavyo vinajumuisha wanafunzi wenye mahitaji ya ziada ya kujifunza. |

| **Changamoto** | **Mikakati** |
|---|---|
| anaevijua vyuo hivyo. | Hakikisha skuli za sekondari, vyuo vikuu na vyuo vya mafunzo ya amali vinatoa mafunzo sahihi ya ushauri kuwahamasisha wanafunzi wenye mahitaji ya ziada katika kujifunza. |
| Naingia matatizoni kwa kuonekana jeuri kwa mwalimu wangu mpya kwa sababu sifahamu anataka nifanye kitu gani. | Hakikisha walimu wana uelewa wa kutosha juu ya usomaji wa kila mwanafunzi; katika kuwasaidia kufanya tathmini ya awali wanafunzi wapya.<br><br>Msaidie mwanafunzi ikiwa hajafahamu, vilevile tarajia wanafunzi wapya kuwa wazungumzaji au wafanyaji zogo sana ikiwa wanayaogopa au wanafurahishwa na mazingira yao mapya. |
| Sikuwahi kuyaona mazingira ya ndani ya skuli yangu mpya hadi siku ya kwanza katika muhula mpya. Niliogopa sana. | Wasaidie wanafunzi kutembelea madarasa au skuli zao za baadae ili wapate kuyazoea mazingira, watu na harakati kabla ya kuhama. |

| | |
|---|---|
| | Andaa siku za matayarisho ya wanafunzi kutembelea skuli zao mpya kabla ya kuhama. Katika siku hizi, wanafunzi wapya wataweza kukutana na walimu wao wapya watakaowasomesha mwaka unaofuata pamoja na kupata uzoefu wa baadhi ya masomo. Vilevile, watapata nafasi ya kuonana na wanafunzi wenzao wa baadae kutoka skuli nyengine pamoja na kupata nafasi ya kuwauliza maswali wanafunzi waliohama mwaka uliopita katika skuli zao. |
| Nina hofu sitopata rafiki wapya au nitashindwa kushiriki kikamilifu katika matukio ya skuli. | Wape mafunzo walimu na wafanyakazi wote juu ya namna ya kusaidia mahitaji ya wanafunzi kihisia, kimwili na kitaaluma wakati wanapohama au kujiunga na skuli na wapatie ushauri unaofaa. |
| | Andaa matukio ambayo yatawasaidia wanafunzi kujenga urafiki katika wiki za mwanzo za masomo. |

| Changamoto | Mikakati |
|---|---|
| | Wafanyakazi wasaidizi wanatakiwa kuhakikisha kuwa hawasababishi wanafunzi kujihisi wametengwa au wanatafautiana na wanafunzi wengine darasani. |
| | Wapongeze wanafunzi wapya kila wanapojitahidi kufanya vizuri kitu chochote na kuyazoea mazingira mapya vizuri. |
| | Hakikisha wanafunzi wapya wanapewa majukumu ya skuli mapema na wanashirikishwa katika kazi mbalimbali pamoja na wanafunzi wengine wakubwa au wakongwe zikiwemo shughuli za nje ya mtaala kama vile michezo, klabu na shughuli za uzalishaji mali. |

| | |
|---|---|
| | Toa msaada wa mpito wa elimu kwa muda wa mwaka mzima kwa wanafunzi wanaohitaji. |
| Sijihisi kuwa na mimi ni sehemu ya skuli hii. | Hakikisha wanafunzi wapya wote wanashirikishwa katika shughuli za ubunifu na za burudani ambazo zimo katika mtaala na nje ya muda ya skuli kwa ajili ya kuwawezesha kwa haraka kushirikiana na jamii mpya, kuwa na hamu na hisia za maendeleo. |
| | Wasikilize wanafunzi wapya na waongozaji rika wao. Andaa mkutano wa mapitio baada ya wiki chache kwa sababu wao ndio wenye taarifa muhimu kuhusiana na mpito wa elimu baina ya skuli na kwa hivyo wapo katika nafasi ya kutoa mapendekezo mazuri kuhusiana na msaada ambao wao na wenzao wanauhitaji. |
| Ninachokozwa, ninanyanyaswa na nimekua naogopa hususani katika muda wa mapumziko na wa chakula cha mchana. | Andaa sera madhubuti ya kupambana na unyanyasaji na hakikisha wanafunzi wakubwa wote wanaohudumia wakati wa muda wa mapumziko na wa chakula cha mchana wanaambiwa kuwa kuna wanafunzi wapya skuli. |

| Changamoto | Mikakati |
|---|---|
| | Toa nafasi ya michezo au shughuli zilizoandaliwa wakati wa mapumziko au chakula cha mchana. |
| | Hakikisha kila mtu anajua sehemu ya kwenda hususan wakati wa mapumziko ikiwa watahisi hawako salama. |
| Siku ya mwanzo kuja skuli nilichekwa kwa sababu sina viatu. | Hakikisha vifaa vya ziada vya mavazi au sare za skuli zinapatikana kwa ajili ya wanafunzi wanaotoka katika familia maskini. |

**Kielelezo nambari 3.23** **Mpango wa Ushauri wa Kipindi cha Mpito wa elimu - kutoka nyumbani au skuli ya maandalizi kwenda skuli ya msingi**

Mkufunzi ampe kila mshiriki nakala ya **Kielelezo nambari 3.23** na kuwataka wakisome kisha waseme ikiwa ushauri huu unafaa. Vilevile, awaulize washiriki ikiwa ushauri huo unafaa kusaidia mpito wa elimu baina ya skuli ya msingi na skuli ya sekondari.

## Kitendo cha 3.6d: Kuendeleza Usaidizi-rika - Urafiki

**Kikuu**

Muda: Dakika 45

Mkufunzi aeleze kwamba sasa hivi wataangalia majukumu ya "marafiki". Wakumbushe washiriki kwamba "marafiki" waliokusudiwa hapa ni wale waliowaona katika filamu waliyoiyangalia katika **Kitendo cha 3.6a**. 'Rafiki' ni msamiati unaotumika kuelezea usaidizi-rika, usaidizi ambao mara nyingi hupewa wanafunzi wapya katika skuli.

Mkufunzi aeleze kuwa wanafunzi wote ambao ni wapya skuli wanaweza kufaidika kwa msaada wa wanafunzi wenzao. Katika mwanzo wa mwaka wa masomo, wanafunzi wakubwa wanaweza kupewa kazi ya kuyatembelea madarasa ya wanafunzi wapya ili kuwasaidia kama vile kwa kuwapa taarifa, kujibu maswali na kuwatembeza katika maeneo ya skuli.

Kwa wanafunzi wanaohamia skuli katikati ya mwaka, au kwa wanafunzi wapya ambao wana mahitaji ya ziada, wanaweza kupangiwa msaidizi-rika binafsi kwa ajili ya msaada na ushauri. Rafiki anaweza kusaidia katika njia nyingi, zikiwemo:

- Kuwaonesha wanafunzi wapya mazingira ya skuli
- Kuwasaidia kujua ratiba ya skuli
- Kuwatambulisha wanafunzi wapya kwa wafanyakazi wote wa skuli
- Kuwatambulisha wanafunzi wapya kwa wanafunzi wengine ambao wanazungumza lugha mama
- Kuwasaidia kwa kuwaelezea utaratibu wa kazi
- Kuwasaidia kujifunza lugha kuu inayotumiwa katika masomo (lugha ya kufundishia). Mfano Kiswahili, Kiarabu au Kiingereza.

- Kujumuika na wanafunzi wapya wakati wa michezo au mapumziko
- Kuwa rafiki anayewezekana au anayefikika
- Kusaidia tathmini ya namna wanafunzi wapya wanavyozoea mazingira ya skuli.

Jambo la muhimu kwa rafiki au msaidizi ni kuwa mtu ambaye anayewajibika na mwenye uwezo mzuri wa kuwasiliana na kuamiliana na watu. Vilevile, washiriki wanatakiwa kukumbuka kwamba, wanafunzi wengine ambao si marafiki au wasaidizi, wanaweza pia kuwasaidia wanafunzi wapya katika njia nyingi. Marafiki au wasaidizi pia wanaweza kuwa vizuri ikiwa watapewa mafunzo na msaada endelevu. Utoaji wa zawadi na kibali au utambulisho utalipa hadhi jukumu la rafiki.

**Kielelezo nambari 3.24** — **Andalio la Somo la Mafunzo ya Urafiki au Usaidizi**


**Kielelezo nambari 3.25** — **Muongozo wa Wasaidizi**

Mkufunzi awatake washiriki kufanya kazi katika jozi na awapatie **Kielelezo nambari 3.24** na **Kielelezo nambari 3.25** kwa kila jozi. Vielelezo hivi vinatoa mfano wa andalio la somo kwa ajili ya kuwasaidia washiriki katika kutoa mafunzo ya usaidizi au urafiki na maelezo ya ushauri kwa wasaidizi wa wanafunzi wapya.

Mkufunzi awatake kila jozi kusoma na kujadili vielelezo vyote kwa umakini, kisha wajiunge katika vikundi ili kujadili mafunzo hayo ikiwa yanaweza kutumika katika skuli zao, na kama ni hivyo, ni mabadiliko gani yanaweza kufanyika ili mafunzo hayo yaweze kutumika kiufanisi. Mkufunzi awatake kila kikundi kutoa mrejesho wa mjadala huu kwa ufupi.

Mwisho, mkufunzi awape washiriki katika kila kikundi karatasi ya chati mgeuzo na kalamu za rangi na awatake wakamilishe **Kitendo cha 4** kutoka katika **Kielelezo nambari 3.24** chenye mafunzo yanayohusu urafiki au usaidizi. Vilevile, mkufunzi awatake washiriki wabuni na kuchora bango lao wenyewe kwa ajili ya kuwapa mafunzo wasaidizi au marafiki, mabango yaeleze taarifa kuu kutoka katika **Kielelezo nambari 3.24 Kitendo cha 1-3** cha andalio la somo.

Mabango hayo kisha yabandikwe ukutani kwa ajili ya washiriki kuangalia wakati wa mapumziko.




*Bango la kuwakaribisha skuli wanafunzi wapya*

**[Maelezo ya picha: Bango lililochorwa kwa mkono ambalo lina kichwa cha habari kinachosomeka, 'Mafunzo ya wasaidizi au marafiki'; mchoro wa mwanafunzi mpya akisaidiwa na mwanafunzi mwenzake (rafiki) ambaye pia anakaribishwa na mwalimu kwa kusema "karibuni wanafunzi wapya". Eneo la ofisi ya walimu na maktaba ya skuli pia limeoneshwa kwenye mchoro.]**



*Kuandaa ramani ya skuli kwa ajili ya wanafunzi wapya*

**[Maelezo ya picha: Washiriki watatu ambao ni wanawake wawili na mwanamme mmoja wapo katika meza ambapo kuna ramani ya skuli ambayo wanaitengeneza. Washiriki wa kike wamekaa na wa kiume amesimama ambaye anatarajia kubandika kikaratasi chenye mchoro katika ramani. Mwanamke mmoja anachora mchoro kwa ajili ya kubandika katika ramani wakati mshiriki mwengine wa kike anajadili pamoja na mshiriki wa kiume aliyesimama akionesha sehemu fulani ya ramani, labda anapendekeza sehemu ya kubandika kikaratasi.]**

## Kitendo cha 3.6e: Kusaidia Kujifunza Lugha ya ziada

Kikuu

Muda: Dakika 30

Baadhi ya wanafunzi wapya ambao kwa mfano wale wote wanaojiunga na skuli nje ya muda wa kawaida, wanaweza wakachanganyikiwa na masomo waliyosoma skuli walizotoka pamoja na yale ya skuli mpya na matokeo yake wanaweza wasiifahamu lugha ya kufundishia inayotumika katika masomo na pia lugha wanayoitumia wanafunzi wenzao. Baadhi ya wanafunzi lugha ya kufundishia inaweza kuwa mpya kwao wakati kwa wanafunzi wenzao sio mpya.

**Kielelezo nambari 3.26**

**Kubali au Kataa**

Washiriki wafanye kazi katika vikundi ambapo mkufunzi atawapa Kielelezo nambari 3.26 kila kikundi na kuwataka waamue sentensi zipi kati ya sentenzi 8 zinazofafanua kuhusu ujifunzaji wa lugha ya ziada wanakubaliana nazo na zipi hawakubaliani nazo.

Baada ya dakika 5 – 10 mkufunzi awatake washiriki kufanya mrejesho kwa kuwataka kuinua mikono ikiwa wanakubaliana au hawakubaliani na kila sentensi.

- Taarifa kwa ajili ya mkufunzi, sentensi nne zifuatazo ni sahihi:
- Wakati wanafunzi wanajifunza lugha ngeni, ni kitu cha kawaida kwa wao kunyamaza kimya kwa muda.
- Wanafunzi hujifunza lugha ya kigeni kwa urahisi zaidi ikiwa hawaogopi kufanya makosa.
- Ni muhimu sana kupata nafasi ya kuzungumza na kufanya kazi na watu wengine wakati mtu anajifunza lugha mpya au ya kigeni.”
- Wanafunzi hujifunza lugha ngeni kwa urahisi zaidi wanapohitaji kuwasiliana na watu wengine wanaozungumza lugha hiyo.

Aidha, sentensi nne zifuatazo **si sahihi**:

- Wanafunzi hujifunza lugha mbalimbali kwa urahisi zaidi ikiwa watajikita na mazoezi ya sarufi ya lugha.
- Ni muhimu sana kusahihisha makosa ya wanafunzi wakati wanajifunza lugha.

- Mara tu wanafunzi wanapoweza kuwasiliana kwa kupitia lugha ya kufundishia, huwa hawahitaji tena msaada wa lugha."
- Wanafunzi hawapaswi kutumia lugha yao ya kwanza darasani kwa sababu huwa inaathiri katika kujifunza lugha ya kufundishia.

Kwa maelezo zaidi, mkufunzi awadokezee washiriki baadhi ya misingi mikuu itakayowaongoza walimu katika kusaidia ujifunzaji wa lugha ya ziada:

- Lazima kuwa na mazingira salama ya kujifunza ambapo wanafunzi huthaminiwa, huwa hawana khofu na huwa na matarajio makubwa katika kujifunza lugha hiyo.
- Wanafunzi hujifunza vizuri zaidi lugha ya ziada kwa kushirikiana na wengine wanaotumia lugha hiyo.
- Lugha ya kwanza ya mwanafunzi ina mchango mkubwa katika kujifunza lugha ya ziada: Hii ni kwa sababu maarifa, dhana na ujuzi wa kitaaluma uliofikiwa katika lugha moja unaweza kuhamishiwa katika lugha nyengine.
- Uzoefu wote wa kujifunza uliopangwa kwa wanafunzi kwa lugha ya ziada unatakiwa kuwa changamoto ya utambuzi kwa wanafunzi wenzao ambao wanaumahiri zaidi katika lugha hiyo.

**Kielelezo nambari 3.27** **Usaidizi wa Lugha ya Kufundishia kwa Wanafunzi Wapya - Vidokezo kwa Walimu**

Mwisho, mkufunzi awape **Kielelezo nambari 3.27** kila mshiriki kwa ajili ya kusoma. Baada ya muda, mkufunzi ashajihishe mjadala kuhakikisha washiriki wanafahamu wazi kielelezo kinavyosema au kinavyoeleza.

# Kipindi cha 3.7: Kuanzisha mpito wa elimu mjumuisho ndani ya skuli yetu

Kipindi hiki kitatoa fursa kwa washiriki kupitia vitendo na mipango yote ya skuli pamoja na kufanya utafiti tatuzi ili kutambua yaliyo mazuri ili kuyaamini na kuyategemea na yale yenye upungufu yanahitaji kutafutiwa ufumbuzi.

## Kitendo cha 3.7a: Hivi sasa tuko wapi na tunataka kuelekea wapi?

Kikuu

Muda: Dakika 80

**Kielelezo nambari 3.28** — **Kadi za vitendo na utowaji wa huduma wa skuli**

**Kielelezo nambari 3.29** — **Bango la maendeleo**

Mkufunzi atawagawa washiriki katika makundi ikiwezekana waweze kuwakilisha nafasi za kitaaluma na ulezi. Wanajamii pia wanaweza kushiriki katika warsha ya mafunzo ya wakufunzi. Washiriki wakae katika vikundi vya skuli zao za majaribio na kukamilisha vitendo, huku wakitafakari namna ya utekelezaji wa mafunzo katika skuli zao za majaribio.

Mkufunzi ataitambulisha dhana hii ya mpito wa elimu mjumuisho na kueleza kwamba wakati wa kufanya vitendo vyengine, washiriki wazingatie dhana hii kuwa ni muongozo kwa kile wanachotaka kukifanya.

> ‘Mpito wa elimu mjumuisho humsaidia kila mwanafunzi kuyazoea mazingira ya skuli mpya na kuwa mwanafunzi mwenye maendeleo ya haraka katika muda mfupi. Hali hii huzifanya wiki muhimu za mwanzo kuwa za furaha. Mabadiliko ya elimu jumuishi yanayoleta mashirikiano mema ya awali kati ya skuli na nyumbani, huhusisha wazazi, walezi na walimu”

Mkufunzi wape kila kikundi **Kielelezo nambari 3.28** chenye kadi za jozi ya vitendo vya kujifunza na **Kielelezo nambari 3.29** chenye mchoro wenye kuonesha maendeleo endelevu katika chati mgeuzo.

Mkufunzi awape washiriki maelekezo yafuatayo:

- Kila kikundi kiamue sehemu ya kuweka kadi ya maendeleo endelevu katika kichwa cha Habari “Mambo tunayoyafanya vyema” au “Mambo yanayohitaji kuimarishwa”

  Maamuzi yako yazingatie namna unavyoijua skuli na ushahidi ambao unaweza kutolewa ili kuunga mkono maamuzi hayo. Kwa mfano, ikiwa umeamua kuiweka kadi katika maelezo, “Walimu wanafahamu vyema watoto wanaoishi katika mazingira magumu na wanafahamu mahitaji yao maalumu tokea mwanzo” karibu na kichwa cha Habari, “Mambo tunayoyafanya vyema”, itakuhitaji kuamini kwamba skuli inazo taarifa zilizokusanywa juu ya jambo hili na vilevile upo mfumo wa kupashana taarifa (fomu za ruhusa ya kujiunga na skuli kupatiwa walimu zikiwa na taarifa hizo).

- Kadi zote zitakapokuwa zimewekwa chini, angalia zile kadi ambazo umeziweka katika au karibu na kichwa cha habari “Mambo yanayohitaji kuimarishwa”. Jadili namna ambavyo wewe au skuli mtakavyoshughulikia na bainisha aina ya vitendea kazi vitakavyohitajika katika utendaji huu. Mfano njia bora za kujifunza ambazo zinaimarisha umoja wa kijamii, njia au mbinu tafauti za tathmini, sifa na ujuzi unaohitaji ili kupata mafunzo, mipango ya muda mfupi, mipango ya maendeleo ya mwanafunzi binafsi, msaada wa kundi rika na kadhalika). Kumbuka washirika wema wa skuli (marafiki) wanaweza kutumiwa ili kuunga mkono mabadiliko ya elimu (mfano jamii na makundi yenye harakati za Imani ambayo yanaweza kuzipokea familia mpya katika maeneo yanayohusika, huduma za kijamii au wahudumu wa afya ambao wanaweza kuwafikia wazazi au walezi.

- Mwisho, chunguza upungufu uliopo katika jozi zako za vitendea kazi na uandike vifaa vitatu ambavyo vinaweza kutoa mchango mkubwa kwa wanafunzi katika dhana nzima ya mabadiliko. Pia eleza namna vitendea kazi hivyo vitakavyokuwa ni chachu ya mabadiliko.

Wakati wa matembezi ukumbini, mkufunzi awatake washiriki katika kila kundi kuwasilisha baadhi ya mambo waliyobainisha ambayo yanakwenda vyema na yale ambayo yanahitaji kuimarishwa. Vilevile, kila kikundi kitoe maelezo ya vifaa vilivyopo na vifaa vyengine ambavyo wangependelea kuwa navyo pamoja na sababu ambazo vipaumbele vya maendeleo ya skuli viyazingatie.

Mkufunzi asisitize umuhimu wa msaada wa pamoja na ushirikiano ambapo skuli zinashirikiana na mashirika mengine yanayotoa huduma ili kuhakikisha wanafunzi na wazazi wanakuwa skuli katika kipindi cha mpito wa elimu.




*Kundi la washiriki wa warsha likijadili pahali pakuweka kadi zao katika bango la maendeleo endelevu*

**[Maelezo ya picha: Washiriki saba wa kike wamekaa kulizunguka bango la maendeleo endelevu katika chati. Washiriki wanne wanaonekana nusu. Michoro mitatu imechorwa katika karatasi. Baadhi ya kadi zimebandikwa katika mstari wa tatu. Washiriki wanajadiliana, na mmoja anaangalia kundi jengine.]**

**Kielelezo nambari 3.29** — **Dondoo na Maswali ya Kuitathmini Skuli**

**Kielelezo nambari 3.29** — **Orodha ya Mambo yanayosaidia Mpito wa Elimu – orodha hakiki kwa ajili ya walimu**

Mwisho, mkufunzi awape washiriki **Kielelezo nambari 3.30** na **Kielelezo nambari 3.31** na awaelezee kwamba Kielelezo nambarikwanza ni orodha ya maswali ya tathmini yenye lengo la kutoamazoezi yenye kusaidia tathmini nzima ya elimu ya mpito katika skuli zao. Kielelezo nambaripili kinatoa muongozo kwa walimu wa madarasa wanapowapokea na kuwasaidia wanafunzi wapya wanapoingia skuli.

## Kitendo cha 3.7b: Matumizi ya Utafiti Tatuzi katika Kuimarisha Mpito wa Elimu ya mjumuisho kwa Wanafunzi Walioko Nje ya Skuli

Kikuu

Muda: Dakika 60

Kwa kukumbuka tafiti tatuzi zilizofanywa kabla, ni muhimu kusisitiza tena kwa vipi kila skuli ina changamoto na faida za kipekee za kielimu ambazo zinahitaji majibu ya kipekee. Kwa ajili hiyo walimu hawawezi kutegemea wataalamu kutoka sehemu nyengine kuwaelezea namna ya kuzifanya skuli zao kuwa jumuishi.

Walimu, wanafunzi, wazazi au walezi pamoja na wajumbe wengine katika jamii ya skuli wanapaswa kuwa wataalamu katika mazingira yao. Wanapaswa kuchunguza mambo yaliyopo katika skuli zao na jamii kwa ujumla, kuvitambua na kujumuisha ufumbuzi wa matatizo ambayo yanahitaji kukuzwa. Kisha, kwa msaada wa watu wengine hatua zinazohusika za mambo hayo zitaanza. Utafiti tatuzi ni nyenzo muhimu ya kufanikisha jambo hili. Utafiti tatuzi husaidia wenza kutizama mazingira yao, kuchambua matatizo yaliyopo, kutoa mapendekezo na kuyafanyia kazi.

Mkufunzi akumbushie **Kitendo cha 3.4b** na **Kitendo cha 3.4c** ambapo washiriki walitumia mbinu mbalimbali za utafiti tatuzi kama vile ugunduzi, usaili, majadiliano ya vikundi na ramani katika kufikiria njia za kuwabaini na kuwaweka pahali panapohusika wanafunzi walioko nje ya skuli.

Mkufunzi awaelezee washiriki kwamba kamati ya elimu mjumuisho ya kila skuli ina jukumu la kufanya uchunguzi kwa ajili ya kutambua maeneo walipo wanafunzi walioko nje ya skuli.

Kitendo hiki kitawapa fursa washiriki, au vikundi vya washiriki, au kamati ya skuli au idara ya kuamua muelekeo wa utafiti wao utakuaje.

Mkufunzi awape washiriki maelezo yafuatayo:

- Kila mmoja afikirie kazi za awali alizofanya kutokana na moduli hii na aweke kumbukumbu (za kifikra) ambazo zilihusu kipindi kilichohusika.
- Fikiria vipindi vyote vilivyofundishwa, pamoja na kikundi chako amueni, jambo gani ambalo utafiti tatuzi ungelenga. Fikiria sababu na iwapo ndio lengo ambalo utaweza kulichunguza. Unaweza kuzingatia juu ya msaada gani wa mpito unapatikana katika skuli yako, na wapi kuna mapungufu ya msingi. Hii itakusaidia kuweza kupanga/kupiga hatua zaidi.
- Vilevile unaweza kuzingatia njia za kushirikisha wanafunzi, ukijumuisha wale ambao wamepata elimu ya mpito au ambao wamehusishwa katika utafiti tatuzi juu ya upatikanaji wa matokeo.
- Jadiliana na makundi mengine juu ya maamuzi yako, na hakikisha yanatekelezeka. Jaribu na fikiria njia za ubunifu za kushirikisha wanafunzi katika kufanya utafiti.

Mkufunzi aandike katika ubao au chati mgeuzo mada ya utafiti iliyochaguliwa na kila kikundi. Kikundi chote kinaweza kujadili iwapo mada zilizochaguliwa ni zenye manufaa. Mwisho mkufunzi awatake washiriki kuwasilisha mitazamo ya tafiti zao katika mfumo wa uchunguzi au maswali.

**Maelezo kwa ajili ya wakufunzi*:***
Maswali yafuatayo yanaweza kujitokeza katika vipindi vilivyosomwa ndani ya moduli hii:

- Vitendea kazi gani vya ziada vilivyopo vya kusaidia wanafunzi katika elimu hii ya mpito?
- Je mfumo wa mazingira rafiki kwa ajili ya wanafunzi wapya unaendelezwa vyema katika skuli yangu? Ikiwa ndio, kwa nini? Ikiwa hapana kwa nini iwe hivyo?

- Je tathmini ya hatua ya mwanzo inayoeleza mpango jumuishi wa mwalimu kwa ajili ya wanafunzi inafahamika?
- Je wazazi na wanafunzi wapya wanapokelewa vizuri na kupewa taarifa za kutosha za mtaala wa skuli?
- Je skuli pamoja na walimu huwashauri wanafunzi namna ya kuifanya skuli kuwa ni mazingira rafiki zaidi na shirikishi? Ikiwa ndio, toa mifano na ushahidi namna skuli inavyoleta matokeo mazuri ya kujifunza. Ikiwa hapana, hatua gani zitumike za kuwashauri walimu?
- Je wanafunzi wapya wanajuilishwa majukumu yao mapema? Ikiwa hapana kwa nini hawakujuilishwa?
- Je walimu wanafahamu mbinu za kukuza upatikanaji wa lugha za ziada kwa wale wanafunzi wasiofahamu lugha ya kufundishia?
- Je walimu na jamii ya skuli inafahamu kwamba baadhi ya wanafunzi wanaacha masomo? Je wanafahamu kuwa ni jukumu lao kuwarejesha skuli?

# Vitendo vya Kuchangamsha

Kichangamshi ni kitendo, mchezo au mazoezi ya hiyari ambayo hutumika kuwakaribisha na kuwaandaa walimu katika mazungumzo na mchanganyiko wa makundi katika warsha, mafunzo, mkutano au tukio jengine.

## Matayarisho ya 1: 'Katika basi!'

Muda: Dakika 20

Haya ni mazoezi ya kuchangamsha, kufurahisha na kukuza mashirikiano. Yanatoa mfano wa njia muhimu na kusaidia kujifunza lugha. Yanaweza kufanywa nje ikiwa darasani hakuna nafasi ya kutosha, kila mshiriki atatoka nje na kiti chake.

Mkufunzi awatake washiriki kukaa katika jozi na kupanga viti vyao katika mistari miwili iliyonyooka yenye kuwakilisha abiria waliomo ndani ya basi. Washiriki wakae katika viti vyao pamoja na marafiki zao. Jozi ya wanafunzi iliyopo mbele ya mstari ndio waliopo mbele ya basi na jozi ya wanafunzi iliyopo nyuma ya mstari ndio waliopo nyuma ya basi.

Mkufunzi aipe kila safu mlalo nambari yake akianzia na 'nambari 1' mbele ya basi. Kwa hivyo, ikiwa kuna safu mlalo 20 (kwa walimu 40) safu mlalo ya nyuma itakuwa na nambari '20'.

Kila mtu atakapokuwa tayari ametulia, mkufunzi awaeleze washiriki kuwa yeye ni mwenye kauli ya mwisho, hata kama atakosea. Mkufunzi ataeleza muda wa kumaliza mazoezi (mfano dakika 10) na kutegesha saa (au kuchagua mtunza wakati ambaye anaweza kuwa hakimu wa mazoezi hayo, kwa mfano, iwapo kuna idadi ya walimu isiyogawika kwa mbili).

Kisha mkufunzi atataja nambari (katika nambari za safu mlalo, kwa mfano; kuanzia 1-20 kama kutakua na safu mlalo 20) watu au abiria walio katika nambari zilizotajwa haraka watanyoosha mikono yao wote kwa pamoja. Iwapo mmoja kati ya wawili hao atachelewa kunyoosha mkono wote wawili watapaswa kurudi nyuma ya basi, iwapo mmoja wao atakosea. Mfano, mtu atanyoosha mkono kimakosa au kutonyoosha panapohitajiwa kunyoosha, yeye na mwenzake watapaswa kurudi nyuma ya basi.

Wakati jozi zikirudi nyuma ya basi, hii ina maana kwamba wengine wataenda mbele ya basi. Washiriki hao wakija mbele ya basi nambari yao inakuwa ile ya safu mlalo mpya. Ni muhimu kwa mkufunzi kujaribu kuhakikisha kwamba washiriki walio safu mlalo ya mbele wanarudi nyuma ili kufanya uadilifu katika mazoezi na kwamba kila mmoja anapata fursa ya kusogea mbele ya basi. Muda unapoisha mchezo unamalizika na washindi ni wale walio mbele ya basi.

Mkufunzi anaweza kutumia mbinu tafauti za kuwakosesha watu wakati mchezo unaendelea. Mfano, aongeze sheria katikati ya mchezo kama vile, 'fuateni maelekezo ikiwa tu nitakuwa nimenyoosha mkono wangu ninapotoa maelekezo'. Mbinu nyengine za kuwababaisha washiriki ni kuwatajia nambari tafauti katika safu.

Mkufunzi anaweza kuwaeleza washiriki kwamba mchezo huu unaweza kuchezwa na wanafunzi na ukaleta mafanikio. Kwa sababu unakuza kazi za vikundi, usikivu na utambuzi wa nambari. Pia, unasaidia wanafunzi wapya katika darasa na ambao wapo katika hatua ya awali ya kujifunza lugha ya kujifunzia. Mfano; lugha za makabila, Kiswahili, Kiarabu na Kiingereza.



*Matayarisho ya mchezo wa Katika Basi*

**[Maelezo ya picha: Washiriki 22 wa kike na kiume wamekaa katika viti vilivyopangwa vinavyowakilisha basi, viti hivi vimepangwa katika safu 2 ambazo ni jumla ya safu 12 zinazoonekana.]**

## Matayarisho ya 2: 'Kikundi cha…'

Muda: Dakika 15

Haya ni mazoezi ya kuchangamsha ambayo yanamfanya mkufunzi kuvipanga tena vikundi ambapo washiriki watafanya kazi na watu tafauti. Kwa mfano, ikiwa jambo hilo litafanyika katika siku ya pili ya warsha, ni mazoezi mazuri ya kufurahisha na kutumika skuli ili kuimarisha mashirikiano miongoni mwa wanafunzi na kuimarisha uhusiano mwema kati yao.

Mchezo huu ufanyike katika sehemu huru (isiyo na vikwazo) yenye nafasi ya kutosha ili kuwawezesha walimu kupita kwa haraka kuelekea kwenye vikundi vyenye ukubwa tafauti.

Mkufunzi awaarifu washiriki kuzunguka nje ya vikundi mpaka waambiwe kuingia katika vikundi hivyo.
Mkufunzi awatake washiriki kuunda vikundi kwa kutumia vigezo tafauti. Kwa mfano wenye umri sawa, urefu wa aina moja, wenye urefu sawa nywele rangi sawa, wapenzi wa timu moja ya mpira, wenye kuvaa viatu vyenye ukubwa sawa, wenye idadi sawa ya kaka na dada, na wale ambao wanatoka masafa ya aina moja kuelekea skuli.

Wanapomaliza kufanya hivyo, mkufunzi atawataka washiriki kwa mara nyengine tena kuzunguuka darasani mpaka waamrishwe tena.

Ni muhimu kuanza kuwagawa katika makundi madogo, lakini mkufunzi anaweza kuongeza kugawa vikundi vikubwa zaidi ambapo washiriki wataulizana maswali kwa kina.

Baada ya kutolewa agizo la kuunda vikundi tafauti, badilisha agizo na badala yake uwatake washiriki kuunda vikundi vyenye idadi maalumu. Mfano, vikundi vya watu 4 - 10 na kadhalika. Waambie washiriki kwamba wakiambiwa kutengeneza vikundi vyenye idadi maalumu wafanye hivyo haraka iwezekanavyo ili mmoja asije kuachwa nyuma, kwa sababu si kila mshiriki ataweza kujiunga na kikundi ikiwa idadi hairuhusu. Kwa mfano kuna washiriki 32 na wanatengeneza kikundi cha watu 10, washiriki 2 wataachwa (hawatojiunga na kikundi).

Mwisho, mkufunzi awatake washiriki kuunda kikundi chenye idadi anayoitaka kufanya kazi nayo, na vikundi hivi ndio washiriki ambao mkufunzi atafanya kazi nao.

Mkufunzi awashukuru wale wote waliochukua juhudi kwa moyo wa dhati wa kufanikisha mazoezi haya.

# Vielelezo

Moduli

3

# Kielelezo nambari 3.1: Kufafanua mambo mbalimbali: Ni nani watoto walio nje ya skuli na kwanini wapo nje ya skuli?

## Utangulizi

**Duniani**: "Kuna watoto na vijana milioni 264 ambao hawaendi skuli…"[6]
**Zanzibar**: "Watoto 35,732 wapo nje ya skuli"[7]

Watoto walio nje ya skuli ni dhana pana sana, kwa kawaida inamaanisha ni watoto ambao hawendi skuli rasmi. Hata hivyo, kumekuwa na mbinu tafauti na muda mwengine mbinu hizo hutafautiana katika kufafanua watoto walio nje ya skuli na kuwapima. Kwa mfano, kabla ya 2005, mashirika makubwa kama vile UNICEF na UNESCO walikuwa wakipima watoto walio nje ya skuli kwa lengo la kushiriki katika skuli za msingi, ambayo ilimaanisha kuwa watoto wenye umri wa msingi wanahudhuria viwango rasmi vya masomo isipokuwa msingi (yaani, msingi awali au sekondari) kwa takwimu zilizingatiwa kuwa nje ya skuli[8]. Ingawa mbinu za kisasa zaidi za kufafanua na kupima watoto walio nje ya skuli zimekuwa zikitengenezwa, kama takwimu zote, ni muhimu kukumbuka kuwa vipimo vya watoto walio nje ya skuli havipaswi kuchukuliwa tu kwa mtazamo wa kawaida. Wanahitaji kuzingatiwa kwa undani zaidi juu ya jinsi wamejengwa na nini hasa, wanapaswa kukipima.

Ingawa kuna kutokubaliana juu ya kuwaainisha na kuwapima watoto walio nje ya skuli, ni muhimu kutizama kwa ufafanuzi wa jumla na mifumo ili kuelewa upana na uhalisia wa tatizo na jinsi ya kulitatua.

Neno watoto walio nje ya skuli inajumuisha watoto ambao hawajawahi kuhudhuria skuli na wale ambao wameacha kuhudhuria skuli. UNESCO imebainisha aina tatu ya watoto walio nje ya skuli:

---

[6] UNESCO (2017) *Accountability in Education. Meeting our Commitments. Global Education Monitoring Report, 2017/18*, http://unesdoc.unesco.org/images/0025/002593/259338e.pdf

[7] UNICEF, Educate A Child & Revolutionary Government of Zanzibar 'Zanzibar joins the 'zero out-ofschool'- initiative' (unicef.org) (accessed December 2021)

[8] UNESCO (2005). *Children Out of School: Measuring Exclusion from Primary Education,* UNESCO Institute for Statistics, Montreal. http://uis.unesco.org/sites/default/files/documents/children-out-of-schoolmeasuring-exclusion-from-primary-education-en_0.pdf

- waliocheleweshwa kupelekwa skuli.
- walioacha kwenda skuli.
- ambao hawajawahi kwenda skuli[9].

Japokuwa suala hili linaweza kuonekana kuwa limenyooka vizuri, inakuwa ni vigumu zaidi tunapofikiria sababu ya vikwazo vinavyowazuia watoto kwenda skuli. Kuna njia tafauti zinazowezekana za kuainisha vikwazo na sababu zao za msingi. Kwa vyovyote vilivyoundwa, vikwazo hivi havitoepukana baadhi yao kuingiliana, au kuunganishwa sana na hakuna kimoja kati yao kinachopaswa kuzingatiwa kama cha pande zote. Mfano wake itakuwa, ikiwa mtoto yuko nje ya skuli kwa sababu familia yake inahama kutoka eneo moja kwenda jengine, mchakato wa uhamiaji unaweza kuchukuliwa kuwa ni kikwazo, lakini sababu za msingi za kuhama kwa familia hiyo inaweza kuwa umasikini, au labda mizozo katika mkoa wao wanaoishi, au vyote viwili.

> "Tafauti nyingi kwa kawaida huingiliana, na kusababisha hali ngumu kwa pande zote mbili za ubaya ambazo zinaweka vikwazo vya masomo na kupoteza fursa za elimu."

Kwenye maeneo mengine ya elimu mjumuisho, ni muhimu kukumbuka kwamba sababu yoyote ya mtoto kuwa nje ya skuli, siku zote ni mfumo ambao ndio wenye tatizo, na sio mtoto. Kwa hiyo, kama mtoto yupo nje ya skuli kwa sababu ni mlemavu na skuli haiwezi kumsimamia ahudhurie, basi tatizo litakuwa ni la skuli na mfumo wa elimu na sio mtoto binafsi. Hivyo, ikiwa tunazingatia, kwa mfano, kwamba lugha ya kwanza ya mtoto au lugha mama inaweza kuwa kikwazo kwa mtoto huyo kuwapo skuli katika maeneo ambayo lugha ya kufundishia skuli ni tafauti na lugha mama, shida sio lugha mama, lakini mfumo wa elimu haubadiliki kwa kukidhi kuchukua watoto kutoka vikundi vya lugha tafauti na lugha kuu ya kufundishia skuli.

[9] Ibid, p.27

## Makundi ya vikwazo vya masomo kwa watoto

Kuna aina kadhaa pana, mtambuka za vikwazo kwa masomo ya wanafunzi ambapo vikwazo mahsusi zaidi vinaweza kuwekwa. Ili kujadili masuala haya mapana, yamewekwa hapa katika sehemu tatu zifuatazo:

- mazingira na rasilimali;
- mtazamo na kiutendaji
- Sera.

Kuna uwezekano kuwa tayari umekutana na dhana ya vikwazo vya mjumuisho wakati wa mafunzo mengine juu ya elimu mjumuisho. Vikwazo vya mjumuisho ni vikwazo vinavyoathiri **uwepo** wa watoto skuli, **ushiriki** wao katika mchakato wa kujifunza, na **kufaulu** kwao.

Kwa ukumbusho wa haraka, vikwazo hivi ni:

- **Vikwazo vya kimazingira**: majengo ya skuli, mazingira ya skuli na vyoo ambavyo havitumiki;
- **Vikwazo vya kirasilimali**: mfano, upungufu wa walimu, madarasa makubwa;
- **Vikwazo vya kitabia**: mfano, woga, fedheha, aibu, huruma, matarajio madogo;
- **Vikwazo vya kisera**: mfano, ratiba za skuli zinazobadilika ukosefu wa usomeshaji kwa lugha mama;
- **Vikwazo vya kiutendaji**: mfano ukosefu wa ushirikishwaji na mashirikiano kwenye kusomesha

Katika moduli hii ya mafunzo tunaangalia zaidi vikwazo ambavyo huwafanya watoto wawe nje ya skuli japokuwa katika uhalisia vikwazo vyao vingi ni sawa na vikwazo vya mjumuisho.

## Mazingira na rasilimali

Neno mazingira hapa linaweza kutumika kumaanisha yaliyotengezwa na binaadamu na yale ya asili. Hii inahusisha eneo (ukanda), nchi, jiji, kijiji au mafikio ambayo yanaweza kuwa mjini au vijijini[10].

Mtoto anapoishi inaweza kuwa ni kipimo cha kuangalia iwapo mtoto huyo yupo skuli au hayupo. Kwa mfano, kwa kawaida kuna mwamko mkubwa wa skuli na urahisi wa kuzifikia skuli katika maeneo ya mjini kuliko vijijini. Matokeo yake sasa, kwa mujibu wa takwimi, kuna watoto wengi walio nje ya skuli katika maeneo ya vijijini kuliko maeneo ya mijini. Mbali na hayo, kwenye maeneo ya ndani ambapo masafa baina ya jamii na jamii yanaweza kuwa makubwa na usafiri ni mgumu kwa njia ya ardhi (kama vile milima mirefu ambayo ni ngumu kuivuka), ukosefu wa miundo mbinu (kama vile barabara na madaraja) na pia hali ya hewa (mfano vipindi virefu vya baridi) inaweza kuwa ni vigumu au kutowezekana kwa baadhi ya watoto kuweza kwenda katika skuli chache ambazo zipo. Mfano wa vikwazo hivyo vya kimazingira vinachangia kuwafanya watoto kuwa nje ya skuli katika maeneo.

Ingawa kunaweza kuwa na tafauti kubwa katika idadi ya watoto walio nje ya skuli kati ya mikoa tafauti katika nchi hiyohiyo, tafiti zinashauri kuwa kwa ujumla, katika nchi ambazo jumla ya viwango vya kitaifa vya mahudhurio ya skuli ni kubwa, viwango vya mahudhurio ya skuli huwa juu katika mikoa yote nchini (Wils na wenzake, 2006) [11] . Tafauti kubwa katika viwango vya mahudhurio ya skuli miongoni mwa mikoa hujitokeza katika nchi ambazo viwango vya jumla vya mahudhurio ni duni.

Rasilimali – ikijumuisha uchumi au vifaa, binaadamu na rasimali za kitamaduni – inaweza kuathiri ama watoto walipo au wasiokuwapo skuli. Rasimali za uchumi za familia na jamii zinaweza kuamua kama familia inaweza au haiwezi kumudu kuwapeleka watoto wao skuli au kama jamii ina skuli kwa ajili ya watoto wao kuhudhuria. Kiuchumi familia za kimasikini zinategemea watoto wake kufanya kazi ili ziweze kuishi na kwa hivyo wanatilia mkazo kufanya kazi kwa watoto kuliko kuwapeleka skuli. Skuli ambazo zipo kwenye maeneo yenye uchumi mdogo zinaweza kupata shida ya upungufu wa rasimali za vifaa kama

[10] UNESCO, 2005.

[11] Wils, A., Zhao, Y., and Hartwell, A. (2006) ‘Looking Below the Surface: Reaching the Out-of-School Children’. Collaborative Working Paper CWP-02-01. Education Policy and Data Center.

vile kwenye ufundishaji na vifaa vya kujifunzia, madarasa na huduma nyenginezo, kwa kutoa msaada katika maeneo yote yenye watoto wenye umri wa kwenda skuli.

Suala la rasilimali watu ambalo linaweza kuathiri watoto kuhudhuria skuli ni ukosefu wa walimu au ukosefu wa walimu wataalamu. Familia bila rasilimali za kitamaduni, kama vile kujua kusoma na kuhesabu, inayotokana na uzoefu wa elimu rasmi, wanaweza kushindwa kuwasaidia watoto wao kujifunza na hii pia inaweza kuathiri watoto wasiohudhuria skuli, au kuacha kwenda skuli hii pia inahusiana na mtazamo na uzoefu.

## Mitazamo na uzoefu

**Mikabala** ya watu, familia, na jamii inaweza kuwa ni sababu kuu ya kuwafanya watoto wawe nje ya skuli. Kwa mfano, baadhi ya familia na jamii zinaamini kwamba watoto wenye ulemavu hawapaswi kwenda skuli. Katika jamii nyengine, familia zinaweza kuhisi kwamba watoto wa kike wanatakiwa kubaki nyumbani na sio kwenda skuli.

Mfano mwengine wa mitazamo inaweza kupelekea watoto kuwa nje ya skuli, ni watoto ambao huchokozwa na wenzao au walimu ndani ya skuli kwa sababu wanatokea kwenye makundi madogo ya kikabila, kidini au lugha. Watoto ambao wanachokozwa kwa njia hii wanaweza kuacha skuli ili kuepusha kunyanyaswa zaidi. Mitazamo hiyo inaweza kuakisi upendeleo wa wale wanaowazuia, na sio uwezo sahihi wa watoto wa kwenda na kufaidika na skuli. Hata hivyo, mitazamo hasi inaweza kuwafanya watoto wasiende skuli.

Kutokana na mitazamo yao na uzoefu wao binafsi wa elimu wazazi, walezi au watoa huduma ambao hawajapata kwenda skuli wanaweza kuona umuhimu mdogo kupeleka watoto wao skuli.  Utafiti unaonesha kwamba, uzoefu wa mama katika elimu ni sababu muhimu ambayo inaweza kuainisha kama mtoto anaweza au hawezi kwenda skuli[12]. Utafiti wa UNESCO wa mwaka 2015 umegundua kwamba, dunia nzima watoto walio na umri wa kwenda skuli ambao mama zao hawana elimu ni mara mbili ya wale watoto wenye mama ambao wana elimu japo ndogo.

[12] UNESCO, 2005.

Ni mara nyingi ujinga na woga husababisha kukuza upendeleo na mitazamo hasi. Katika njia inayoendana, ujinga na woga huathiri sera na mifumo ya kielimu.

## Sera na mifumo

Sera za kitaifa za ndani na hata za skuli zinaweza kuchangia tatizo la watoto kuwa nje ya skuli. Kwa mfano, kama nchi haina sera ya elimu bila malipo, watoto wengi watakuwa hawawezi kuhudhuria skuli kwa sababu wao na wazazi au walezi na watoa huduma wao hawawezi kumudu kulipia ada ya skuli.

Mfano kutoka ngazi ya skuli inaweza kuwa na sera ya skuli ya kulazimisha kuanza skuli mapema kwa siku za skuli na kwa wakati huohuo ikawa inashughulikia watoto wanaochelewa kuja skuli. Sera kama hiyo inaweza kuwatenga watoto ambao wanaishi mbali na skuli ambao huenda na kurudi skuli kwa miguu.

Utekelezaji wa elimu hususani kufundisha na kujifunza, ina athari kubwa kwa masomo ya wanafunzi wa skuli. Baadhi ya watoto wanachagua kutokwenda skuli kwa sababu wanahisi wanachoka, wanatengwa au wapo sehemu ambayo haiwafai kuwepo. Wanaweza kuhisi kusomeshwa au elimu haiwasaidii na ina maana ndogo sana katika maisha yao. Hasa, mitindo migumu ya kufundisha inaweza kusababisha watoto kujitenga darasani na kuacha masomo. Au, kwa mfano mwingine, watoto hawawezi kwenda skuli kwa kuogopa adhabu ya bakora. Masuala haya yote yanahusiana na mifumo, na mara nyingi mifumo mibaya ya kufundisha ni matokeo ya mafunzo duni ya waalimu.

## Vikwazo maalumu vya wanafunzi katika kujifunza

Miongoni mwa vikwazo vingi vya ujifunzaji kwa mtoto, kuna vikwazo maalumu. Ni muhimu kusisitiza tena kwamba masuala yote mawili jumla na mahsusi yanayoathiri uhudhuriaji wa watoto skuli yanahusiana, na hili huonekana zaidi tunapojaribu kufatilia mtiririko wa sababu au vyanzo.

Badala ya kuwa rahisi, sababu moja ya kumfanya mtoto kuwepo nje ya skuli, kuna mtiririko wa sababu na athari. Kwa mfano, upungufu wa walimu wenye mafunzo inaweza kupelekea skuli kuwa na mwalimu mmoja asiye na ujuzi wa kutosha kuwajibika kwa madarasa yenye wanafunzi wengi. Hii kwa upande mwengine, hupelekea kwa baadhi ya watoto kupata elimu iliyo duni; ambayo inasababisha kuacha kuhudhuria skuli kwa kutengwa na kuwa nyuma

kimasomo. Wazazi au walezi na watoa huduma wao wanahisi haina maana kuwalazimisha kwenda skuli. Inawezakana pia skuli kuwepo eneo la mbali sana kutoka makaazi ya baadhi ya watoto na hivyo kuwa ni vigumu kwa wao kuweza kufika, na hii pia inasababisha wasihudhurie skuli.

Katika mifano ya awali, tunaweza kusema kwamba usomeshaji mbaya ni sababu ya watoto kuacha kuhudhuria skuli. Hata hivyo, kauli kama hii haizungumzii sababu ya usomeshaji mbaya [kama vile upungufu wa walimu, uhaba wa mafunzo ya jinsi ya kudhibiti madarasa makubwa na usomeshaji unaozingatia mtoto], au sababu nyenginezo zinazochangia kama vile mitazamo ya wazazi au walezi au watoa huduma kuhusiana na elimu rasmi.

Sasa tuangalie baadhi ya vikwazo vyengine vya watoto kwenye kusoma. Hivi hujumuisha:

- umri
- Mtazamo wa kitabaka la kijamii na kiuchumi
- migogoro na majanga
- Mahitaji ya ziada kama vile mahitaji maalum ya kielimu na ulemavu
- kabila, dini na utamaduni;
- jinsia
- afya
- lugha
- uhamiaji
- umaskini

## Umri

Umri unaweza kuwa ni sababu muhimu ya mtoto kuwa nje ya skuli, hasa kuhusu watoto kuacha kwenda skuli. Kuna ushahidi kwamba mtoto akichelewa kupelekwa skuli [kama vile kucheleweshwa zaidi ya watoto wa rika lao], au kurudia madarasa, mara nyingi hupelekea watoto kuacha kuhudhuria skuli kabla kumaliza masomo yao[13]. Vilevile, katika mitazamo myengine kuna shindikizo kwa watoto kufanya kazi katika umri mdogo sana, kitu ambacho husababisha watoto hao wasihudhurie skuli.

## Tabaka la Kijamii na Kiuchumi

Katika mazingira mengine, masuala ya tabaka la kijamii na kiuchumi huamua ikiwa watoto wanaweza kupata masomo au la. Kwa ujumla, watoto waliozaliwa katika familia za hali ya chini kijamii na kiuchumi zina uwezekano mdogo wa kuwa skuli, au kukaa skuli kwa muda wote, kuliko watoto wa matabaka ya juu ya kiuchumi.

## Migogoro na Majanga

Migogoro (kama vita vya wenyewe kwa wenyewe) na majanga (kama mafuriko na matetemeko ya ardhi) inaweza kuwa sababu kuu, au sababu inayochangia kuwazuia watoto wasiende skuli. Katika maeneo yenye migogoro au majanga, skuli zinaweza kuharibiwa, kubomolewa au kutoweka kabisa. Usafiri wa kwenda na kurudi skuli unaweza kuwa sio salama au kutowezekana kutokana na mapigano yanayoendelea, mabomu ya ardhini, na uharibifu wa miundombinu kama vile majengo ya skuli, madaraja, barabara, na mengineyo. Hata wakati skuli zinapofunguliwa, huenda zisiwe sehemu salama kwa wanafunzi kwa mnasaba wa migogoro, kwa mfano, skuli zinaweza zikalengwa katika vurugu. Zaidi ya hayo, baadhi ya nchi wanafunzi wanaweza kulazimishwa kupigana wakiwa wanajeshi watoto.

[13] UNESCO, 2005

“Ingawa hakuna idadi maalumu, mamia na maelfu ya watoto wa chini ya umri wa miaka 18 wanafanya kazi katika majeshi ya serikali au vikundi vya uasi. Baadhi yao ni wadogo sana wa umri wa miaka 8. Tangu mwaka 2001, ushiriki wa watoto wakiwa majeshi umeripotiwa katika mapigano karibuni 21 katika kila kanda ya dunia.

Katika baadhi ya nchi watoto ambao waliwahi kuwa majeshi wanapelekwa katika programu maalumu ili kupatiwa matibabu ya kisaikolojia na kuwasaidia kukutana na familia zao na kurudi skuli kupatiwa elimu mbadala, pamoja na kurudi katika maisha ya heshima. Hata hivyo, watoto wengi hawakupata programu hizo. Huenda ikawa hawana njia ya kujikimu wenyewe na wakabaki katika hatari ya kuajiriwa tena katika jeshi.”

## Watoto wenye mahitaji ya ziada

Watoto wenye mahitaji ya ziada ya kielimu na/au ulemavu mara nyingi hutengwa katika elimu. Hii inaweza kutokana na sababu nyingi, zikiwemo:

- Mitazamo ya kijamii na Imani – kwenye baadhi ya sehemu inaaminika kuwa watoto wenye ulemavu hawawezi na hawatakiwi kwenda skuli kujifunza;
- Upatikanaji wa skuli– skuli zinaweza kuwa hazipatikani kiurahisi kwa baadhi ya watoto wenye ulemavu;
- Ukosefu wa rasilimali na uwezo – baadhi ya skuli {au zinaaminika zinakosa} rasilimali ya vifaa na uwezo; kwa kuangalia wingi wa wafanyakazi na ufundishaji, kwa kuweza kuwajumuisha ipasavyo wanafunzi wenye mahitaji ya ziada.

Wanafunzi wenye matatizo ya mihemko na tabia mara nyingi hutengwa katika elimu kwa sababu wanaonekana kuwa ni wasumbufu na wenye hatari kwa wao wenyewe, kwa watoto wengine na kwa wafanyakazi wa skuli. Hili mara nyingi ni suala linalohusiana na rasilimali na mafunzo, wafanyakazi na msaada unaofaa.  Skuli zinaweza kuwachukua na kuwajumuisha wanafunzi wenye matatizo ya mihemko na tabia.

## Ukabila, Dini na Utamaduni

Wanafunzi wanaweza kutengwa skuli kwa sababu ya makabila yao. Hili mara nyingi ni suala la vikundi vya watu wachache vya kikabila. Sababu nyengine kama vile migogoro ya kikabila inaweza kuzidisha matatizo na kufanya kabila fulani kuwa nje ya skuli. Hata kama sio waziwazi, hutengwa skuli, wanafunzi wengine huamua kuacha kwenda skuli wakikutana na ubaguzi na unyanyasaji kutokana na ukabila.

Wanafunzi huenda pia wakawa nje ya skuli kwasababu ya dini yao. Hii inaweza kuwa kwasababu watoto wanatengwa katika kuhudhuria skuli au kuacha kwenda skuli kutokana na mateso ya kidini. Au kwa mfano, baadhi ya wazazi au walezi au watoa huduma wanawazuia watoto wao kwenda skuli kwa sababu elimu iliopo haikidhi mahitaji ya imani za kidini za familia zao.

Inaweza kuwa masuala yanayohusiana na suala la mitazamo ya kiutamaduni na kimawazo. Mara nyingi, masuala ya kiukabila, kidini na kiutamaduni [na lugha] yanaingiliana.

## Jinsia

Kiujumla ukosefu wa usawa wa kijinsia kwa wanafunzi walio nje ya skuli umekuwa ukipunguzwa tangu miaka ya 1990, bado kuna idadi kubwa ya wanafunzi wa kike walio nje ya skuli duniani. Athari za jinsia katika kujifunza hutafautiana kimkoa. Mikoa mengine ina idadi kubwa zaidi ya wanafunzi wa kike walio nje ya skuli, na mikoa mengine ina usawa wa watoto wa kike wa kiume ndani na nje ya skuli, au hata asilimia kubwa zaidi ya wanafunzi wa kiume walio nje ya skuli, hususan katika nchi zilizoendelea.[14]

Hata hivyo, mitazamo hasi ya tamaduni zenye madhara yanayohusiana yanaendelea kuathiri sana wanafunzi wa kike na upatikanaji wao wa masomo. Kwa mfano, ndoa za utotoni ambazo watoto wa kike wenye umri wa miaka minane au tisa katika nchi nyengine wanalazimishwa kuolewa, kati ya athari nyengine mbaya kwa maisha ya watoto wa kike, hupunguza sana uwezekano wao wa kuhudhuria au kubaki skuli.

[14] UNESCO, 2005

## Afya

Afya mbaya, kwa sababu ya utapiamlo na maradhi, huwazuia wanafunzi wengi kwenda skuli. Kwa kuongezea, mara nyingi kuna unyanyapaa na chuki zinazoambatana na magonjwa fulani, hususan VVU na UKIMWI, ambavyo huchangia kuwatenga wanafunzi na skuli.

Kama ilivyo, vikwazo vingi kwa wanafunzi wanaohudhuria skuli, afya zao mara nyingi huunganishwa na matokeo ya moja kwa moja ya vikwazo vyengine, kama vile umaskini, majanga na migogoro.

## Lugha

Lugha ya kufundishia skuli, inaweza kuwa kikwazo kwa watoto kuhudhuria skuli. Kama lugha ya kufundishia skuli ni tafauti na lugha ambayo mwanafunzi anayoizungumza nyumbani [lugha mama], mwanafunzi huyo hupata shida kujifunza na kufahamu na hivyo huacha kwenda skuli. Hii mara nyingi inaathiri wanafunzi wanaotoka katika makabila yenye lugha inayozungumzwa na wachache. Pia, suala la lugha mara nyingi linahusishwa na ukabila, dini na utamaduni.

## Uhamiaji

Mwenendo wa watu kutoka sehemu moja kwenda nyengine kutokana na sababu za kiuchumi, kukimbia majanga, migogoro, kwa sababu za kiutamaduni au mjumuisho wa sababu zote hizi, huwa ni vikwazo kwa wanafunzi kujifunza.

Kwa mfano, wanafunzi ambao wanalazimika kuhama kwa sababu ya majanga na migogoro katika nchi zao, mara nyingi huishia katika kambi za wakimbizi zinazoungwa mkono kimataifa katika nchi nyengine ambazo upatikanaji wa masomo unaweza kuwa mdogo. Hata hivyo hali hii huwa mbaya kwa wanafunzi ambao ni wakimbizi wa ndani ya nchi zao, kwani wana uwezekano mdogo wa kupata kambi za wakimbizi zinazoungwa mkono kimataifa. Hivyo hawana nafasi ya kupata masomo rasmi ikilinganishwa na watoto katika kambi rasmi za wakimbizi.

Hata wanafunzi ambao huhama kwa sababu tu familia ipate kazi wanaweza kujikuta wakiondoka skuli. Wanaweza kukabiliwa na vikwazo vya lugha au utamaduni, wazazi au walezi au watoa huduma wao hawawezi kumudu gharama zinazohusiana na elimu, au ukweli wa kuwa mahali pageni inaweza

kuwa vigumu kwa wazazi au walezi au watoa huduma wao kuelewa na kuzifikia huduma ambazo zinapatikana.

## Umasikini

Umaskini ni miongoni mwa vikwazo sugu na endelevu kwa wanafunzi kuhudhuria skuli. Hali ya uchumi ya watu katika familia, jumuiya za mitaani, mikoa, nchi na katika eneo kubwa la kijografia inaweza sana kuathiri wanafunzi kuwa au kutokuwa skuli. Katika maeneo maskini kiuchumi, kwa ujumla skuli zilizo na rasilimali ni chache na walimu wachache walio na mafunzo kuliko katika maeneo yenye rasilimali nyingi kiuchumi. Masuala haya yanachangia wanafunzi kuwa nje ya skuli. Familia nyengine hazina uwezo wa kupeleka wanafunzi wao skuli. Wanafunzi wanaweza kulazimishwa kufanya kazi badala ya kuhudhuria skuli. Hata wakati wanafunzi wanaokabiliwa na umaskini wa kiuchumi wanakwenda skuli, wana uwezekano mkubwa wa kuacha skuli kabla ya kumaliza kuliko wanafunzi wanaotoka katika familia tajiri kiuchumi.

Kama ilivyo vikwazo vyengine, umasikini nao ni kikwazo, zaidi ya sababu ya jiografia. Hata katika maeneo tajiri kiasi ambacho kwa ujumla kuna nafasi nzuri ya kusoma, kunaweza kuwa na mifuko ya umaskini na ufinyu unaosababisha wanafunzi wengine kuwa nje ya skuli.

Ulimwenguni kote, skuli zinazodaiwa kuwa ‘bure’ mara nyingi zina gharama zilizojificha, kama vile sare na vitabu vya kiada. Katika skuli nyengine, wanafunzi hawawezi kufundishwa ipasavyo, au wanaweza kufeli kwa makusudi ikiwa wao au wazazi au walezi au watoa huduma wao hawawezi kutoa rushwa kwa walimu.

# Kielelezo nambari 3.2: Orodha ya Vikwazo vya Kujifunza kwa Watoto

## Makundi Makuu ya Vikwazo vya Ujifunzaji kwa watoto

- Mazingira na rasilimali
- Mtazamo na uzoefu
- Sera na utendaji

## Vikwazo mahsusi vya kujifunza kwa wanafunzi

- Mtazamo wa umri
- Mtazamo wa kidarasa
- Migogoro na majanga
- Mtazamo kwa wanafunzi wenye mahitaji ya ziada
- Mtazamo wa kikabila, kidini na kiutamaduni
- Mtazamo wa kijinsia
- Afya
- Lugha
- Uhamiaji
- Umaskini

# Kielelezo nambari 3.3: Mfumo wa sera na sheria

## Sera na sheria za kimataifa

Boksi la maandishi lifuatalo linaorodhesha sera kuu za miundo ya sera na sheria kuu kimataifa:

**Utambuzi wa haki ya kupata elimu kimataifa**

"Haki hii imeanzishwa na mfululizo wa Mikataba ya Umoja wa Mataifa, kutoka Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu la mwaka 1948 hadi Mkataba wa Haki za Mtoto wa 1989, ambao ulipata hadhi ya sheria ya kimataifa mnamo mwaka 1990. Kulingana na Kifungu cha 28 cha Mkataba, serikali zina jukumu la kufanya elimu ya msingi kuwa ya lazima na ipatikane bila malipo kwa wote.

Inatambulika kwamba elimu ni muhimu kwa maendeleo ya binaadamu. Harakati ya Elimu kwa Wote na Malengo ya Maendeleo ya Milenia yameleta umakini mkubwa wa ushiriki wa kielimu na kukamilika. Elimu ya Msingi kwa Wote ni lengo la pili la Harakati za Elimu kwa Wote zote mbili ni za Jomtien katika mwaka 1990; imethibitishwa tena Dakar mwaka 2000 na Malengo ya Maendeleo ya Milenia, zilizopitishwa na Nchi Wanachama wa Umoja wa Mataifa mnamo mwaka 2000 na (UNESCO mwaka 2000; UN mwaka 2003)."

Kati ya mifumo na sera zote za kimataifa, Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Mtoto unaeleza kwa kina kuhusu viwango vya msingi vya haki za watoto ya kupata elimu, pamoja na haki nyeingine. Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Mtoto umeundwa na vifungu 54 vinavyozungumzia haki za watoto. Kifungu cha 28 cha Mkataba huu hususani unashughulikia haki ya kupata elimu. Lakini vifungu vyengine vingi pia vinagusia maswala ambayo yanaathiri elimu kama haki za watoto kwa afya na ustawi wao.

**Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Mtoto - Makala ya 28**

1. Nchi Wanachama zinatambua haki ya mtoto kupata elimu, na kwa nia ya kufikia haki hii kimaendeleo na kwa msingi wa fursa sawa, hususani kwa lengo la:-

a) Kuifanya Elimu ya Msingi iwe ya lazima na ipatikane bila malipo kwa wote.

b) Kuhimiza ukuzaji wa aina tafauti za Elimu ya Sekondari, pamoja na elimu ya Jumla na ya Mbadala, kuifanya ipatikane na kila mtoto, na kuchukua hatua zinazofaa kama vile kuanzishwa kwa elimu bila malipo na kutoa msaada wa kifedha katika hali ya uhitaji.

c) Kuifanya Elimu ya Juu ipatikane kwa wote kwa msingi wa uwezo kwa kila njia inayofaa.

d) Kufanya elimu na taarifa juu ya elimu mbadala kupatikana na muongozo wake kupatikana kwa watoto wote.

e) Kuchukua hatua za kuhamasisha mahudhurio ya kawaida skuli na kupunguzwa viwango vya kuacha masomo.

2. Nchi Wanachama zitachukua hatua zote zinazofaa kuhakikisha kwamba nidhamu ya skuli inasimamiwa kwa njia inayolingana na utu wa mwanadamu kulingana na Mkataba uliopo.

3. Vyama vya Kimataifa vitakuza na kuhimiza ushirikiano wa kimataifa katika maswala yanayohusiana na elimu, hususan kwa nia ya kuchangia kuondoa ujinga na kutokujua kusoma na kuandika ulimwenguni kote na kuwezesha upatikanaji wa maarifa ya kisayansi na kiufundi na njia za kisasa za kufundisha. Katika swala hili, dhima maalumu itachukuliwa kwa mahitaji ya nchi zinazoendelea.[15]

[15] www.unicef.org.uk/wp-content/uploads/2010/05/UNCRC_united_nations_convention_on_the_rights_of_the_child.pdf

## Mfumo wa Sera, mipango na sheria Zanzibar

Zanzibar iliungana na Tanganyika kufanya Muungano wa Tanzania mwaka 1964, lakini ni nchi yenye mamlaka kamili. Ina serikali yake, utawala wake ambapo inaongozwa na rais wa Zanzibar na ina mfumo wa mahakama. Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania imesaini mkataba wa kimataifa wa haki za watu wenye ulemavu na mikataba mingine mbalimbali.

Serikali ya mapinduzi ya Zanzibar ina wajibu katika mambo ya ndani na kusimamia maendeleao ya sekta muhimu ikiwemo elimu, ukitoa elimu ya juu ambayo bado ni jambo la muungano.[16]

Ni muhimu kutambua kwamba mfumo wa elimu wa Zanzibar upo katika kipindi cha mpito cha miaka 12 ya elimu ya lazima kama ilivyoelezwa na sera ya elimu ya 2006 (miaka 2 ya maandalizi, miaka 6 ya msingi na miaka 4 ya sekondari).

Mifumo ya sera za kitaifa na sheria ni kama ifuatavyo:

- Zanzibar ina sheria yake yenyewe (1985), ambayo kwa ujumla haizungumzii haki ya kupata elimu. Hata hivyo, sura ya 2 katika malengo ya msingi na miongozo ya kanuni kama vile kifungu kinachosema: "itasimamia sera ili kuhakikisha kwamba kila mtu anapata (.....) nafasi sawa ya elimu kwa wote" (Kifungu 10(6)).[17]

- Mwaka 2000, Serikali iliweka malengo ya 2020, ambayo yalidhamiria kuondosha umasikini hapa Zanzibar. Sera ya elimu ya (2006) iliandaliwa kwa kuzingatia Malengo hayo ya 2020 na MKUZA II, Mpango wa kukuza maendeleo wa Taifa. Mbali na malengo ya Zanzibar ya 2020, kuna lengo jengine la elimu la "ujumuishi na upatikanaji wa elimu bora na mafunzo katika stadi mbalimbali kwa lengo la kuimarisha maendeleo ya taifa.[18] Kwa kuzingatia MKUZA na malengo ya maendeleo endelevu (SDG) namba 4: kuhakikisha ujumuishi na elimu bora iliyo sawa na kuimarisha ujifunzaji endelevu kwa wote, mpango wa maendeleo wa Zanzibar (ZPDPII) umeweka matarajio ya serikali katika elimu kwa miaka mitano.

---

[16] OPM (2016). Utaiti wa Elimu Zanzibar

[17] Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (1985). Katiba ya Zanzibar

[18] Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Mpango wa Maendeleo ya Elimu Zanzibar II (ZEDP II) 2017/18-2021/22

- Mpango wa Maendeleo ya Elimu namba II (ZEDP II) umebaini kwamba kunakosekana usawa katika kujifunza, upatikanaji wa elimu na vifaa katika ngazi zote. Uwepo wa utafauti wa jinsia katika kujifunza na hali ya kutengwa, lakini kwa vile hali haiko sawa kwa maeneo yote, utafili zaidi unahitajika ili kufahamu sababu za kukosekana usawa huo.

- Watoto wenye ulemavu wana idadi kubwa ya kutengwa katika elimu kuliko inavyodhaniwa. Vikwazo vinavyowakumba watoto wenye ulemavu ni pamoja na miundombinu isiyofikika na upungufu wa vifaa na zana za kufundishia na kujifunzia. Mpango umejikita kutekeleza sera jumuishi ya taifa, kuwafunza walimu na wakaguzi juu ya elimu ya mjumuisho, kuandaa taarifa za miundombinu na kutoa kipaumbele katika upatikanaji wake.[19]

[19] Ibid

# Kielelezo nambari 3.4: Vikwazo vinavyolingana na haki

## Elimu, watoto walio nje ya skuli, na Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Mtoto

- Soma toleo linalohusu mtoto la makala ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Mtoto (hapa chini).
- Tafuta nakala zinazohusiana na elimu (wengine hufanya hivi moja kwa moja na wengine hufanya kwa njia isiyo ya moja kwa moja au la).
- Jadilini katika vikundi vyenu ni vikwazo vipi vinavyowafanya watoto wasiende skuli vinashughulikiwa na vifungu katika Mkataba wa Umoja wa Mataifa. (Rejea majadiliano ya zamani na rasilimali kwa ukumbusho juu ya vikwazo vinavyowezekana.)
- Inapowezekana, jaribu kulinganisha vikwazo na mifano uliyoitambua mapema kwa haki. Waandike katika nafasi chini ya haki zinazofaa.

**Kifungu cha 1**
Kila mtoto aliye chini ya miaka 18 ana haki hizi.

**Kifungu cha 2**
Watoto wote wana haki hizi, haijalishi wao ni nani, wanaishi wapi, wazazi wao wanafanya nini, wanazungumza lugha gani, dini yao ni ipi, iwe ni mtoto wa kiume au wa kike, ni nini utamaduni wao, ikiwa wana ulemavu, wawe matajiri au maskini. Hakuna mtoto anayepaswa kutendewa haki kwa msingi wowote

**Kifungu cha 3**
Watu wazima wote wanapaswa kufanya kile kinachofaa kwako. Wakati watu wazima wanapofanya maamuzi, wanapaswa kufikiria jinsi maamuzi yao yatavyowaathiri watoto.

**Kifungu cha 4**
Serikali ina jukumu la kuhakikisha haki zako zinalindwa. Lazima zisaidie familia yako kulinda haki zako na kuunda mazingira ambayo unaweza kukua na kufikia uwezo wako.

**Kifungu cha 5**
Familia yako ina jukumu la kukusaidia kujifunza kutumia haki zako, na kuhakikisha kuwa haki zako zinalindwa.

**Kifungu cha 6**
Una haki ya kuishi

**Kifungu cha 7**
Una haki ya kupewa jina, na hili linapaswa kutambuliwa rasmi na serikali. Una haki ya utaifa (kuwa unahusika na nchi).

**Kifungu cha 8**
Una haki ya kitambulisho - rekodi rasmi ya wewe ni nani. Hakuna mtu anayepaswa kukuondolea haki hii.

**Kifungu cha 9**
Una haki ya kuishi na wazazi wako, itakapokuwa ni vibaya kwako. Una haki ya kuishi na familia inayokujali.

**Kifungu cha 10**
Ikiwa unaishi katika nchi tafauti na wazazi wako, una haki ya kuwa nao mahali pamoja.

**Kifungu cha 11**
Una haki ya kulindwa dhidi ya utekaji nyara

**Kifungu cha 12**
Una haki ya kutoa maoni yako kwa watu wazima na kusikilizwa na kuchukuliwa kwa uzito maoni hayo.

**Kifungu cha 13**
Una haki ya kujua mambo na kushiriki kile unachofikiria na wengine, kwa kuzungumza, kuchora, kuandika au kwa njia nyingine yoyote isipokuwa kuwadhuru au kuwaudhi watu wengine.

**Kifungu cha 14**
Una haki ya kuchagua dini yako na imani yako. Wazazi wako wanapaswa kukusaidia kuamua lililo sawa, baya na nini ni bora kwako.

**Kifungu cha 15**
Una haki ya kuchagua marafiki wako mwenyewe na kujiunga au kuanzisha vikundi, madhali havina madhara kwa wengine.

**Kifungu cha 16**
Una haki ya kupewa faragha (siri)

**Kifungu cha 17**
Una haki ya kupata habari ambayo ni muhimu kwa maendeleo yako, kutoka kwenye redio, gazeti, vitabu, kompyuta na vyanzo vingine. Watu wazima wanapaswa kuhakikisha kuwa habari unayoipata sio hatari, na kukusaidia kupata na kuelewa habari unayohitaji.

**Kifungu cha 18**
Una haki ya kulelewa na wazazi wako kama inawezekana.

**Makala ya 19**
Una haki ya kulindwa kutokana na vitendo vya kuumizwa na kutendwa vibaya, mwilini au akilini.

**Makala ya 20**
Una haki ya kutunzwa na kusaidiwa ikiwa unaishi mbali na wazazi wako

**Makala ya 21**
Una haki ya kutunzwa na kulindwa ikiwa umechukuliwa au kulelewa kwenye vituo maalumu.

**Makala ya 22**
Una haki ya ulinzi maalumu na usaidizi ikiwa wewe ni mkimbizi (ikiwa umelazimishwa kuondoka nyumbani kwenu na kuishi katika nchi nyingine), pamoja na haki zote za Mkataba huu.

**Makala ya 23**
Una haki ya kupata elimu maalumu na utunzaji ikiwa una ulemavu, na pia haki zote katika Mkataba huu, ili uweze kuishi maisha kamili.

**Makala ya 24**
Una haki ya kupata huduma bora za afya, maji safi na salama ya kunywa, chakula chenye virutubisho, mazingira safi na salama, na habari kukusaidia kukaa vizuri.

**Makala ya 25**
Ikiwa unaishi katika vituo vya matunzo au katika hali nyengine mbali na nyumbani, una haki ya kuishi katika maeneo hayo, kupata uangalizi wa mara kwa mara ili kuona kama ndiyo inayofaa zaidi.

**Makala ya 26**
Una haki ya kusaidiwa na serikali ikiwa ni maskini au muhitaji.

**Makala ya 27**
Una haki ya chakula, mavazi, pahali salama pa kuishi na kupata mahitaji yako ya kimsingi. Hupaswi kudharauliwa ili usije kufanya mambo mengi ambayo watoto wengine wanaweza kufanya.

**Makala ya 28**
Una haki ya kupata elimu bora. Unapaswa kuhimizwa kwenda skuli kwa kiwango cha juu zaidi unachoweza.

**Makala ya 29**

Elimu yako ikusaidie uweze kutumia na kuibua vipaji na uwezo wako. Inatakiwa ikusadie kujifunza kuishi kwa amani na kulinda mazingira yaliyokuzunguka na kuheshimu watu wengine.

**Makala ya 30**
Una haki ya kufuata utamaduni wako, lugha na dini yako - au chochote utakachochagua. Vikundi vidogo na asilia vinahitaji ulinzi maalumu wa haki hii.

**Makala ya 31**
Una haki ya kucheza na kupumzika.

**Makala ya 32**
Una haki ya ulinzi kutokana na kazi inayokuumiza, na ni mbaya kwa afya yako na elimu. Ikiwa unafanya kazi, una haki ya kuwa salama na kulipwa haki yako.

**Makala ya 33**
Una haki ya kulindwa na dawa za kulevya na biashara ya dawa za kulevya.

**Makala ya 34**
Una haki ya kuwa huru kutokana na unyanyasaji wa kijinsia.

**Makala ya 35**
Hakuna anayeruhusiwa kukuteka nyara au kukuuza.

**Makala ya 36**
Una haki ya kulindwa kutokana na aina yoyote ya unyonyaji (kuchukuliwa faida).

**Makala ya 37**
Hakuna anayeruhusiwa kukuadhibu kwa adhabu kali za kikatili au zinazoweza kukuletea madhara.

**Makala ya 38**

Una haki ya ulinzi na uhuru kutokana na vita. Watoto walio chini ya miaka 15 hawawezi kulazimishwa kwenda kwenye jeshi au kushiriki katika vita.

**Makala ya 39**
Una haki ya kusaidiwa ikiwa umeumizwa, umepuuzwa au umetendewa vibaya.

**Makala ya 40**
Una haki ya msaada wa kisheria na kutendewa haki katika mfumo wa kisheria ambao unaheshimu haki zako.

**Makala ya 41**
Kama sheria za nchi yako zinaruhusu ulinzi bora wa haki zako kuliko vifungu vya Mkataba huu, sheria hizo zinapaswa kutumika

**Makala ya 42**
Una haki ya kujua haki zako, Watu wazima wanapaswa kujua kuhusu haki hizi na pia wakusaidie kujifunza juu ya haki hizo.

Makala ya 43 mpaka 54
Vifungu hivi vinaeleza jinsi serikali na mashirika ya kimataifa kama vile UNICEF hufanya kazi kwa kuhakikisha kuwa watoto wanalindwa na haki zao.

Adapted from UNICEF's 'UN Convention on the Rights of the Child in Child-friendly Language'
www.unicef.org/rightsite/files/uncrcchilldfriendlylanguage.pdf

## Kielelezo nambari 3.5: Kadi tisa za almasi – vikwazo vya watoto kuwepo skuli

Kadi zinatakiwa kukatwa vipande kabla hazijagawiwa kwa washiriki.

| | | |
|---|---|---|
| **Mtazamo wa kiumri** | **Mtazamo wa darasa** | **Migogoro** |
| **Mtazamo juu ya mahitaji ya ziada ya kujifunza (kama vile mahitaji maalum ya kujifunza na/au ulemavu)** | **Mtazamo wa kikabila** | **Mtazamo wa kijinsia** |
| **Afya** | **Lugha** | **Uhamiaji** |
| **Umasikini** | **Mtazamo wa kidini** | **Mtazamo wa kiutamaduni** |
| **Majanga** | Kadi tupu kwa ajili ya walimu kuandika mawazo yao juu ya vikwazo | |

# Kielelezo nambari 3.6: Visa Mafunzo vya Watoto walio nje ya skuli

1. **Amina** anatumia kiti cha magurudumu. Anataka kuhudhuria skuli yake ya karibu na marafiki kutoka nyumbani. Skuli haina miundombinu ya kutumia kiti cha magurudumu, kwa hivyo binamu yake ambaye hakuwa na kazi alifuatana naye kwenda skuli kumsaidia kupanda ngazi na kumsogeza kupita milangoni. Binamu yake sasa ana kazi na hawezi kufuatana naye tena. Skuli inasema Amina hawezi kwenda skuli bila msaidizi. Amina amekuwa nyumbani tangu wakati huo.

2. **Ali** ana matatizo ya kitabia na kihisia. Alipokwenda skuli, aliweza kukaa tu darasani kwa dakika 15 na kwa kawaida alikuwa na shida mwishoni mwa kipindi. Hii ilimsababisha afanye vurugu kubwa, ambazo zilisababisha aingie katika shida zaidi na mara nyingi walimu wake waliishia kumtenga darasani. Hatimaye Ali aliacha kuja skuli. Sasa haendi skuli tena, lakini hutumia siku zake nyumbani ambapo amekuwa akitumia muda wake akiwa na watoto wakiume wakubwa na kupata shida na wafanyabiashara na polisi

3. **Issa** ana ulemavu wa uoni na shida nyengine za kujifunza. Wazazi wake huhisi wanajisikia aibu kwa ulemavu wake. Wanaishi umbali mrefu kutoka skuli kwa hivyo huisaidia familia kwa biashara ya kuuza mboga kwenye soko la karibu na hajawahi kwenda skuli.

4. **Ahmed** ana umri wa miaka 11 katika skuli ya msingi. Ana matatizo katika somo la hesabati; hana ufahamu katika kufanya kazi na marakwamara anapata jawabu zisizosahihi. Mwalimu humpiga anapofanya makosa na kwa hivyo Ahmed hukosa masomo ya hesabati.

5. Hussein ana umri wa miaka 10. Alikuwa na furaha ya kuanza skuli miaka michache iliyopita, lakini furaha yake ilikuwa ni ya muda mfupi. Mwalimu wake hakuwa na huruma ya kufanya kazi pamoja naye. Hussein hakubadilika na mwalimu wake anadhani kwamba alikuwa na tabia mbaya, mvurugaji na mharibifu. Kila siku alikuwa na migogoro na wazazi wake. Wazazi wake walijaribu kutafuta suluhisho pasina kufanikiwa. Walihisi kutokuwa na nguvu zaidi, wakafadhaika na kukasirika na baadhi ya wakati humkasirikia, humtukana, humuadhibu na kuacha kusema naye. Rafiki zake katika kiwanja cha michezo na majirani humfanyia dhihaka na kutocheza naye; husema anaharibu michezo yao. Mtu anaweza kujiuliza swali "lakini kwa nini?" baadaye Hussein haendi tena skuli.

6. Alipokuwa ana miaka 13 **Halima** alikuwa yatima alikwenda kukaa na bibi yake. Alisita kuhudhuria skuli katika kipindi cha mtihani wa darasa la 7. Wakati uongozi wa skuli ulipoitembelea familia yake, baada ya kuandika karatasi zake mbili za kwanza, aligoma kurudi skuli na bibi yake hakusema chochote kumsaidia kubadili maamuzi yake. Baadae, alipozungumza na marafiki, alisema kwamba skuli haina manufaa na amechagua kuolewa.

7. **Subira** ana umri wa miaka 10. Familia yake ni masikini sana. Mama yake hutembea kilomita 6 kila siku kukusanya mabaki ya chakula kilichoachwa katika mkahawa na kantini ya watalii ili kuongeza chakula cha familia. Baadhi ya wakati Halima hutumwa kwenda kuuza karanga katika kituo cha basi kilichokaribu. Baba yake alimsitisha kwenda skuli ili aisadie familia nyumbani. Subira alipomuuliza kuhusu skuli alijibiwa "Lazima ufanye kazi kwa ajili ya chakula unachokula".

## Kielelezo nambari 3.7: Mifano ya Karatasi za Uchunguzi

| Vitu ninavyovitazama | Vitu ninavyoviona au kuvisikia | Nahisi | Hatua inayowezekana |
|---|---|---|---|
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |

# Kielelezo nambari 3.8: Miongozo ya usaili

Ifuatayo ni miongozo ya kukusaidia kufanya usaili mzuri

## Maandalizi

- Hakikisha usaili wako una malengo mahususi
- Tengeneza orodha fupi ya mada na maswali 5 ili yakuongoze katika usaili wako

## Utangulizi

- Jitambulishe kwanza mwanzoni mwa usaili wako
- Eleza wazi wazi malengo ya usaili wako
- Waulize washiriki kama wana muda wa kutosha wa kuwafanyia usaili kwa wakati huo, kama hapana, waambie wapendekeze muda unaofaa.
- Waulize washiriki kama wanataka usaili uwe wa siri.

## Kufanya usaili

- Anza na mazungumzo ya kirafiki ya ujumla yanayoweza kuwafanya washiriki waweze kujiskia vizuri.
- Lifanye swali la kwanza liwe rahisi kwa mshiriki kulijibu. Kuanza usaili kwa maswali binafsi na magumu inaweza kuleta shida na kusitisha mtiririko wa Habari.
- Jaribu kuelezea wazo moja kwa swali moja ili kuepuka mkanganyiko.
- Epuka kuwepo kwa maswali mengi ya ndio na hapana au maswali yaliyofungwa kwa sababu yanaweza kuharibu mtirirko wa habari.
- Kuwa makini katika kuangalia ni mara ngapi unatumia kuuliza “kwa nini”. Japo kuwa “kwa nini” ni swali muhimu, kuuliza hivi mara nyingi au kulazimisha mtu kutoa jawabu kunaweza kumfanya mshiriki asiwe na amani.
- Kuwa makini kwenye kuuliza ‘maswali yanayoongoza – haya ni maswali yanayojaribu kushawishi majibu ya mhojiwa. Mfano wa ‘swali linaloongoza ‘ni’ Je, hufikirii kwamba …?’
- Muulize mshiriki kurudia jibu ikiwa hajalifahamu au hakuweza kurekodi walichosema. Pia, watake waeleze au wafafanue majibu yao ikiwa hakufahamu kabisa.

- Epuka kutoa hukumu, kutoa ushauri, au kufikisha maoni yako mwenyewe □ Mwambie mhojiwa wakati unabadilisha mada, ili aweze kujiandaa**.**
- Jihadhari na lugha yako ya mwili, kwa sababu hii inaweza kuwaambia wahojiwa nini unahisi kuhusu majibu yao na inaweza kusumbua usaili. Inaweza pia kumfanya yule aliyehojiwa  kuwa nawasiwasi au kama wewe hupendezewi sana na kile wanachosema ikiwa, kwa mfano, unaonekana kuchoka, au, kuhangaika au epuka kutazamana

## Kufunga usaili

- Fanya usaili wako kuwa mfupi (chini ya saa moja ikiwezekana).
- Jaribu kufanya muhtasari wa mambo ambayo umejifunza wakati wa usaili ili kuoana na mhojiwa ikiwa umeakisi usahihi wa kile kilichosemwa.
- Waulize wanaohojiwa kama wana maswali yoyote wanayotaka kukuuliza.
- Washukuru wahojiwa wako kwa muda wao na usumbufu wowote uliojitokeza.

## Miongozo ya kuhifadhi usaili

- Tumia daftari
- Andika kwa kina kila kilichozungumzwa
- Rekodi kwa kina lugha ya mwili na hisia zilizojitokeza wakati wa usaili.
- Andika uchunguzi wako kuhusiana na jinsi usaili ulivyokwenda.
- Kama ilikua usaili wa kikundi, nani alisema nini na je wengine waliwafiki?
- Andika maelezo yoyote ya ufuatiliaji mara tu baada ya mahojiano
- Andika hisia zako binafsi.

Imetolewa kutoka: S.B. Rifkin and P. Pridmore, (2001) 'Partners in Planning – Information; participation and empowerment', Macmillan Education.

# Kielelezo nambari 3.9: Matokeo ya Utafiti – Sampuli A

Ugunduzi mmoja ulibaini kwamba mara nyingi kuna kushuka kwa maendeleo ya kitaaluma wakati wa wiki za mwanzo za mwanafunzi katika skuli mpya.

Ingawa utafiti unamaanisha kwamba, matatizo/makosa ambayo wanafunzi wanajirekebisha ili kuendana na tamaduni na taratibu tafauti za skuli inaweza kutokea kwa muda mfupi. Mambo mengine yanaweza kupelekea maendeleo duni ya kitaaluma, kama vile kukosa mapumziko marefu, kukosa malengo baada ya kufanya mitihani au kufanya kazi kwa kukariri mambo waliyokuwa wakiyafanya kabla katika skuli zao za mwanzo au makundi ya kujifunza.

Ijapokuwa, baadhi ya wanafunzi wanakabiliana na matatizo makubwa kuliko wengine. Kwa mfano:

- Baadhi ya wanafunzi wenye hali ngumu wanaweza kuhitaji msaada wa ziada ili kukabiliana na vizuizi zaidi na changamoto za kijamii.
- Baadhi ya wanafunzi ni wahanga wa kuonewa na kudhulumiwa.
- Mahitaji ya ziada ya wanafunzi yanahitaji yapangiliwe kwa uangalifu; bila ya mpangilio huu, wanaweza wakakosa msaada na kufahamu wanachokihitaji.
- Baadhi ya matatizo au makosa yanayorekebishwa yanahitaji kufahamika kwa kina. Kwa mfano, hata kama wasichana wanafanikiwa kitaaluma, pamoja na kuwaliganisha na wavulana, baadhi ya wasichana katika mwaka wao wa pili katika skuli ya sekondari wataonesha uwezo mdogo wa kufanikiwa na kuwa na maisha mazuri.
- Wanafunzi wanaofika skuli ndani ya mwaka au muhula wa masomo (mfano; wanafunzi ambao hawakuwahi kupelekwa skuli, wanafunzi ambao wamekwenda nyumbani, wote waliotolewa kutoka skuli nyengine, wakimbizi) mara nyingi wanapata msaada usiojitosheleza wanapoingia skuli.

# Kielelezo nambari 3.10: Matokeo ya Utafiti – Sampuli B

Mpito wa elimu unaweza ukamkumba mwanafunzi pamoja na kuwepo tamaduni tafauti na unaleta madhara ‘mtikisiko wa utamaduni’. Jambo hili linatokea katika awamu tafauti kwa miezi michache ya mwanzo.

- Kipindi cha furaha, mfano, mwanafunzi anaweza kufuata tamaduni mpya za skuli kwa hamu na matarajio makubwa.
- Kipindi cha kupatana, mfano, kujilazimisha kukabiliana na mazingira yao mapya baada ya kuona matumaini na matarajio yao hayafikiwi, kwa hivyo wanajihisi kukata tamaa na inawezekana kukasirishwa au kuchanganyikiwa.
- Hatua ya kupatana. Mfano, wanalazimika kupambana na hali zao, wanajifunza mambo ya kutarajia, kuweka utaratibu wakudhibiti udhaifu na maharibiko wanayoyahisi, na kuthamini mazingira yao mapya.
- Hatua ya marekebisho. Mfano wanakuwa ni sehemu ya jamii mpya ya skuli yao kwa ukamilifu, inawatambulisha na kujifunza kutatua matatizo yao kupitia mitazamo inayotokana na tamaduni za skuli.

Ni kawaida kupata mshituko wa tamaduni, kuwepo hali ya mashaka na migogoro. Ijapokuwa, wanafunzi wanaweza kuona mpito wa elimu una changamoto kubwa, wakiwemo vijana baleghe, wanafunzi ambao wanapata tabu sana kuelewa utamaduni wa skuli ile, wanaweza kujihisi wamepoteza hadhi katika skuli yao mpya, inawezekana wamejisikia vibaya kutokana na dhana potofu inayowafanya kujitenga katika kujielewa katika skuli. Walimu wanaweza kuchangia dhana hii potofu kwa kutofahamu skuli zao za awali na maendeleo yao.

Kama mwanafunzi atashindwa, anaweza akakata tamaa haraka, ikapelekea kujitenga na kukata tamaa hasa pale anapokosa kujenga urafiki, majukumu na kukubalika katika jamii mpya. Utafauti wa jamii kwa wazazi na walezi unapelekea ugumu wa mashirikiano katika maisha ya skuli.

# Kielelezo nambari 3.11: Matokeo ya Utafiti – Sampuli c

Wanafunzi wenye mahitaji ya ziada, kama vile mahitaji maalumu ya kielimu na/au ulemavu wanaweza wakauona mpito wa elimu ndilo jambo lenye changamoto.

- Wakati mwengine mwalimu wa mwanafunzi hafahamu mipango iliyopo skuli ya kumsaidia mwanafunzi katika skuli yake ya zamani
- Idadi kubwa ya wanafunzi wanakutwa na mateso katika mihula yao ya mwanzo.  Wengine wanaona kwamba hawana msaada tena utakaowafanya wafanikiwe.
- Baadhi ya wanafunzi wenye mahitaji ya ziada wana shida ya kuzifahamu njia zinazopitika wanapokwenda skuli.
- Baadhi ya wanafunzi hasa iwapo matokeo mabaya yanahusishwa na baadhi ya mahitaji yao ya ziada, wana muelekeo wa kutengwa kwa misingi ya tabia mbaya.

# Kielelezo nambari 3.12: Matokeo ya Utafiti – Sampuli D

Wakati wanafunzi waliposailiwa kabla ya kuelekea katika mpito wa kutoka skuli za msingi kwenda skuli za sekondari, walielekea kukubaliana na uoni kwamba ikiwa kiwango cha mwendelezo ni muhimu, ndio hivyo hivyo kiwango cha kumaliza.

- Walipata hofu ya kukabiliana na kazi, hata hivyo walifurahishwa kupata masomo mengi ya kusoma, hasa masomo ya vitendo kama vile sayansi, sanaa, kuchora na teknolojia.
- Walijutia kumkosa mwalimu wao wa skuli ya msingi lakini walitegemea kufundishwa na wataalamu mbalimbali wa masomo.
- Walihofu kuwakosa marafiki zao wa zamani wa skuli ya msingi lakini walivutiwa kuhusiana na kutengeneza mahusiano mapya.

Hili hasa linaweza kuwa linafaa kwa vile mpito wa elimu unatokea kwenye wakati muhimu wa maendeleo ya ujana. Wakati, wanafunzi katika hatua ya maendeleo wanaweza kuwa wahanga wa baadhi ya msongo wa mawazo, wanaweza pia kutamani mabadiliko, uhuru mpana na uzoefu mpya.

Wanafunzi walielekea kuonesha ustawi chanya kupitia kipindi cha mpito skuli ambapo mkazo uliwekwa katika uhuru mkubwa wa wanafunzi, mazingira yasiyodhibitiwa sana, na pale fursa zaidi za kuthubutu zilipotolewa wakati wa masomo kinyume na skuli zilizowafanya wanafunzi wajihisi wako salama na wanajaliwa kupitia kanuni kali zilizowekwa kwa kurekebisha tabia. Mfano, kutembea vizuri katika koridoo, kuwatumia wanafunzi wakubwa kama ni wasimamizi katika viwanja vya michezo na kuwapatia zawadi ili kuongeza bidii.

Hii inaonesha kuwa ipo haja ya skuli kurekebisha mchakato wa kuandaa kanuni na kutathmini maendeleo ili ziongeze ushiriki wa wanafunzi na hitajio la kiwango bora cha umiliki. Mfano, michakato iliyohusu kuunga mkono mpito wa elimu inahitaji ionekane kama ni ya kimaelekezo kuliko kudhibiti.

# Kielelezo nambari 3.13: Filamu ya ‘Kufika Skuli’ ya EENET, Mpango wa 3 na Maelezo yake

Nenda moja kwa moja mpaka kwenye video kwenye YouTube. Fanya hivyo kwa dakika 4 na sekunde 40

www.youtube.com/watch?v=d3Lon8YdsL0

Au tembelea EENET’s website kutafuta video nyengine zaidi na uweze kuona na upakue viunganishi:

www.eenet.org.uk/the-10-videos-and-manuals/

## ‘Kufika skuli’ nakala ya filamu

Jaalia siku zote kuna pahala fulani unakwenda, ukifika huko hukaribishwi wala hujisikii vizuri

Kwa bahati mbaya, jambo hili linatokea kwa watoto wengi kila siku.

Skuli inaweza kuwa ni sehemu ya shida kwa watoto wengi, hasa ikiwa ni kubwa, yenye kelele, au ni skuli yenye msongamano.

Kufika skuli na mawazo mabaya inaweza ikaathiri hali ya mtoto siku nzima na hata ikamvunja moyo wa kurudi tena skuli.

Watoto mara nyingi wanasubiri kwenye viwanja vya michezo kabla ya kwenda darasani. Hii ni sehemu inayoweza kuwa na harakati nyingi na kelele.

Kwa wanafunzi wengi, hili linawafurahisha, fursa kubwa ya kukutana na marafiki na kucheza kabla masomo kuanza.

Lakini kwa wengine, inaweza kuwadhalilisha na kuwahofisha.

Mwanzo wa siku inaweza kuwachanganya baadhi ya wanafunzi, kama vile wanafunzi wadogo sana kiumri, ambao wamejiunga karibuni skuli, wenye shida ya kuona au kusikia, au wenye shida ya kujifunza.

Wanaweza kuhangaika kufanyakazi au kukumbuka pale wanapopaswa kwenda na kwa wakati gani

**Utafanya nini?**

Unaweza kusaidia kuzifanya dakika chache za mwanzo za skuli kuwa zenye uzoefu chanya kila siku

Mwalimu mwenye urafiki na tabasamu ambaye anamkaribisha vizuri kila mmoja asubuhi anaweza kuleta mabadiliko makubwa.

Watoto wanaweza pia kushajihishwa kukaribishana vizuri wao kwa wao.

Watu wote wanamjua Ana na humwambia ‘habari yako Ana’. Wanasema, ‘mpe Ana tano’ ‘mpe tano’, na Ana anafurahi kwa hilo. Anaona mkabala ni chanya mno. Hakuna mkabala hasi. Tangu siku ya kwanza, Ana alikuwa na furaha kwenda skuli. Kwa nini? Kwa sababu mazingira ni rafiki sana’.

Unaweza ukawashajihisha watoto kukaa wawili wawili ili wasaidiane kutembea mazingira ya skuli. Jambo hili baadhi ya wakati linajulikana kama ni la kusaidiana.

“Jambo zuri katika madarasa yetu ya mjumuisho ni mkabala wa watoto kuhusu Varia. Inapendeza kuona vipi wanamkaribisha na vipi wanacheza naye katika duara. Hazungumzi lakini wanamfahamu na wanamkubali. Varia ameonesha utu wake. Anaweza kuwasiliana na wenzake na hali hii ikawa na faidakubwa kwake. Maendeleo ya Elimu Mjumuisho yanaifanya jamii iwe ni yenye huruma zaidi na yenye ubora kwa kiasi fulani.”

Unaweza ukaweka alama ............ au ukatumia rangi tafauti kwenye kuta, sakafu na milango kuwasaidia watoto kukumbuka wapi pa kwenda.

Unaweza kutumia mwenendo mzuri wa asubuhi. Hali hii inawasaidia watoto kujifunza, ni wakati gani, wapi, na vipi watembee kutoka viwanja vya michezo kwenda madarasani.

Unaweza ukatengeneza maeneo tulivu katika skuli, kwa ajili ya watoto wanaopata shida kukaa katika viwanja vya michezo vyenye kelele kubwa.

# Kielelezo nambari 3.14: Khadija mwenye Miaka 7

Khadija alifika hapa miezi sita iliyopita. Alikuja na mama yake na ndugu zake wawili wakubwa, wanaishi na familia ya watu wengine ambao wanafanya kazi ya kilimo maeneo ya karibu. Khadija ameandikishwa darasa la kwanza. Ni mdogo na asiye na afya nzuri na anaonekana ana umri mdogo.

Tokea Khadija aanze skuli anaonekana bado hajazoea, au kuwa na urafiki na watoto wengine. Anatabia kama mtoto mdogo sana, na anapata shida ya kuzingatia, mara kwa mara analala kwenye sakafu. Mwalimu amejaribu kuwasiliana na Khadija lakini hili halikufanikiwa. Watoto wengine wanasema kuwa Khadija hafahamu wanasema nini. Mwalimu amegundua kwamba Khadija anaonekana kufurahia kucheza katika mchanga na maji. Sasa mama yake Khadija ameanza kuhudhuria msikitini.

**Jadilli:**

- Una mawazo gani?
- Niyepi mahitaji ya Khadija na utatumia mikakati gani kumsaidia Khadija katika mahitaji haya?
- Ni vipi wewe na wahudumu au wataalamu wengine mtamsaidia Khadija katika mafanikio yake ya mpito?

Kielelezo nambari 3.15: Afifa mwenye umri wa miaka 7

Mama Afifa anasema kuwa Afifa ni mtoto ambaye ana matatizo kila wakati analia na anashida kutulia. “Ni mtoto wangu wa mwanzo na nilikuwa sijui kama ninavofanya sio sahihi. Baada ya miezi kumi na nane nilihisi nafanya kitu

sio sahihi lakini nilikuwa sijui kwanini, alikuwa na maneno machache ambayo ni sahihi na alikuwa haonekani kama anacheza vizuri, alikuwa anavunja vitu na wala alikuwa hashirikiani na wenzake".

"Nilifikiria kwamba anafanya vibaya, wakati huo Afifa alikuwa na miaka mitatu". Mama yake aliona hana ushirikiano na wenzake aliona mtoto wake anachanganya maneno na alikuwa hafahamu baadhi ya mambo, lakini alikuwa hajui afanye nini.

Afifa alipoanza skuli ya maandalizi, mama yake alibaini kwamba muingiliano wake na watoto wengine ulikuwa si mzuri lakini wafanyakazi wa skuli walisisitiza kuwa kila kitu kilikuwa sawa, na kwamba Afifa angekua kwa kiwango chake mwenyewe.

Afifa alipoanza skuli ya msingi mwalimu wake hakufurahishwa na tabia zake kutokana na malezi mabaya ya mama yake. Hivyo kauli ya mwalimu ilimkasirisha mama ake Afifa   Miezi mitano baadae mama ake Afifa alimtoa mtoto wake skuli.

**Jadilli:**

- Nini maoni yako?
- Nini mahitaji ya Afifa na ungetumia mikakati gani kusaidia mahitaji haya?
- Wewe, wahudumu, na wataalamu wengine, mtamsaidiaje Afifa katika mafanikio yake ya mpito?

# Kielelezo nambari 3.16: Rashid mwenye miaka 10

Rashid aliwasili mwezi mmoja uliopita katika skuli ya msingi katika Jiji la Zanzibar. Ana miaka kumi, alifikiria Jiji la Zanzibar ni nchi iliyojitenga. Alipowasili alifikiria kuwa anaweza kufika kijijini kwake wakati wowote anaoutaka.

Rashid alikuwa anaishi kijijini na bibi yake tokea ana umri wa miaka sita, sasa amekuja katika Jiji la Zanzibar kuishi pamoja na mama yake na baba yake mwengine wa kambo ambaye hajawahi kumuona kabla. Rashid husema aliomba dua, 'Tafadhali niruhusu niende Jiji la Zanzibar nikawe pamoja na mama yangu'

Alipofika skuli Rashid alionekana kuwa na hamu ya masomo lakini alionekana kukasirika kirahisi. Wakati anapopewa kazi kufanya katika meza yake akianza kuandika, mara huondoka na kwenda kuchonga penseli yake na kwenda kuzungumza na jirani zake na kutoa vitu vyake ndani ya mkoba na kuanza kuvichezea na mara anaendelea kutafuta vitu mkobani mwake asivyovielewa, wakati mwalimu anapomzuia kuangalia hutizama juu na hapohapo husahau alikuwa akitafuta nini. Huanza kufanya kazi zake lakini hamalizi, na anapojuulishwa baba yake wa kambo aliwataka skuli wampe taarifa wanapompa kazi za nyumbani na atahakikisha Rashid amefanya hiyo kazi.

Rashid anapenda michezo, kupitia hiyo michezo anapata fursa ya kubishana na wanafunzi wenzake.

**Jadilli:**

- Nini maoni yako?
- Ni yepi mahitaji ya Rashid na utatumia mikakati gani kumsaidia katika mahitaji haya?
- Wewe, wahudumu na wataalamu wengine mtamsaidiaje Rashid katika mafanikio yake ya mpito?

# Kielelezo nambari 3.17: Suleiman mwenye umri wa miaka 11

Suleiman ni mtoto mwenye uwezo, anajitegemea na mwenye shauku ya kusoma. Wazazi wake wanataka afanikiwe katika masomo, hakuwahi kuacha kuhudhuria skuli.

Karibuni mwalimu wa Suleiman aligundua kuwa Suleiman hafanyi vizuri katika kazi zake, alionekana amechanganyikiwa na mwenye khofu na pia hayupo makini.

Mwalimu wake alipanga kuonana naye wakati wa chakula cha mchana na amuulize tatizo lake, alisema kwamba familia yake imetakiwa kuhama, na eneo lao linataka kufanywa eneo la mashamba ya kibiashara, na familia yake wameambiwa watahamishiwa eneo la mbali ambapo udongo wake hauna rutuba na pia kuna huduma chache za kijamii na skuli ipo mbali. Alisema ana hofu kubwa kwamba mama, baba pamoja na familia yake ni vipi wataweza kumudu. Na hajui kama ataweza kuhudhuria skuli kikawaida kwa sababu itambidi atembee masafa marefu.

**Jadilli:**

- Una maoni gani?
- Ni yepi mahitaji ya Suleiman na utatumia mikakati gani kumsaidia katika mahitaji haya?
- Wewe na wahudumu na wataalamu wengine mtamsaidiaje Suleiman katika mafanikio yake ya mpito?

# Kielelezo nambari 3.18: Juma mwenye umri wa miaka 14

Akiwa katika skuli ya msingi, Juma alisitasita kuhudhuria skuli. Alipohudhuria, mara nyingi aligombana na mwalimu. Mara kadhaa alikaribia kutengwa kwa tabia yake na alipata usaidizi kutoka kwa mwalimu wa ushauri nasaha. Aligundua kuwa, Juma alikuwa na wasiwasi sana kuhusu mama yake (mwemye mahitaji muhimu ya kiafya), na hii inaeleza wazi kwa nini Juma anaogopa skuli. Huruma za mwalimu wa ushauri nasaha zilijumuisha ziara ya nyumbani ili kumsaidia mama yake kujifunza kumsaidia Juma kwa ufanisi zaidi.

Familia ya Juma sasa imehama, na anasoma skuli mpya ya sekondari. Alipokuwa akijiandaa kwa ajili ya uhamisho wake, mwalimu wa ushauri nasaha alizungumzia wasiwasi wa Juma kuhusu mama yake na skuli yake mpya. Ilikubaliwa kuwa, Juma anaweza kuomba kwenda ofisi ya skuli wakati wowote ikiwa atahisi wasiwasi juu ya mama yake. Hatolazimika kujifanya anaumwa na tumbo au kufanya matatizo ili aruhusiwe kurudi nyumbani na kuangalia hali ya mama yake. Juma ana aibu sana kukubali msaada darasani hata katika masomo yenye udhaifu kwake, lakini alikubali kukutana na mwalimu wa ushauri nasaha au msaidizi mara moja kwa wiki.

Kisha bila ya kutarajia, tatizo la kuhudhuria likatokea. Mama yake Juma alimwambia mwalimu wa mwongozo na ushauri kwamba, hatokwenda skuli tena. Kundi la wavulana wakubwa walimfuata baada ya muda wa skuli, na aliamini kwamba wanataka kumshambulia.

**Jadilli:**

- Una maoni gani?
- Ni yepi mahitaji ya Juma na utatumia mikakati gani kumsaidia katika mahitaji haya?
- Wewe na wahudumu na wataalamu wengine, mtamsaidiaje Juma katika mafanikio yake ya mpito?

# Kielelezo nambari 3.19: Shamila mwenye umri wa miaka 15

Shamila anatarajia kwenda skuli ya sekondari. Ni mwanafunzi mwenye mtindio wa ubongo. Inabidi atumie kiti cha magurudumu na hawezi kuzungumza kwa ufasaha. Wazazi wa Shamila, wanafunzi wenzake na walimu wote wanaweza kuwasiliana nae na kumuelewa.

Shamila ana uwezo wa kiakili na ana malengo. Katika skuli yake ya sasa, marekebisho yamefanywa kwa ajili yake ili kupata masomo mengi.

Baada ya kuwasiliana na skuli ya sekondari kujadili mahitaji ya Shamila, mwalimu wa udahili wa skuli anamuhoji Shamila na kudhani kuwa nae ana matatizo ya kujifunza. Anakataa kumkubali kwani anafikiri hataweza kumudu masomo. Pia anasema kwamba, ingawa vifaa vingi vya skuli vinaweza kufikiwa na viti vya magurudumu, hataweza kupata baadhi ya masomo ya msingi kwani madarasa haya hawezi kuyafikia.

**Jadilli:**

- Una maoni gani?
- Ni yepi mahitaji ya Shamila na utatumia mikakati gani kumsaidia katika mahitaji haya?
- Wewe na mhudumu na wataalamu wengine, mtamsaidiaje Shamila katika mafanikio yake ya mpito?

Tanbihi:
Wanafunzi wote wanastahili na wana haki ya mpito mwepesi.

## Kielelezo nambari 3.20: Kanuni muhimu za mabadiliko

- Wanafunzi wote wanastahili na wana haki ya ‘mpito’ mwepesi.
- Mahusiano mazuri ni muhimu: mageuzi ya ufanisi yanategemea juu ya kuaminiana na kuheshimiana kati ya mwanafunzi, wazazi au walezi na wataalamu wote wanaohusika.
- Kila mwanafunzi ana mahitaji binafsi: usaidizi wa mpito unapaswa kunyumbulika na kulengwa kulingana na mahitaji ya mwanafunzi.
- Usaidizi ulioratibiwa na mawasiliano mazuri kati ya mwalimu na mawakala *mashirika* ni muhimu.
- Mazingira ya skuli yanasaidia mawasiliano ya wazi, ya kuaminiana na ya uaminifu na yanahimiza ushirikiano.
- Muda na rasilimali za kutosha zimetengwa ili kuhakikisha udahili, tathmini ya awali na msaada wa mafunzo ni wenye ufanisi.
- Wanafunzi husikilizwa hata wakiwa wadogo ili mahitaji yao yaeleweke na maoni yao yazingatiwe.
- Familia zinahusika katika kupanga: wazazi au walezi ni chanzo muhimu cha taarifa na usaidizi katika skuli.

## Kielelezo nambari 3.21: Kadi za Changamoto

Nakili na kata seti ya kadi hizi kwa kila kikundi kidogo. Tafadhali kumbuka kwenye kadi isiyo na maandishi, walimu wanaweza kuandika changamoto za ziada wanazozitambua wakati wa majadiliano.

| | |
|---|---|
| Siwezi kupata njia yangu au kupata njia zinazoweza kufikiwa katika skuli yangu mpya. | Kama msichana, sasa mimi ni mkubwa. Lazima nifanye kazi nyingi nyumbani. Hili linanifanya nichelewe skuli na ninaingia matatizoni. |
| Nimechanganyikiwa na ratiba mpya. Ninapaswa kwenda wapi na lini? Nimegombwa kwa kuchelewa. | Skuli yangu mpya iko sehemu tafauti ya mji na lazima niende skuli mwenyewe, lakini sio salama. |
| Wazazi wangu hawafahamu kwamba lazima nifanye kazi za nyumbani ninaporudi nyumbani. Siku zote wanatarajia nimtunze ndugu yangu na kufanya kazi nyengine za nyumbani. | Walimu katika skuli yangu ya zamani walipanga jinsi ya kunisaidia katika masomo. Skuli yangu mpya haijuwi kuhusu hili. Mipango yote ya usaidizi lazima ianzishwe tena.<br>Natamani mwalimu wangu wa zamani angehusika. |
| Wazazi wangu hawajishughulishi sana na skuli, sasa niko katika darasa la juu lakini bado nawahitajia wazungumze na walimu wangu ninapopata matatizo. | Walimu wa skuli hii wanafanya mambo tafauti. Wana njia tafauti za kufundishia. Siwezi kuzoea matarajio yao. |

| | |
|---|---|
| Siku ya kwanza nilichekwa kwa sababu sikuwa na viatu. | Sijazoea kuwa mbali na wazazi wangu siku nzima. |
| Masomo yanachosha. Ninajifunza mambo yaleyale niliyojifunza katika skuli ya awali. | Ninaonewa na ninaogopa sana hasa nyakati za mapumziko na chakula cha mchana. |
| Nataka kwenda chuo cha ufundi. Sijui ni vyuo gani vinavyojumuisha wanafunzi wenye mahitaji ya ziada.<br>Pia katika skuli yetu hakuna mtu anayejua. | Sikuwahi kuona ndani ya skuli yangu mpya hadi siku ya kwanza ya muhula. Niliogopa. |
| Ninaingia matatizoni kwa kuwa jeuri kwa mwalimu wangu mpya kwa jinsi ninavyomuuliza wakati sielewi anataka nifanye nini. | Nina wasiwasi sitaweza kupata marafiki wapya au kushiriki kikamilifu katika matukio ya skuli. |
| Sijisikii kuwa sehemu ya skuli hii. | Sehemu isiyo na maandishi kwa ajili ya washiriki kuandika changamoto za ziada. |
| | |

## Kielelezo nambari 3.22: Kadi za mikakati

Nakili na ukate seti ya kadi hizi kwa kila kikundi kidogo. Tafadhali kumbuka, zinapaswa kuwa za rangi tafauti na **Kielelezo nambari 3.22**. Kwenye kadi isiyo na maandishi, washiriki wanaweza kuandika mikakati yoyote ya ziada wakati wa majadiliano ikiwa ipo.

| | |
|---|---|
| Watayarishie ziara wanafunzi wapya, ramani na panga usaidizi rika (mfano, rafiki wa darasa) ili kumsaidia kutafuta njia. | Wasiliana na wazazi au walezi mapema unapotayarisha mipango ya maendeleo ya mtu binafsi na ile ya mpito, wape wazazi au walezi vipeperushi kuhusu nini cha kutarajia na shughuli gani wao na skuli wanaweza kufanya ili kurahisisha mabadiliko. |
| Hakikisha kuwepo kwa usaidizi rika kwa wanafunzi wote wapya wanaowasili kwa wiki kadhaa, na wanafunzi wote wanajua kwamba wanatarajiwa kusaidiana na kupewa zawadi kwa kusaidiana. | Wawezeshe walimu kuwatembelea baadhi ya wanafunzi majumbani kwao ili kugundua mahitaji yao na mifumo ya usaidizi ya familiya na jamii. |

| | |
|---|---|
| Wakaribishe kwa moyo mkunjufu wazazi au walezi wote na andaa mkutano wa udahili ambapo taarifa zinaweza kupelekwa kabla ya kuwasili kwa mtoto wao darasani. Waalike tena wazazi au walezi wa wanafunzi wapya baada ya wiki kadhaa ili 'kusherehekea' maendeleo ya awali na kufafanua matarajio ya skuli. | Watunze kwa haraka wanaowasili kwa kujaribu kwa bidii au kwa jambo lolote wanalofanya vyema na kwa utulivu.<br><br>Dumisha usaidizi wa mpito mwaka mzima kwa wanafunzi wanaohitaji. |
| Wakaribishe wazazi au walezi darasani (hasa darasa la maandalizi na mapokezi) ili kuwasaidia watoto wao kutulia. | Washirikishe wazazi au walezi wakati wa kuandaa mipango ya shughuli na mpito. |
| Kuwa na mfanyakazi anayeratibu mabadiliko ya daraja au skuli. | Wasiliana ili kusaidia wanafunzi kabla, wakati na baada ya mpito. |
| Rekebisha mtaala na mbinu za kufundishia ili kuelewa uwezo wa awali wa kujifunza wa wanafunzi wapya katika skuli zao walizotoka. | Andaa utaratibu wa kubadilishana kwa walimu kati ya skuli kwa mfano, mwalimu wa skuli mpya ambaye ndiye msimamizi wa mwaka wa mpito pamoja na MEM wa skuli, wanaweza kutembelea darasa la wahitimu ambao wanakaribia kuondoka ili kujua wanafunzi na kujibu maswali yao. |

| | |
|---|---|
| Hakikisha mipango ya mtu binafsi inarikodiwa na kuchangiwa na mwalimu au skuli mpya ya mwanafunzi. | Andaa tathmini ya awali ya ufanisi na kuweka malengo ya muda mfupi ya kubakia katika jamii na taaluma kwa kila mwanafunzi mpya aliyewasili na kukagua maendeleo baada ya wiki chache. |
| Hakikisha skuli za sekondari zinapatiwa habari kuhusu chaguzi zinazoweza kufikiwa/ujumuishi za elimu ya juu na ya ufundi. | Hakikisha skuli za sekondari, vyuo vya juu na taasisi za ufundi zinatoa mwongozo wa taaluma inayotoa motisha na ushauri unaofaa kwa wanafunzi wenye mahitaji ya ziada. |
| Msaidie mwanafunzi asipoelewa; tarajia baadhi ya waliowasili wapya kuwa wazungumzaji au wenye kelele, ikiwa wana wasiwasi au furaha katika mazingira yao mapya. | Hakikisha wanafunzi wote wapya wanashirikishwa katika shughuli za ubunifu na burudani ndani na nje ya saa za mtaala na ili waweze kujiunga na jamii mpya kwa haraka, wahisi shauku na wapewe hisia ya kusudio na ufaulu. |
| Wasaidie wanafunzi kutembelea darasa jengine au skuli ili waweze kufahamu mazingira, watu na taratibu kabla ya kuhama. | Hakikisha walimu wanafahamu kikamilifu ujifunzaji wa awali wa kila mwanafunzi, ukisaidiwa na tathmini ya kina ya awali ya wanaowasili wapya. |
| Wafanyakazi wasaidizi wanahitaji kuhakikisha kuwa, hawafanyi mwanafunzi wao ajisikie kutengwa au tafauti na wengine darasani. | Panga shughuli za kujenga urafiki katika wiki chache za mwanzo za masomo. |

| | |
|---|---|
| Andaa siku za utangulizi ndani ya muhula kabla uhamisho. | Wasaidie wanafunzi wapya wanaowasili kusimamia masomo |
| Katika siku hizi, wanaowasili wanaweza kukutana na walimu watakaokuwa nao mwaka ujao na kupata uzoefu kwa baadhi ya masomo, kupata fursa ya kukutana na wanafunzi wenzao wa baadaye kutoka skuli nyengine na kuwauliza maswali wanafunzi waliohama katika skuli yao mwaka ulipita. | yao wenyewe na kwa pamoja waweze kuakisi uzoefu wao katika mabadiliko. Baadhi ya skuli zimefanya mijadala yenye mafanikio makubwa kuhusu jinsi wanafunzi wanavyohisi na itakuwaje watakapohamia skuli mpya. |
| Andaa sera madhubuti ya kupambana na unyanyasaji na uhakikishe kuwa wale watu wazima wanaofanya kazi saa za mapumziko na chakula cha mchana, wanajulishwa iwapo kuna mwanafunzi mpya yeyote aliyewasili. | Wafunze wafanyakazi wote jinsi ya kuwasaidia wanafunzi mahitaji yao ya kihisia, kimaumbile na kitaaluma, kuwapatia nyenzo za mwongozo wanapoondoka au kujiunga na skuli. |
| Hakikisha kuwa vifaa, nguo na sare za skuli vinapatikana kwa wanafunzi kutoka familia maskini. | Wapangie michezo au shughuli wakati wa mapumziko au wakati wa chakula cha mchana. |

| | |
|---|---|
| Hakikisha kuwa, wanaowasili wanapewa majukumu mapema na kwamba wanashirikishwa katika shuguli pamoja na wanafunzi wa zamani, ikijumuisha shughuli za ziada kama vile michezo, vilabu, na uandaaji wa michezo ya skuli. | Wasikilize wanafunzi wapya wanaowasili na washauri wenzao. Panga mikutano na hakiki pamoja nao baada ya wiki chache za mwanzo. Wao ndio wenye ujuzi wa moja kwa moja kuhusu jinsi ya kufanya mabadiliko kati ya skuli na hivyo wanaweza kutuambia ni usaidizi gani wao na wengine wanaouhitaji. |
| Hakikisha kila mtu anajua wapi aende (hasa wakati wa mapumziko) ikiwa hajisikii salama. | Kadi tupu kwa washiriki kuandika mikakati ya ziada. |
| | |
| | |

# Kielelezo nambari 3.23: Ushauri wa Mipango ya Mpito wa Elimu – kutoka Nyumbani au Maandalizi kwenda Skuli ya Msingi

[Kutoka Daraja la Matumaini (2017) 'Mikakati ya kuimarisha mazingira ya mjumuisho wa/ujifunzaji kwa watoto. Ushauri wa mpito wa elimu kusaidia mpito mwepesi kutoka skuli ya maandalizi kwenda skuli ya msingi' https://bridgeofhope.am/wp-content/uploads/2018/02/Final-TransitionGuide_English-3.pdf]

Mipango bora inaweza kuhakikisha kwamba wanafunzi, familia, na walimu kujihisi wamesaidiwa vizuri kupitisha mpito kwa urahisi, kila mmoja anahitaji kupangiwa majukumu na hatua za kufuata kwa uangalifu.

- Upangaji wa mpito lazima uanze vizuri kabla mtoto hajaanza skuli ya msingi. Kwa watoto wasiohudhuria skuli ya maandalizi, skuli za msingi zinapaswa kutoa taarifa kwa wazazi au walezi kupitia ziara za wazazi au kupitia njia nyengine mfano vituo vya afya.
- Skuli iwe na taarifa sahihi kuhusu wanafunzi walioandikishwa kwa wakati kabla ya siku ya kuanza ili waweze kupanga.
- Watendaji wa skuli ya maandalizi waitishe vikao vya upangaji ndani ya skuli kujadili mahitaji ya ziada kwa wanafunzi na misaada wanayoihitaji.
- Skuli ya msingi imuweke mtu imara atakayewajibika kufanya mawasiliano na skuli ya maandalizi.
- Watendaji wa skuli ya msingi wapewe mafunzo sahihi kabla mtoto hajaanza skuli.
- Andalio la vitendo litayarishwe na skuli ya msingi kusaidia mpito rahisi. Andalio hilo lijumuishe ratiba ya vitendo vitakavyofanywa kuwawezesha watoto wote kushiriki.
- Andalio la mpito la mtoto litayarishwe kwa kila mwanafunzi ikiwezekana, hususan kwa wanafunzi wenye mahitaji ya ziada.
- Skuli ya msingi imuweke mwanafunzi mkubwa aliyepewa mafunzo ya kuwasaidia wanafunzi wapya awe muelekezi rika.
- Uangalizi baada ya wadahili ufanywe ndani ya miezi miwili baada ya kuanza skuli, umshirikishe mwanafunzi, mzazi au wazazi wake au walezi na mwalimu. Ukaguzi unaweza kufanywa katika hali ya kawaida kupitia mjadala baina ya mzazi au wazazi na mwalimu.

# Kielelezo nambari 3.24: Mafunzo ya Marafiki

## Vifaa vinavyohitajika

Chati mgeuzo au mfano wake; penseli ya kawaida, penseli za rangi, kalamu, kalamu rashasha, nakala za muongozo rafiki, picha, darasa lipangwe kwa ajili ya kazi ya vikundi.

Ni kwa namna gani mwalimu anapaswa kuanzisha utaratibu wa marafiki kwa wanafunzi? Elezea yafuatayo:

- Kipindi hiki kinakusudia kumuelimisha kila mmoja kuwa na marafiki kwa wanafunzi wapya darasani au skuli. Ni lazima wajengwe kuwa wamoja. Tukizingatia kwamba mara nyingi skuli inakuwa na wanafunzi wengi wanaohitaji msaada wa ziada wanapofika kwa mara ya kwanza.
- Pale mwanafunzi mpya anapofika, mwalimu wa darasa atapendekeza mwanafunzi mmoja au wawili kumkaribisha na kumsaidia na kuwa rafiki yake.
- Watabakia kuwa ni wenza wa wanafunzi wapya kwa kiasi cha wiki tatu baada ya hapo watahojiwa na mwalimu wa darasa.

Ikiwa mwanafunzi mpya anazoea kwa haraka, inaweza kuwa chini ya wiki tatu, Ikiwa mwanafunzi mpya anahitaji msaada baada ya wiki tatu, aina nyengine za misaada zitapangwa.

Mwalimu wa darasa asisitize kwamba ukaribishaji wa mwanafunzi mpya ni **wajibu wa kila mmoja.** Kila mmoja anatarajiwa kuwasaidia na kuwaunga mkono wote; mwanafunzi mpya na mwenza wake.

Katika mafunzo haya watazingatia kuhusu:

- Kukubaliwa.
- Yale yanayoendelea nyumbani, skuli na darasani yanaweza kufanana.
- Kile kinachoelekea kuwa ni kipya.

Pia wataandaa taratibu za kuzifanya wiki chache za mwanzo za wanafunzi kuwa ni za furaha wanapokaribishwa vyema, uwezo wa kutengeneza marafiki na kuendelea na kazi na maisha ya skuli kwa haraka.

Kitendo cha 1: Kufikiria kuwa mwanafunzi mpya
Watake wanafunzi wazungumze wawili wawili na waulizane ikiwa kila mmoja aliwahi kuwasaidia wanafunzi wapya katika skuli waliyopo au skuli aliyotoka. Aidha, watake waulizane ikiwa kila mmoja ilikuwa na jambo alilolifurahia au lenye shida na mengineyo. Watake watoe mrejesho ili kujadili kwa pamoja darasani. Utambue ujuzi wa wanafuzi katika ukaribishaji na usaidizi.

Wanafunzi baadaye wafumbe macho yao na wapige taswira ya nyumba zao, watu wanaoishi huko, wanavyovimiliki, jaalia kila kitu kipo kimya na tulivu. Watu wanaonekana kuendelea na maisha yao katika utaratibu wao wa kawaida.

Baada ya mapumziko, tangaza yafuatayo kwa haraka:

> "Ghafla watu na gari zinatokea na kila kitu kinatolewa nje ya nyumba yenu, vitu vyako vyote na vya familiya yako. Kila mmoja anaonekana kuwa na haraka, kelele na taharuki zimetawala. Unashindwa hata kuaga kama ambavyo, familia yako na vitu vyako vinachukuliwa vyote kupelekwa kuishi eneo tafauti".
>
> Sasa jenga taswira ya kufika katika nyumba mpya kwenye eneo jipya; kulala katika chumba usichokizoea, kuamka asubuhi, tayari kwenda skuli mpya. Safari yako ya kwenda skuli unapitia katika mitaa na njia usizozizoea. Unajihisi umechanganyikiwa.
>
> ''Sasa upo katika skuli yako mpya. Kila mmoja anapiga mayowe au kucheka; wapo wengine wanaonekana kufahamu wapi pa kwenda na kipi kinachoendelea''

Mwisho, wanafunzi wanaweza kufumba macho yao lakini ni lazima wajaribu na kuyashika mawazo yao juu ya kufika katika skuli mpya.

**Fikiria** mawazo haya na uyaandike ubaoni au kwenye chati.

## Kitendo cha 2: Msaada gani unahitajika?

Ligawe darasa katika vikundi vya wanafunzi 4 au 5 kila kikundi.

Vikundi vitabungua bongo kwenye karatasi za chati mgeuzo. Kwa mfano, kutumia ramani dhahania, **'mahitaji ya kusaidiwa mwanafunzi mpya'**. Vielelezo au michoro ikusanywe na ibandikwe kwenye darasa.

Wakati wa tendo hili mwalimu anaweza akaongeza matukio, mfano, itakuwaje ikiwa mwanafunzi mpya hawezi kuzungumza lugha kuu, au kujihisi anatamani nyumbani, au ana mahitaji ya ziada, au hatahudhuria skuli karibu mwaka nzima, au hajawahi kupata kwenda skuli kabla, au ni mwanamichezo hodari, anapenda kusoma, au ni mwenye aibu sana, na mengineyo.

## Kitendo cha 3: Kitabu cha Muongozo wa Rafiki

Watake wanafunzi wafanye kazi kwa makundi na wasome kupitia kitabu cha muongozo wa rafiki pamoja, baadae wajadili, wajibu maswali wakiona nukta walizozitoa katika kitendo cha pili ni sawa au tafauti, na wahakikishe maelekezo yamefahamika.

## Kitendo cha 4: Kutengeneza Bango

Mwisho, kitake kila kikundi kitengeneze bango, likijumuisha ujumbe mkuu uliopo katika kitendo cha 1, 2, na 3. Ili bango liweze kutumika likiwa ni kifaa cha kujifunzia na libandikwe maeneo ya skuli.

# Kielelezo nambari 3.25: Muongozo wa Rafiki

## Anachokifanya rafiki

Shukurani kwa kukubali kuwakaribisha na kuwasaidia wanafunzi wapya. Ni kazi muhimu sana unayoifanya.

Unaweza kuikumbuka siku yako ya kwanza katika skuli hii? Wengi wenu mliiona ni yenye kutisha. Baadhi yenu inawezekana mulifika katikati ya muhula na ikawa vigumu kujua wapi pa kwenda na nini cha kufanya. Jenga taswira kama huwezi kuzungumza lugha mama, au Kiingereza, au kuja kutoka skuli tafauti na hii.

Unaona namna ambavyo ni muhimu kumfanya mwanafunzi mpya ajihisi amekaribishwa na mwenye furaha. Hii ni kazi ya kila mmoja, lakini kwa wiki mbili za mwanzo inakuwajibikia wewe kwa mwanafunzi mpya kuanzia sasa.

Kwa sababu kazi yako ni muhimu utapata utambulisho kwa kazi hii. Tutaitaja kazi yako katika faili lako la maendeleo au ripoti ya skuli, ili utakapokwenda katika skuli nyengine au chuo au kutafuta kazi, watu waweze kuona kwamba unapaswa kupewa dhamana muhimu. Pia tutakupa zawadi kwa kazi yako njema kwa namna nyengine.

## Siku ya kwanza

- Kama utatakiwa uwe rafiki kwa wanafunzi wowote wapya, nenda katika ofisi ya skuli na uwaweke pamoja. Hakikisha umejitambulisha na kujua majina yao. Waelezee utakuwa ukiwaongoza.
- Watambulishe wanafunzi wapya darasani na kwa walimu. Hakikisha walimu wanatamka majina yao kwa usahihi. Kama hawaifahamu lugha mama, au, Kiingereza watambulishe kwa wengine wanaozungumza lugha zao (kama watakuwepo).
- Waoneshe wanafunzi wapya chumba cha ushuri nasaha kilipo, vyoo vinapopatikana, maktaba ya skuli, sehemu ya kula, maeneo ya michezo, na sehemu ya skuli wanayokusanyika wanafunzi.
- Wasaidie kuijaza ratiba binafsi. Waelezee taratibu muhimu za skuli.
- Kama wamo darasa unalosoma, waoneshe pahali pa kukaa kwa kila kipindi cha masomo. Watambulishe kwa walimu. Kaa nao karibu wakati wa mafunzo katika sehemu ya mbele. Ikiwa uko darasa tafauti mtake

mwengine ambaye yumo darasa moja kuhakikisha wanafahamu pahali pa kwenda.

- Hakikisha si wapweke wakati wa mapumziko na wakati wa chakula. Kama hawataki muungane pamoja, hakikisha wanafahamu kuhusu sehemu wanayokwenda, ikiwemo maktaba au shughuli za klabu.

## Baadhi ya maswali na majibu

**Je, ninalazimika kufanya vitu vyote ulivyoviorodhesha katika kitabu hiki?**
Haya yanategemea na hali, lakini utafanya yale ambayo mwanafunzi wako mpya anayahitaji zaidi. Jambo la msingi ni kwamba, unafanya kile unachodhani ni bora zaidi, kila ukipata uzoefu wa kukaribisha wanafunzi wapya.

**Itakuwaje ikiwa mwanafunzi mpya na mimi hatuendani?**
Kadri unavyowasaidia wanafunzi wapya pia unatakiwa uwe rafiki. Na uhakikishe wanazifahamu taratibu za skuli na pahali pa kupata msaada. Kwa hivyo, hakuna sababu za kuwa pamoja ikiwa hamuendani.

**Itakuwaje ikiwa mwanafunzi mpya hahitaji usaidizi zaidi?**
Wakati mwengine mwanafunzi mpya hahitaji msaada na hupata marafiki kwa haraka. Kwa hivyo utawaachia wakabiliane na maisha ya skuli mapema sana.

**Wakati gani nitamaliza kuwa rafiki wa mwanafunzi?**
Ndani ya wiki tatu. Wakati mwengine mwalimu wako atakuhoji baada ya hapo, kuelewa hali ilikwendaje na kujifunza kupitia uzoefu wako. Usisahau marafiki wengine darasani mwako au walimu wako kwa kila msaada utakaouhitaji.

# Kielelezo nambari 3.26: Kubali au Kataa

Nakili na kata seti (mkusanyiko) za kadi hizi kwa kila kikundi

| | |
|---|---|
| Wakatiwanafunzi wanajifunza lugha ni kawaida yao kukaa kimya kwa kipindi | Wanafunzi wanajifunza lugha kiurahisi zaidi kama hawahofu kufanya makosa. |
| Ni muhimu sana kupata fursa ya kuzungumza na kufanya kazi na wengine wakati wa kujifunza lugha mpya. | Ni muhimu sana kusahihisha makosa ya wanafunzi wanapojifunza lugha. |
| Wanafunzi wanajifunza lugha vizuri kwa kufanya mazoezi ya sintaksia. | Wanafunzi wanajifunza lugha kiurahisi zaidi wanapokuwa na mahitajio halisi ya kuwasiliana na watu wegine wanaozungumza lugha hiyo. |
| Mara tu wanafunzi wakiweza kuwasiliana kwa lugha ya kufundishia, hawahitaji msaada zaidi wa lugha. | Wanafunzi hawapaswi kutumia lugha yao ya msingi darasani. Wataifahamu wanapojifunza lugha ya kufundishia. |

# Kielelezo nambari 3.27: Msaada wa Lugha kwa Wanafunzi wapya– Baadhi ya nukta kwa walimu

## Kabla mwanafunzi mpya kufika

- Jaribu kujifunza kuandika na kutamka majina ya wanafunzi wapya kwa usahihi.
- Ijue lugha yao ya msingi na uzoefu wao wa kitaaluma walioupata kabla.
- Fikiria kuhusu makundi yatakavyokuwa ni msaada. Usiwaweke wanafunzi wapya katika vikundi vyenye uwezo mdogo.
- Wapange marafiki wa darasa watakaoweza kuwasaidia wanafunzi wapya kujua taratibu za skuli na kutengeneza marafiki.
- Wataarifu wazee wengine wanaolishughulikia darasa.

## Kumbuka

- Baadhi ya wanafunzi ambao ni wageni wa lugha kuu ya kufundishia (mfano, lugha mama, Kiswahili, Kiarabu, au Kiingereza) wanakuwa na aibu, ukimya na utulivu kwa mara ya kwanza wanapofika. Watakuwa wanajiweka sawa katika hali yao mpya na kuuweka usikivu wao kwenye lugha mpya. Katika hatua za awali za kujifunza lugha ya ziada, ukimya ni jambo maarufu na utulivu ni jambo la kawaida.

## Nukta kuhusu wakati anapofika mwanafunzi mpya.

- Fanya ukaribishaji mzuri
- Wape nafasi ya kutosha ya kusikiliza na kuzungumza katika kila kipindi cha masomo.
- Washajiishe wanafunzi wapya kuzungumza, kusoma na ikiwa ni waelewa wa hilo, waandike kwa lugha yao ya msingi wapate kuitumia elimu ya nadharia na kuthamini utamaduni wao. Jifunze namna ya kusema maneno machache kutoka lugha ya msingi ya wanafunzi wapya kama wewe si mzungumzaji wa lugha hiyo. Wafanye waelewe kwamba na wewe unafanya juhudi.
- Yahusishe maarifa na uzoefu wao wa zamani kuwasaidia kutumia maarifa yao darasani.
- Muweke mwanafunzi mpya na wanafunzi wenye huruma na wasaidizi. Ikiwa mmoja ndani ya kikundi chao anaweza kuzungumza lugha yao. Hilo litakuwa pia ni msaada kwao.

- Toa misaada mingi ya kuona. Kama vile vitu halisi, picha, ramani, michoro au vielelezo.
- Toa nafasi za kutosha kwa kazi za jozi na kazi za vikundi ili kukuza ujuzi wa kuzungumza.
- Tafautisha vitendo vya somo, endapo somo zima ni kusikiliza au kuandika
- Weka fursa kwa wasaidizirika au wazee wengine wa kuwasaidia wanafunzi wapya kuchangia na kushiriki kadri inavyowezekana.
- Hakikisha familia ya mwanafunzi mpya inajua taratibu za kusaidia kujifunza.

## Kielelezo nambari 3.28: Kadi za mapitio/tathmini

Nakili na ukate seti ya kadi hizi kwa kila kundi la mfano la skuli.

| | | | |
|---|---|---|---|
| Walimu wana matarajio makubwa kwa wanafunzi wapya wote na wamewaingiza katika makundi ya kujifunza ambayo yanawapa changamoto. | Tumepangilia wahitimu wetu kutembelea skuli au chuo chengine ili wafahamu mazingira, watu, na taratibu kabla hawajenda. | Wanafunzi wote wapya wanaona utamaduni wao, historia, na maarifa yanaonekana katika mtaala, na wanajua skuli inathamini tunu zao | Wanafunzi wapya waliofika katikati ya mwaka walitathminiwa mwanzo na maendeleo yao yanafuatiliwa, yanasimamiwa, na yanaangaliwa tokea hatua za mwanzo. |
| Wanafunzi wote wapya na familia zao wanakaribishwa, taarifa wanapewa zikiwa zimetafsiriwa pale inapolazimika. | Skuli ina kiunganishi imara na mawakala wengine na wahudumu wanaoshughulikia wanafunzi katika maeneo yanayohusika | Zipo taratibu za wazi za uandikishaji na upokeaji wa wanafunzi wapya na watendaji | Wazazi au walezi wapya wanaunganishwa na wazazi au walezi na kwa jumuiya ya wazazi na walimu na shughuli nyengine. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Walimu wanakutana na wazazi au walezi wa wanafunzi wapya na kujadiliana pamoja kuhusu maendeleo ya awali. | Watendaji wamepewa habari ya kutosha kuhusu historia, kujifunza kwa awali na utamaduni wa wanafunzi wapya. | Wanafunzi na wazazi au walezi wao wanashauriwa kuhusu uzoefu wa mpito wa elimu na mahitaji ya watoto wao. | Tunahakikisha wanafunzi wapya wanapata shuguli za ziada za kujifunza na matendo ya ubunifu. |
| Wanafunzi wanapewa muda kwa mchakato uliopo, kuangalia na kusikiliza mpaka wawe tayari kujiunga. | Watendaji wanafahamu mikakati ya kusaidia ujumuishi wa wanafunzi wapya. | Walimu wanatumia mikakati tafauti ili, kushajihisha na kuharakisha maendekeo kwa wanafunzi wapya. | Taarifa zilizotafsiriwa kuhusu skuli zinapatikana katika lugha kuu zinazotumiwa na jamii. |
| Watendaji wanajiamini kuhusu kuwahoji marafiki | Mtendaji wa skuli anaunganisha kupatikana kwa wanafunzi wapya | Walimu wana muda wa kuwapanga wanafunzi wapya wote na huwasiliana na watendaji wengine. | Tunawapatia msaada wa kuondokea wanafunzi wanaopaswa kuondoka mwanzo kabla kikosi chake hakijaondoka. |
| Matokeo ya mambo yaliyoanzishwa na skuli kwa wanafunzi wapya yanasimamiwa. | Ujumuishi wa wanafunzi wapya huingizwa katika mpango wa maendeleo ya skuli. | Je, Walimu wanawajua wanafunzi wahanga na mahitaji yao maalumu kutoka siku ya mwanzo na kuendelea? | Upo msaadarika kwa kila wanafunzi wapya. |

## Kielelezo nambari 3.29: Bango la Maendeleo Endelevu

Nakili kwenye karatasi ya chati (mlalo) kwa kila kikundi cha mfano cha skuli

**Tathmini maendeleo ya skuli kwa kuzingatia ukaribishaji na matayarisho ya wanafunzi wote wapya**

**Mambo tunayoyahitaji tunayoyafanya kuyaendeleza**

**Nusu ya safari hapa**

**Mambo vizuri**

# Kielelezo nambari 3.30: Mapitio ya maswali na vidokezo kwa kuisaidia skuli kujitathmini

**1. Tunafahamu hatua ya mpito wa mwanafunzi au mwenendo wa ndani na nje ya skuli na taarifa za wanafunzi wapya?**

- Kufuatilia na kutunza taarifa za wanafunzi wapya wanaoingia skuli.
- Kubainisha makundi yaliyo hatarini
- Upitiaji wa kawaida wa kuangalia mwenendo na taratibu za-kufika skuli.
- Taarifa nzuri za usuli wa mahitaji ya kilughawiya, kielimu na kiutamaduni kwa wanafunzi wapya.
- Uongozi wa skuli na timu ya utawala ziimarishe kujitolea kwa skuli kuwa mjumuisho

**2. Je, tunao mpangilio bora wa udahili na utambulisho wa wanafunzi wapya?**

- Makaribisho kutoka kwa Mwalimu Mkuu au Meneja Mkuu kwa wazazi au walezi na wanafunzi.
- Uendelezaji wa majukumu ya mratibu wa udahili na utambulisho.
- Utumiaji wa wakalimani inapobidi hivyo.
- Panga siku za kufanya usaili na siku ya kuanza masomo.

Taratibu za kusambaza taarifa darasani au kwa walimu wa masomo.

- Msaada wa mahitaji ya haraka yakiwemo mahitaji ya upatikanaji wa chakula na sare za skuli.

**3. Je, tunasimamia na kufuatilia jinsi wanafunzi wapya wanavyoishi skuli na kuwapatia msaada unaofaa kwa mwenye mahitaji maalumu?**

- Upimaji bora wa awali, kufahamu hatua za awali za kujifunza na kiwango cha ufasaha cha lugha ya kufundishia. Mfano, lugha mama au Kiswahili au Kiarabu au Kiingereza.
- Darasa na kundi analopelekwa yazingatiwe kwa makini na kufuatiliwa.
- Usaidizirika na urafiki.
- Mpango makini wa usimamizi kwa misaada iliyokusudiwa
- Muungano wa uongozi unaosimamia upatikanaji wa msaada kwa wanafunzi wapya waliotengwa, wakiwemo wanafunzi wenye mahitaji ya ziada.

**4. Tunayo mikakati imara ya kufundishia na kujifunzia ambayo inawawezesha wanafunzi wapya kushiriki kwa ukamilifu katika fursa za kielimu ambazo zitawafanya wapate matokeo bora ya kielimu na ya kijamii.**

- Kuhusisha maazimio ya kazi ili yaweze kufikia mahitaji ya mwanafunzi na wanafunzi kwenye makundi.
- Mbinu nyepesi za kuubadilisha au kuurekebisha mtaala.
- Kuwatambua wanafunzi wapya wenye vipaji.
- Mikakati ya kuzionesha tafauti katika matokeo ya kujifunza kutokana na changamoto za kujifunza' kidogo au kutokuwepo na taarifa zilizopita kabla.
- Tafauti kati ya utamaduni na lugha ya skuli unazingatiwa katika kupanga mtaala.
- Matumizi ya mkusanyiko na maonesho yataleta uelewa wa utafauti na kuimarisha usawa.
- Matumizi ya mbinu tafauti za kufunzia zinazosaidiwa na vifaa tafauti vya kujifunzia na vielelezo ambavyo vinalingana na mbinu tafauti za kufunzia.
- Upimaji makini wa kujifunza ambao unamsaidia mwanafunzi kujenga ufahamu wa anachokijua na kumsaidia mwalimu katika kupanga malengo sahihi ya kufundishia.
- Fursa za elimu zisiyo rasmi baada ya muda wa skuli.

**5. Tuna uhusiano mzuri na wazazi au walezi wa wanafunzi wapya; wakiwemo wenye mahitaji ya ziada?**

- Usimamizi na ushirikishwaji wa wazazi au walezi wa wanafunzi wapya 

  Utoaji wa taarifa zinazohusu skuli.
- Mpangilio wa mikakati ya mawasiliano na;
- Uanzishaji wa uhusiano baina ya skuli na jamii.
- Kutoa fursa za mafunzo kwa familia zitakazosaidia wazazi na walezi kuwasaidia na kuwajumuisha watoto kupata mafanikio katika skuli.
- Kuanzisha maendeleo ya uhusiano baina ya jamii na makundi ya kiroho.

# Kielelezo nambari 3.31: Kusaidia Mpito Jumuishi – Orodha ya dondoo kwa ajili ya Walimu

- ☐ Nimetayarisha vifaa na makundi ya kujifunza kuhakikisha mapokezi mazuri ya wanafunzi wapya na kuwajumuisha katika vitendo vya kujifunza.
- ☐ Watendaji wengine muhimu wa skuli watajumuishwa katika mpango wangu.
- ☐ Darasa limefahamishwa na wasaidizi wametambulishwa.
- ☐ Marafiki watatayarishwa, watasaidiwa na watatambulishwa rasmi.
- ☐ Nimesoma na nimejadili taarifa zinazopatikana katika mikutano ya udahili na tathmini ya mwanzo, na nimepanga kurekebisha mtaala ili ukidhi mahitaji ya wanafunzi wangu.
- ☐ Nafahamu kutamka jina la mwanafunzi, naifahamu lugha yake ya msingi na historia ya utamaduni wake na nimewatambulisha wanafunzi wengine darasani walio sawa na yeye.
- ☐ Nimekusanya nyenzo au vifaa kusaidia kufikia na kuwapokea wanafunzi kwa furaha.
- ☐ Nimekutana na mzazi au mlezi na nitawafahamisha kuhusu maendeleo ya awali nilipowaona.
- ☐ Nitahakikisha mwanafunzi wangu mpya anachanganyika katika makundi tafauti ya kijamiii, ajihisi yuko salama, na kwamba kuna taratibu nzuri na zinazotekelezwa dhidi ya unyanyasaji.
- ☐ Nitafuatilia kwa uangalifu maendeleo ya awali ya mwanafunzi wangu mpya.
- ☐ Nitakuwa ninaangalia ustawi wake baada ya muda wa mapumziko au chakula cha mchana.
- ☐ Nitakuwa ninasimamia mahudhurio na hapo hapo kushughulikia jambo au shida yoyote.
- ☐ Nitakuwa ninapitia maendeleo tukiwa na mwanafunzi na watendaji muhimu baada ya wiki chache za mwanzo.

# Rejea

Bennett, J. (2007). *Towards strong and equal partnerships*. In Moss, P. and Woodhead, M. (2007) (Eds) Early Childhood in focus 2 Transitions in the lives of young children. Milton Keynes: The Open University

Bridge of Hope (2017). 'Strategy to maximise the inclusive learning environment for children. Transition Guidance to Support Smooth Transition from Pre-school Institutions to Primary School' Accessed March 2018 https://bridgeofhope.am/wp-content/uploads/2018/02/Final-TransitionGuide_English-3.pdf

Dobson, J. M., Henthorne, K., and Lynas, Z. 2000 *Pupil Mobility in Schools Final Report.* London UCL

Evangelou, M., Taggart, B., Sylva, K., Melhuish, E., Sammons, P., and SirajBlatchford, I. (2008). *What makes a successful transition from primary to secondary school?* Department for Children, Schools and Families Research Report No. DCSF-RR019. London: DCSF

Galton, M., Gray, J., Ruddock, J. 1999. *The Impact of School Transitions and Transfers on Pupil Progress and Attainment*. London DfEE

Hirst, M., Jervis, N., Visagie, K., Sojo, V. and Cavanagh, S. (2011). *Transition to primary school: a review of the literature*, Commonwealth of Australia, Canberra. https://minerva-access.unimelb.edu.au/bitstream/handle/11343/123771/Transition-to-Primary-School-A-literature-review.pdf?sequence=1&isAllowed=y

Human Rights Watch, 2008 http://www.hrw.org/news/2008/12/03/facts-about-child-soldiers

Johnstone, C. (2010). *Inclusive Education as Part of a Child-Friendly Schools Framework: Results and Recommendations from a Study in Macedonia*. UNICEF.

Margetts, K. (2007). *Understanding and supporting children: shaping transition practices*. In Dunlop, A. and Fabian, H. (Eds) Informing transitions in the Early Years. Berkshire: Open University Press

Ministry of Education and Vocational Training Zanzibar (2017). *Zanzibar Education Development Plan II 2017/18 – 2021/2* Accessed February 2022 https://planipolis.iiep.unesco.org/en/2017/zanzibar-education-developmentplan-ii-20172018%E2%80%9320212022-6391

OPM 2016 Zanzibar Education Situation Analysis

The Revolutionary Government of Zanzibar (2006). *The 1985 Constitution of Zanzibar* Zanzibar: College of Education Press www.unesco.org/education/edurights/media/docs/668b626c6f075ceb43f5f7e843ae6fa6c3be324a.pdf
Accessed December 2021

Rice, F., Frederickson, N., Shelton, K., McManus, C., Riglin, L. and Ng-Knight, T. 2015 *Identifying factors that predict* findings *successful and difficult transitions to secondary school.* London UCL

Rifkin, S.B. and Pridmore, P 2001 *Partners in Planning – Information; participation and empowerment* Macmillan Education.

Spavoski, O., Ballazhi, S. and, Friedman, E. 2010 *Mapping Policies and Practices for the Preparation of Teachers for Inclusive Education in Contexts of Social and Cultural Diversity - Country Report - Former Yugoslav Republic of Macedonia.* European Training Foundation - A Report prepared by SCIENTER and Centre for Education Policy

Symonds, J. (2015), *Understanding School Transition: what happens to children and how to help them*. Routledge Education

UNESCO Institute for Statistics (2005). *Children Out of School: Measuring Exclusion from Primary Education*. Montreal: UNESCO Institute of Statistics. Accessed before June 2020
www.uis.unesco.org/Library/Documents/oosc05-en.pdf

UNESCO, *Education For All - Global Monitoring Report* 2010: p – 1 Accessed before June 2020
http://unesdoc.unesco.org/images/0018/001866/186606E.pdf

UNICEF, *UN Convention on the Rights of the Child in Child friendly Language* Accessed before June 2020
www.unicef.org/rightsite/files/uncrcchilldfriendlylanguage.pdf

UNICEF and UNESCO Institute for Statistics, 2011 Accessed before June 2020
www.unicef.org/education/files/OOSCI_flyer_FINAL.pdf

United Nations High Commissioner for Human Rights, (2005)
www2.ohchr.org/english/law/crc.htm

Werner, D. (cited in), Linney, B. 1995 *Pictures, People and Power.* London and Oxford: Macmillan.

Wils, A., Zhao, Y., and Hartwell, A. (2006). *Looking Below the Surface: Reaching the Out-of-School Children.* Collaborative Working Paper CWP-02-01. Education Policy and Data Center.